Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Pili – Tarehe 29 Oktoba, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

**Fedha za Kuhudumia Ofisi za Wabunge**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD (K.n.y. MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikuwa na utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuzihudumia Ofisi za Wabunge katika Majimbo au maeneo yao:-

(a) Je, katika mwaka 2001 hadi Juni 2008 Mkoa wa Pwani ulitengewa kiasi cha fedha na kila Wilaya ilipata kiasi gani?

(b) Je, katika hicho, Wilaya ya Mafia ilitengewa na kupokea kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kuhudumia Ofisi ya Mbunge?

(c) Kama haukutengewa fedha, Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutoa fedha angalau za ukarabati mdogo wa Ofisi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika,, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah Mbunge wa Mafia lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika,, ni kweli Serikali inao utaratibu wa kuhudumia Ofisi za Wabunge kupitia bajeti za Mikoa na baadaye kupelekwa katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Hii inatokana na ukweli kwamba Ofisi nyingi za Waheshimiwa Wabunge zipo kwenye majengo ya wakuu wa Wilaya.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika,, Ofisi ya Mbunge wa Mafia ipo kwenye jengo la Halmashauri ambalo lilikuwa linatumiwa na watumishi wa Hifadhi ya Bahari.

Katika kipindi kilichotajwa Mbunge wa Mafia amekuwa akihudumiwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa kukarabati ofisi yake kuwekewa samani na kulipia umeme.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika,, kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa dharura wa kutoa fedha kukarabati Ofisi ya Mbunge wa Mafia, badala yake kuna mpango wa mpatia Mheshimiwa Mbunge wa Mafia Ofisi bora zaidi katika jengo la Mkuu wa Wilaya ya Mafia ambalo kwa mwaka wa fedha 2008/2009 litafanyiwa ukarabati mkubwa na kiasi cha shilingi milioni 130 kimetengwa kwa ajili hiyo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, haileweki sasa utaratibu wa fedha hizi kupatikana kwa ajili ya Ofisi ya Wabunge na kwa sababu pia huwa hawajulishwi pesa hiyo inapokuwa inatoka.

Je, suala hili ni hisani au ni lazima?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shahidi hapa kwamba mwaka 2007/2008 kupitia Bunge lako hapa zilitengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge, na katika bajeti hii iliyopita zimetengwa tena shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge na yote haya ni kufuatana na maelekezo ambayo yamekuwa yanatolewa hapa na yale ambayo yametolewa kwa Serikali na sisi wote tumekuwa tunashughulika kwa ajili ya shughuli hiyo, nataka kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba kwa mwaka uliopita wa fedha shilingi bilioni moja zilizojengwa hapa zilikuwa zimekusudiwa kujenga Ofisi 32 kwa ajili ya Tanzania Bara na Ofisi 8 kwa ajili ya Tanzania Visiwani (Zanzibar).

Mheshimiwa Naibu Spika, *rate of inflation* imeonekana kwamba imetufikisha mahala ambapo milioni 25 zilizotengwa kwa ajili ya Ofisi za Wabunge kwa mwaka uliopita imepanda mpaka imefika milioni 40, kwa hiyo inaonekana kwamba ili kukamilisha Ofisi 40 zilizokusudiwa utahitaji kuchukua milioni 600 ambazo zimeingia katika hizi za sasa na kuzipeleka katika Ofisi za Wabunge za mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wote ambao wanahusika katika ujenzi wa Ofisi za Wabunge wamearifiwa kwa barua kuambiwa kwamba Ofisi zitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwambia Mheshimiwa Nyami kwamba suala hili siyo suala la hisani hili ni suala la wajibu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeamua kujenga Ofisi za Wabunge, Serikali haioni kwamba ingekuwa busara ianze kujenga Ofisi kwa Wabunge ambao hawana Ofisi badala ya kuwajengea na wale ambao wana ofisi katika majengo ya Wakuu wa Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema vigezo vilivyotumika ni pamoja ni hiki anachozungumza Mheshimiwa Mgana Msindai, Ofisi ambazo zinajengwa sasa hivi hazijengwi kwa wale Wabunge ambao tayari wanazo Ofisi katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya, sasa siwezi kujua vizuri analenga nini maana yake yeye ni Mbunge wa Iramba Mashariki najua pale Iramba zimetengwa kwa ajili ya Iramba Magharibi na yeye anatoka Iramba Mashariki, sasa siwezi kujua kwamba yeye ndiye ameachwa ndiyo maana ameuliza swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba Iramba najua imetengewa hela hizo na kigezo kilichotumika ni kupeleka pale ambako hakuna Ofisi kabisa hata zile ambazo haziko katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya, hata hivyo nitamwomba Mheshimiwa Msindai tukutane tuzungumze vizuri ili tuweze kujua hizi hela zimekwenda wapi, vinginevyo nitamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu ili tuweze kutafakari upya.

**NAIBU SPIKA:** Mnataka kuwagonganisha Wabunge, haya tunaendelea na Wizara ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Basil Mramba atauliza swali.(*Kicheko*)

Na.17

**Kujenga Kituo cha Forodha Holili**

**MHE. BASIL PESAMBILI MRAMBA** aliuliza:-

Kwa Serikali ina mpango wa kujenga kituo cha forodha *(Dry Port)* kwenye eneo la Holili- mpakani na Nchi ya Kenya:-

Je, ni lini mradi huo utaanza hasa kwa kuzingatia kuwa viwanja vinagawiwa kwa wawekezaji?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE-NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba Mbunge wa Jimbo la Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kujenga kituo kitakachotumiwa na Idara ya Forodha pamoja na Taasisi nyingine katika eneo la Holili umeshaanza na uko katika hatua yakuridhisha. Kwa sasa tunasubiri ruhusa (*No objection*) kutoka benki ya Dunia katika kuchagua mshauri mwelekezi wa mradi atakaye tayarisha michoro ya majengo, zabuni na kusimamia kazi ya ujenzi huo. Tunategemea Mshauri Mwelekezi wa mradi huu atakuwa amepatikana kufikia Januari 2009 na ujenzi utakamilika mwishoni mwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika,, eneo la sasa zilizopo ofisi za Idara ya Forodha na ulipo mpaka wa Kenya, ni kubwa na ndipo tunapotarajia kujenga ofisi hizo za kisasa za *One Stop Boarder Post*, kwa sasa mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya kazi ya kufuatailia upatikanaji wa hati miliki ya eneo hilo kutoka katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa maana hiyo, suala la ukosefu wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha forodha halipo.

**MHE. HAMZA A. MWINEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *dry port* ni muhimu sana katika nchi hii kutokana na ukubwa wake, na kwa kuwa pale Mbezi pana msongamano wa magari ambayo mara nyingine huwezi kujua yanafanya nini, kama ni *dry port* au Ofisi tu.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza kile ni kitu gani na kama ni *dry port* inaweza kutengenezewa nafasi kubwa kwa sababu inasababisha msongamano mkubwa sana pale?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu tulijibu swali ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kituo kile kilichopo pale Mbezi sasa hivi kinatumika *TRA* kukusanyia mapato kwa ajili ya magari makubwa na madogo yanayosafiri kwenda nje ya nchi lakini, lakini tukasema kwamba kituo kile ni cha muda, baada ya muda si mrefu utaratibu unafanywa ili tuweze kupata eneo jingine muafaka zaidi katika Wilaya ya Kibaha ambao utaratibu wa kushirikiana na Wilaya zinazohusika tutaendelea nao, kwa hiyo kile ni kituo cha muda lakini baada ya hapo tutapata eneo jingine muafaka zaidi.(*Makofi*)

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa vituo hivi vya kukusanya fedha ni vituo ambavyo vimewekwa miaka mingi iliyopita, na wakati huohuo kuna sehemu ambazo zimejitokeza lakini sisi kwa kukwepa tunaviita panya *root*?

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuangalia upya suala la vituo vipya ili tuweze kuondokana na hili suala la kuviita panya *root* wakati ni vituo ambavyo vingeweza vikatusaidia kukusanya mapato?

**NAIBU WA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni sahihi kabisa Serikali kuangalia vituo vipya ili tuweze kukusanya Mapato ya Serikali, nataka niseme tu kwamba panya *root* ni tofauti na kuangalia vituo vipya, panya *root* ni vituo ambavyo vinatumika na wananchi kuiibia mapato Serikali, kwa hivyo tutaimarisha ulinzi katika maeneo hayo ili watu wasiweze kukwepa kodi kupitia maeneo hayo.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunavyo vituo vingi vya ushuru, polisi vya kupimia magari katika barabara, kuanzia Dar es Salaam hadi Tunduma ni karibu vizuizi 24 na zaidi, wakati kuanzia Mombasa mpaka wa Uganda ni vituo viwili tu.

Je, hali yetu hii ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi au inaweza ikakwaza biashara? (*Makofi*)

**NAIBU WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Nataka niseme tu kwamba kuna vituo kwa ajili ya ushuku na kuna vituo kwa ajili ya ushuru na kuna vituo kwa ajili ya *check point* kwa ajili ya usalama wa nchi yetu na wananchi wetu, sasa nataka tuweze kutofautisha, kuna baadhi ya vituo ambavyo hivyo anavyozungumza Dr. Kigoda si vya Ushuru ni kwa ajili ya Usalama na vituo vya usalama tunalazimika kuwa navyo vingi zaidi ili tuweze kuona usalama wa Nchi hii na wananchi wake unaimarika.

Na. 18

**Jumla ya Fedha za Serikali na zisizo za Serikali**

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ipo dhana kuwa fedha nyingi zaidi zinamilikiwa na wananchi na makampuni kuliko zile zinazomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(a) Je, dhana hiyo ni kweli?
(b) Kama ni kweli, Je, taarifa za kiuchumi zinaonyesha tofauti hiyo kwa asilimia ngapi kati ya fedha za Serikali na zisiszo za Serikali kwa ujumla wake?

**MHE. JEREMIAH S. SUMARI-NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika,, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mbunge wa Jimbo la Tumbatu lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika,, ni kweli kuwa fedha nyingi zinamilikia na wananchi na makampuni, kuliko zile zinazomilikiwa na Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba mwaka 2008, Serikali ilikuwa inamiliki wastani wa shilingi trilioni 1.626 na shilingi trilioni 6.993 kumilikiwa na wananchi na makampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika,, kwa hiyo Serikali ilikuwa inamiliki asilimia 18.87 ya fedha zote za wananchi na makampuni kumiliki asilimia 81.13. Hivyo kuna tofauti ya shilingi trilioni 5.367 sawa na asilimia 62.27 kati ya fedha zinazomilikiwa na wananchi na makampuni na zile zinazomilikiwa na Serikali katika kipindi hicho cha mwezi Septemba, 2008.

Na. 19

**Utaratibu wa Kutoa Madawa ya Kilimo**
**na Mbolea ya Ruzuku**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID (K.n.y. MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, mara nyingi Serikali huwa inatenga fedha kwa ajili ya dawa na mbolea ya ruzuku ili kuwanufaisha wakulima; na kwa kuwa, katika maeneo mengi ruzuku hiyo haifiki kama ilivyokusudiwa:-

(a)Je, utaratibu ulioandaliwa katika kipindi cha 2008/2009 unatekelezwa vipi na Serikali imefuatilia kwa kiasi gani ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata ruzuku hiyo?

(b) Je, tangu bajeti ya mwaka 2008/2009 ipitishwe ni wakulima wangapi wamefaidika katika Wilaya zipi na wamepata mbolea kiasi gani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika,, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Maida Abdallah Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Kwa utaratibu wa zamani wa kutoa ruzuku ya pembejeo, Serikali ililipa fidia ya gharama ya usafiri kwa makampuni ya pembejeo za kilimo yaliyoingia mkataba na Serikali. Matatizo yaliyojitokeza katika utaratibu ni ifuatavyo:-

(a) Makampuni ya pembejeo za kilimo kushindwa kufikisha pembejeo kwa walengwa kwa wakati.
(b) Kuwepo kwa bei mbili kwenye soko (bei ya ruzuku na bei ya soko).
(c) Mbolea kutowafikia walengwa (wakulima wadogo).
(d) Mbolea ya ruzuku kuvushwa nje ya nchi.

Ili kukabiliana na matatizo haya, Serikali imebadili mfumo wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa kutumia vocha kuanzia msimu wa 2008/2009. matumizi ya vocha yataongeza ufanisi wa kutoa ruzuku ya pembejeo kama ifuatavyo:-

(i) Ruzuku itatolewa moja kwa moja kwa mlengwa (mkulima) badala ya makampuni ya pembejeo.

(ii) Itaondoa bei mbili za pembejeo (bei ya ruzuku na bei ya Soko) hali ambayo inatumiwa vibaya na mawakala wa mbolea wasio waaminifu.

(iii) Kuongeza ushindani kwa makampuni ya pembejeo kusambaza pembejeo kwa bei nafuu na kuongeza mtandao wa usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika,, baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:- (a)Utaratibu ulioandaliwa katika kipindi cha 2008/2009 unatekelezwa kwa kutoa vocha moja kwa moja kwa wakulima badala ya kulipa kwa makampuni kama ilivyokuwa hapo awali. Ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata ruzuku hiyo, Serikali imetoa elimu kwa viongozi kuanzia ngazi ya kijiji hadi Mkoa namna ya kuteua wakulima wanaostahili kupatiwa ruzuku ya mbolea na mbegu, kusambaza vocha na kusimamia matumizi ya vocha.

(b)Jumla ya wakulima 700,000 wanufaika na ruzuku ya mbolea na mbegu katika Wilaya zote za Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Kigoma na Wilaya ya Tarime (Mkoa wa Mara) na Sikonge (Mkoa wa Tabora) kiasi cha tani 155,00 za mbolea na tani 6,500 za mbegu zitatumika. Kiasi cha

mbolea ambacho wakulima wamepata hadi sasa katika maeneo hayo ni jumla ya tani 33, 720 za mbolea ambapo tani 5,900 ni *DAP* na tani 27,820 ni *MRP*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alizuru Mkoa wa Mbeya lakini pia alitembelea Wilaya ya Mbozi, tatizo kubwa ambalo wananchi walikuwa wanamwuuliza Mheshimiwa Rais na ambalo pia Wabunge wengi hapa Bungeni tumekuwa tunalizungumza ni uchahce wa mbolea ambayo inakwenda kwa wananchi wetu kwa mpango huu sasa wa vocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe kwa Wilaya ya Mbozi, wilaya ya Mbozi ina kaya takribani 120,000 lakini juzi tumetangaziwa kwamba wakulima watakaofaidika na mpango huu wa mbolea chini ya utaratibu wa vocha ni takribani kaya elfu hamsini, maana yake kaya 69,000 hazitapata mbolea.

Je, Mheshimiwa Waziri kwa mwendo huu kweli tumedhamiria kuondoa tatizo la njaa nchini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza takwimu elfu hamsini tu wa Wilaya ya Mbozi ndiyo watakaopewa mbolea inawezekana ikawa siyo sahihi kwa sababu Wilaya ya Mbozi ndiyo watumiaji wakubwa kabisa wa mbolea kuliko Wilaya nyingine kwa sababu ndiyo wanaolima mahindi kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa ni kweli kwamba katika Wilaya ya Mbozi nzima ni wakulima elfu hamsini ndiyo wanaopata mbolea naomba tuonane na Mheshimiwa Zambi ili tuweze kukubaliana na kubadilishana takwimu ili tuone ni kitu gani ambacho kimeharibika kule Mbozi tuweze kukirekebisha kabla ya mvua hazijaanza kunyesha.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeonesha nia njema ya kuendelea kuwapatia wakulima ruzuku ya mbolea kwa kuongeza bilioni 10 kwa mwaka 2008/2009 na kufikia bilioni 31 lakini bei ya mbolea imeongezeka sana hadi kufikia laki moja.

Je, Serikali kwa fedha zitakazotolewa za nyongeza kutokana na fedha za EPA inaweza kuzilipia gharama zaidi ya usafiri ili kupunguza bei hiyo ya mbolea na kuleta *impact?*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba Bunge hili limeipatia Wizara ya Kilimo shilingi 31.5

bilioni kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, wakati ule bei ya mbolea ilikuwa haijapanda sana katika soko la dunia, bei ya mbolea ilipanda kwa asilimia kubwa sana na kuifanya kwa mfano bei ya mbolea aina ya *DAP* ambayo ilikuwa inauzwa shilingi 35 mpaka elfu 40 ikafikia shilingi elfu 95-100,000, hivyo ni dhahiri kwamba shilingi 31bilioni zilikuwa haziwezi kutoa tena kiwango kile kile cha mbolea kilichokuwa kimekusudiwa na ruzuku ileile iliyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo moja ya sababu iliyomfanya Rais akaamua fedha za *EPA* zifanye kazi hii kwa sababu zile zilikuwa *eroded* na *inflation* kutokana na kupanda na bei ya mbolea, kwa hiyo fedha za *EPA* imeongezwa kwa mpango huu na sasa badala ya kutumia bilioni 31Serikali itatumia shilingi bilioni 68 kwa ajili ya kufidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango huo wakulima walio mbali zaidi kwa mfano kule Namtumbo watakuwa wanafidiwa zaidi kuliko walio karibu zaidi kwa sababu gharama yote ya usafiri itakuwa inafidiwa na Serikali na Mkulima wa Mbozi atalipa sawasawa na Mkulima wa Namtumbo.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, wakulima wote hapa nchini wana haki sawa na kwa kuwa ruzuku hii inakuwa inapangwa makundi makundi, kuna wakulima wa mikoa kama wa Kanda ya Ziwa hususani wakulima wa Bunda ambapo Mheshimiwa Waziri anatoka na Magu ambako mimi natoka, hii ruzuku hawajawahi kuiona wanaisikia tu.

Je, Serikali inampango gani wa kuhuisha suala zima la ruzuku kwa wakulima ili tuondokane na suala la umaskini kwa Watanzania wote?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakulima wote wana haki sawa lakini ni kweli vilevile kwamba mahitaji ya wakulima yanatofautiana kutoka mahali mpaka mahali, na kwa sababu hiyo tumetoa ruzuku kwa kuzingatia mahitaji ya maeneo mbalimbali.

Kwa mfano wakulima wa pamba mwaka jana wamepewa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya dawa inayotumika kwa ajili ya kuulia wadudu wa pamba, na wakulima wa kahawa wamepewa ruzuku ya miche, wakulima wa chai wamepewa ruzuku ya miche na wakulima wa korosho wanasaidiwa kupata ruzuku ya madawa ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia hivyo utaona karibu wakulima wote kwa namna moja au nyingine wameguswa na ruzuku, wakulima ambao hawana mazao ya kudumu kama mazingira ya katikati kwenye ukame.

Tunatoa ruzuku kwa mbegu za mtama ambazo zinastawi katika maeneo hayo, kwa hiyo ruzuku hii inaika isipokuwa inafika kwa kiwango tofauti kwa sababu mahitaji ya nchi ya chakula nayo ni makubwa inabidi yapewe umuhimu wa pekee.

Na. 20

**Faida kwa Wananchi wenye Mashamba yaliyoathirika na Dawa ya Kuua Magugu**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2006 mkulima wa kizungu aitwaye Lucas mwenye shamba la ngano West Kilimanjaro alinyunyizia dawa kwenye shamba lake kwa kutumia ndege; na kwa kuwa ndege hiyo ilipokuwa inazunguka ilimwaga dawa katika mashamba ya Wananchi na kusababisha mazao kufa na kusababisha njaa.

(a)Je, kwa nini mkulima huyo asiwelipe fidia wakulima hao ambao mashamba yao yaliharibiwa?

(b)Je, Serikali inasemaje kuhusu jambo hilo kwani licha ya ya wananchi kutoa malalamiko yao bado hawajapewa jibu lolote?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la *Mountainside* ambalo ni mali ya Kampuni ya Bia ya Tanzania *TBL* liko mpakani mwa Wilaya ya Siha na Longodo. Shamba hili linasimamiwa na bwana Luca Edwards ambaye ndiye mwekezaji mkuu kwa sasa. Miongoni mwa vijiji vinavyopakana nalo uapnde wa Magharibi ni Olmolog na Elerai. Mazao yanayolimwa na wanavijiji ni maharage, ngano, njegere na mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya tarehe 04 na 10 Disemba 2006 mwekezaji wa shamba la *Maountainside* alinyunyuzia kiunagugu aina ya *Touchdown* (*Glyphosate*) katika shamba hilo kwa kutumia ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tafiti mbalimbali athari za kiuagugu aina ya glyphosate hujitokeza baada ya siku 2 hadi 4 ambapo majani ya mimea huonyesha

rangi ya hudhurungi iliyopauka. Aidha baada ya siku 7 toka siku ya kunyunyiza *glyphosate* haina madhara kwa mimea iliyopandwa au kuota.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer Mbunge wa Longido lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuatia malalamiko ya wakulima wa *West Kilimanjaro* kuathiriwa na kiuagugu kilichonyunyiziwa na Bwana Lucas, Serikali iliunda kikosi kazi cha watalaam kutoka kituo cha utafiti wa viuatilifu (TPRI), Ofisi ya Kilimo Wilaya ya Monduli na Kituo cha Utafiti wa kilimo Selian. Tathimini hiyo ilifanyika 28/12/2006 hadi 06/01/2007 na ilihusisha viongozi na watendaji wa kata ya Olmolog na Elerai, wakulima, viongozi wa *Mountainside Farm Co. Ltd.* pamoja na Kampuni ya Bia Tanzania *(TBL).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tathimini hiyo ilibaini mambo yafuatayo:-

- Kiuagugu kilichotumika katika shamba la *Mountainside (Touchdown Glyphosate* hakikuonyesha madhara dhahiri kwenye mashamba ya wakulima waliolalamika mfano, kubadilika rangi kwa mazao ya wakulima.

- Baadhi ya mashamba ya walalamikaji yalionekana kunyunyiziwa kwa kutumia bomba la mgongoni (*knapsack sprayer)* au la mkononi *(hand sprayer)* kwa kuwa eneo lililonyunyiziwa lilikuwa jembemba na siyo pana kama eneo lililonyuziwa kwa kutumia ndege.

- Baadhi ya wakulima walikuwa wametumia kiuagugu aina ya 2- 4 – D *Amine* na *Bactril* katika mashamba ya ngano na siyo aina ya *touchdown* inayolalamikiwa.

- Pamoja na kuwa wakulima walisisitiza mashamba yao kuathirika, wakati wa tathmini asilimia kubwa ya mazao yalikuwa na hali nzuri licha ya siku saba kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo siyo rahisi kutamka Bwana Lucas kuwafidia wakulima. Viongozi na wakulima waliohusishwa kwenye tathmini hiyo walipewa maelezo ya kina kuhusu yaliyobainika na tathimini hiyo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri siyo sahihi kabisa, kwa sababu mimi mwenyewe ni shahidi nilikwenda kuangalia mashamba hayo na ni kweli yamekufa kwa ajili ya kunyunyiziwa hiyo dawa na mteja wa *Breweries* aliyolalamikiwa hiyo Tume iliyotumwa ilikwenda kwake walilala kwake, walikula kwake, walizunguka na gari yake. Kwa hiyo, nategemea kabisa kwamba wananchi hawawezi kupewa haki na

kwa vile wananchi hawakupewa haki na mashamba yaliyokufa mwaka huo ni mashamba hayo hayo yaliyonyunyiziwa dawa wakati mashamba mengine yamevunwa vizuri.

(a) Je, Serikali itasema nini kwa sababu hawa wananchi bado wanadai haki, hawakutendewa haki?

(b)Kwa kuwa mwaka huo hawa wananchi wamekosa mavuno na mwaka jana bahati mbaya mvua haikunyesha huko. Kwa hiyo wananchi hao wameshindwa hata kuwasomesha watoto na hawana chakula.

Je, Serikali itachukua hatua gani kuwapatia hawa wananchi chakula kwa sababu hawana wamekuwa maskini wa kutupwa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri huo ni ushahidi, (*first class* ushahidi) sasa unasemaje?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Laizer kama ifuatavyo:-

Kwamba kama majibu siyo sahihi hiyo nayo vile vile siyo sahihi. Siyo sahihi kwa sababu uharibifu unatokana na madai yanayotolewa lazima uthibitishwe kitalaam.

Haiwezekani kwa kweli kwenda kuangalia hivi kwa macho bila utalaam wowote ukasema hapa pameathiriwa na dawa ile. Ndiyo maana ilibidi kutumia watu ambao wamesomea fani hiyo kwenda kuthibitisha madhara yaliyotokea. Taarifa niliyoiwasilisha hapa inatokana na utafiti wa kitalaam. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Lakini kwamba walilala kwake, walikula kwake hiyo taarifa ndiyo naisikia haikuwepo katika taarifa ile ya uchunguzi. Kwa hiyo, nitazungumza na Mheshimiwa Laizer ili tujue walilalaje kule na walikulakulaje kule na kama ni lazima kufanya uchunguzi kwa kutumia vyombo vingine vya dola vyenye utalaam tofauti na jambo hili basi hivyo vyombo tutavikabidhi kwa sababu sasa wanazungumza habari ya rushwa zaidi kuliko uharibifu wa mazao. (*Makofi*)

Kuhusu swali la pili, la kukosa mavuno kwa sababu ya kukosa mvua na kusababisha kuwepo kwa upungufu wa chakula hilo ni suala tofauti ambalo hutokea katika maeneo mengi na sisi tumekamilisha tathimini ya hali ya chakula mpaka kufikia mwezi huu na tunaelewa maeneo ambayo yana upungufu wa chakula na kama eneo hili analolizungumzia Mheshimiwa Laizer litakuwa sehemu ya watu ambao wanaathirika na chakula Serikali itachukua hatua ya kuhakikisha kwamba kunapatikana chakula kwa bei nafuu. Wale wakulima ambao watakuwa hawakupata kabisa na hawana uwezo wa kununua tutawapa kama ambavyo tumefanya katika miaka mingine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 45 (3) inasema hivi, iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge. Swali hili naomba lijibiwe tena katika Kikao cha Bunge. (*Makofi*)

Na. 21

**Huduma ya Umeme katika Manispaa ya Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Singida inahusisha vijiji vya Mwankoko, Mtipa, Mungumaji, Mtamaa na Unyambwa na kwamba vijiji hivyo vinakua sana na kuhitaji Nishati ya Umeme kwa wingi na kwa kuwa vijiji hivyo havina nishati ya umeme hivyo kuathiri shughuli mbalimbali za Maendeleo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha umeme katika Manispaa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, vinakua kwa kasi kimaendeleo hasa kwa upande wa ufugaji, kilimo na biashara ndogondogo hivyo kuhitaji huduma ya umeme kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumtaarifa Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali kupitia Bajeti ya *TANESCO* katika mwaka 2008 itapeleka umeme katika kijiji cha Mtipa kwa gharama ya shilingi milioni 14. Kiasi hicho cha fedha kitatumika katika ujenzi wa njia ndogo ya msongo wa KV 0.4 yenye urefu wa kilomita mbili na ufungaji wa *transfoma* ya KVA 200. Wateja wa umeme 25 ikiwemo shule ya sekondari ya Mtipa, wataunganishwa. Kazi hii inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2008 au mwanzoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyobaki yaani Mwankoko, Mungumaji, Mtamaa na Unyambwa havimo kwenye Bajeti ya *TANESCO* ya mwaka wa 2008. Awali ilipendekezwa vijiji hivyo vipatiwe umeme kwa kutumia Bajeti ya *TANESCO* ya mwaka wa fedha wa 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya awali ya tathmini imefanyika. Kazi hiyo imebaini kwamba kwa sababu ya umbali wa vijiji hivyo na mahali ambapo nyaya za umeme zilipoishia wa kilomita kati ya 6 na 22, mradi huo utagharimu kiasi cha shilingi 1,908,573,681.09. Fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa njia kuu ya kuunganisha vijiji hivyo na gridi ya taifa, njia ndogo ya usambazaji umeme na uwekaji wa *transfoma.* Hivyo itajengwa njia ya umeme ya msongo wa kv 11 yenye urefu wa kilomita kumi kutoka *VETA* – Singida mpaka Kijiji cha Mwankoko, kilomita saba kutoka *Kititimo Mission* mpaka Kijiji cha Mungumaji, kilomita 22 kutoka *VETA* – Singida hadi Kijiji cha Mtamaa na kilomita sita kutoka *Kinyeto Mission* mpaka Kijiji cha Unyambwa. Transfoma mbili zitafungwa Mwankoko, mbili zitawekwa Mungumaji, moja itafungwa mtamaa na moja itawekwa Unyambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya kila linalowezekana ili kuongeza uwezo wake wa kugharamia miradi ya umeme. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuboresha ukusanyaji wa tozo kwenye mfuko wa nishati wa asilimia 3 kwa watumiaji wote wa umeme kama tulivyoeleza humu ndani ya Bunge lako tukufu.

Aidha, tunaendeleza mawasiliano na miongoni mwa taasisi, wahisani na nchi marafiki kwa lengo la kupata ufadhili wa miradi hii mikubwa. Kwa hivi sasa nchi yetu inatarajia kupokea ufadhili wa *ADB*, *MCC* Serikali ya Japan na Serikali ya Sweden katika baadhi ya miradi yetu mikubwa.

Lengo ni kupata ufadhili wa mifuko wa nishati vijijini kwa ajili ya kuwezesha miradi itakayotekelezwa chini ya *REA* kama ilivyo kwa miradi hii ya Mwankoko, Mungumaji, Mtamaa na Unyambwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini alifika Wizarani kwetu kufuatilia utekelezaji wa miradi hii, naomba kumpongeza kwa kazi yake. Aidha, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati Serikali kupitia Wizara yangu ikikamilisha upelekaji wa umeme katika kijiji cha Mtipa na pia mipango ya siku za usoni ya kuvipatia umeme vijiji vilivyobaki kwa utaratibu na mipango kama tulivyoeleza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri yenye mkakati mzuri wa kupeleka umeme katika vijiji vilivyoainishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa Mkoa wa Singida una maeneo mengi ambayo yana kero ya umeme, pamoja na makao makuu ya Tarafa ya Kilimatinde, Wilaya ya Manyoni, Makao Makuu ambayo yana taasisi nyingi za Serikali kwa mfano shule za sekondari mbili, hospitali ya *Mission* pamoja na ndani ya Hospitali kuna kitengo ambacho kinataka kutengeneza maji ya drip kwa ajili ya wagonjwa. Kitengo ambacho kikifanyika kitatoa huduma katika Mkoa wa Singida na Mikoa ya jirani.

Lakini kinashindwa tu kwa sababu ya umeme na kwa kuwa Meneja wa Mkoa wa Singida alitueleza kwamba umeme ulioko Manyoni una uwezo wa kupeleka umeme

Kilimatinde. Je, Serikali kwa umuhimu tu wa umeme katika Makao Makuu ya Tarafa ya Kilimatinde itaona umuhimu huo wa kutuletea umeme ili huduma hizi ziweze kufanyika kwa maslahi ya watu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Diana Chilolo haya makao Makuu ya Tarafa ya Kilimatinde na hasa suala hili la hospitali linakidhi kila vigezo vya kupata umeme hasa kwa sababu kuna hili suala la kuweza kutengeneza maji ya *drip* ambayo yatapunguza manunuzi ya nje ya maji hayo ya *drip* kwa ajili ya wagonjwa maeneo hayo.

Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Chilolo kwamba kupatiwa umeme Kilimatinde kinakidhi vigezo vyote ambavyo huwa tunatumia kuweka *allocation* ya *resources* kwa ajili ya mahitaji ya umeme maeneo mbalimbali. Naomba nimhakikishie kwamba tutafanya tathimini ya kutoa umeme Manyoni kwenda Kilimatinde na tutaangalia katika njia hizi mbalimbali ambazo tunaweza kuupatia ufadhili mradi huo kama ni kutoka wakala wa Nishati Vijijini ama kutoka njia nyingine ili hasa kukidhi mahitaji ya hospitali ile kubwa ambayo kweli inawapatia huduma Watanzania wengi wa maeneo hayo.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakati wa Kikao cha Bajeti Serikali iliahidi kwamba utekelezaji wa miradi wa *MCC* ya umeme ungeanza mara moja mwezi wa 10 mwanzoni ukiwemo ule mradi wa kupeleka umeme Ikonda katika Wilaya ya Makete. Lakini mpaka sasa hivi mwezi wa 10 unakwisha hakuna kilichotendaka. Je, Serikali inasema nini au inawaambia nini wananchi wa Makete kwamba utaanza kutekelezwa hiyo miradi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge kwamba miradi aliyoitaja iko chini ya MCC ambayo ni ufadhili wa Serikali ya Marekani ambao tumeahidiwa Serikali ya Tanzania mwezi Februari ambao una kadri ya jumla ya dola kama milioni 700 hivi na sisi tuna kama dola milioni 200 kwa ajili ya miradi ya umeme mbalimbali pamoja na miradi hiyo. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali ipo kwenye taratibu za kukamilisha ufadhili wa miradi hii ya umeme pamoja na miradi hiyo mingine naamini kwa hii miradi yetu ya umeme na tumeshajiweka kwenye mikakati ya utekelezaji kwamba mara tutakapopokea fedha hizi tunakamilisha utaratibu wa kuanza kutekeleza miradi hii ambayo kusema kweli utekelezaji wa miradi hii kwa muda mkubwa kwanza utaanzia katika ngazi ya Wizara mpaka itakapofikia hapo chini lakini tutaendelea kushirikiana naye katika kumfahamisha utekelezaji wa miradi hii ili naye awawasilishie taarifa wananchi wake.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kuongezea majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka kwenye swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu katika kuongezea ufafanuzi wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na wananchi kwa ujumla kwamba utekelezaji inayofadhiliwa na *MCC* umeshaanza na mkandarasi kwa maana ya *consultant* ameshapatikana katika ile mikoa 6 ya Tanga, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Iringa inaendelea na tunatarajia kwamba sisi kama Wizara

kupitia Shirika la *TANESCO* tutakuwa tunawaarifu Watanzania kwa kadri utekelezaji unavyoendelea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naona ni taarifa tu.

Na. 22

**Wananchi wa Kondoa Kuchimba Madini**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MHE. MASOUD A. SALIM)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumegundulika kuwepo kwa madini ya dhahabu katika kitongoji cha Maji ya Shamba jimbo la Kondoa Kaskazini na kwa kuwa wananchi walianza kuchimba madini hayo kwa zana duni bila kuathiri mazingira lakini Serikali ya Wilaya ya Kondoa imesitisha zoezi hilo:-

Je, ni lini Serikali itawaruhusu wananchi wa Kondoa kuendelea kuchimba madini hayo ili waende sambamba na dhana nzima ya MKUKUTA?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni 2008 wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu walivamia eneo la Kitongoji cha maji ya shamba na kuanza kuchimba dhahabu. Wananchi hao walifanya hivyo kinyume cha sheria ya madini ya mwaka 1998 kwani hawakuwa na leseni ya kuwaruhusu kufanya uchimbaji katika eneo hilo. Wakati uchimbaji huo unaanza, kulikadiriwa kuwepo wachimbaji kati ya 50 na 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya eneo hilo kuvamiwa na wachimbaji wadogo lilikuwa chini ya leseni ya utafutaji mkubwa wa madini wa awali *PRL* 3588/2005 ya Charles R. Rugabela iliyotolewa tarehe 21 Septemba, 2005. Leseni hiyo tarehe 6 Disemba 2005 ilihamishiwa kwenye kampuni ya JV *Mining Company Limited*. Muda wa leseni hiyo ulimalizika tarehe 20 Septemba, 2007.

Mheshimiwa NaibuSpika, kabla ya muda wa leseni hiyo haujamalizika kampuni mbili ziliwasilisha maombi ya leseni ya utafutaji wa mkubwa wa madini kwa ajili ya eneo hilo. Kampuni hizo ni Kampuni hizo ni *JV Mining Company Limited* na *Noble Azania Investment Limited*. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Madini ya mwaka 1998 maombi ya kampuni hizo mbili ambayo yaliwasilishwa wakati eneo hilo likiwa chini ya leseni hiyo hayakustahili kupewa leseni. Wachimbaji wadogo 14 nao waliwasilisha maombi ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini mwezi Julai 2008 wakati eneo hilo likiwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 11 Agosti, 2008 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilitoa tangazo kwa umma la kusitisha uchimbaji madini usiozingatia sheria kanuni na taratibu katika eneo la Maji ya Shamba na Munguri kuanzia tarehe tangazo lilipotolewa. Watu wote waliokuwa wakichimba katika eneo husika walipewa siku saba kuanzia siku ya tangazo kutolewa wawe wamesitisha shughuli zao na kuondoka katika maeneo hayo mara moja. Hatua hii ilichukuliwa ili kuepuka uvunjifu wa amani, uharibifu wa mazingira na upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, tangazo hilo lilieleza bayana kuwa uchimbaji madini utaendelea baada ya Sheria za Madini, Ardhi na Mazingira kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi walioomba leseni za uchimbaji mdogo wa madini katika eneo la Maji ya Shamba waliwasilisha maombi yao wakati eneo hilo likiwa halina leseni wanastahili kupewa leseni.

Aidha, msukumo huu wa kuwapatia wachimbaji wadogo maeneo ya kufanyia kazi kwa utaratibu unaotambulika kisheria unalenga kujenga misingi ya wachimaji wadogo kuwezeshwa kiuchumi. Wizara yangu inalifanyia kazi suala hili, ili kupata utekelezaji wa azma hii kwa mfumo endelevu na wenye ufanisi, kama tulivyoahidi wakati wa hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu, mwezi Julai mwaka huu. Leseni hizi zitatolewa kwa wachimbaji hao wadogo pindi utaratibu wa utoaji leseni utakapokuwa umekamilika.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa na tabia ya muda mrefu ya kuondoa wachimbaji wadogo wadogo pale wanapogundua madini na badala yake kuwaleta wawekezaji wakubwa kwa visingizio mbalimbali ambavyo mara nyingi huwa havina msingi.

(a)Je, ni lini sera hii ya ukandamizaji wa wananchi wanyonge ambao wanahangaika kila siku kutafuta angalau mlo wa siku ikasita?

(b)Kwa kuwa wananchi hawa waliotajwa ambao wamefika 150 walikuwa wameshaanza kuvuna madini. Je, ni lini matayarisho ya kuwapatia leseni wachimbaji hao yatakamilika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimsahihishe Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, si kweli kwamba pale ambapo wachimbaji wadogo wanapogundua madini Serikali mara moja inakuja kuwaondoa na kuwaleta wachimbaji wakubwa. Hilo si kweli.

Lakini la pili ni kwamba kwa sasa hivi Serikali inafanya mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba uchimbaji wa aina yoyote ile unaofanywa hauna athari za kijamii, wala za kimazingira kwa sababu kama ingewezekana Mheshimiwa Salim Hemed Khamis akaenda kwenye maeneo ambayo uchimbaji mdogo unafanywa bila kuzingatia sheria uhalibifu wa mazingira unaotokea pale ni wa muda mrefu sana hali ya kwamba baada ya

pale uchimbaji ukishapita miezi sita eneo lile linabaki na kusema kweli linakuwa halina matumizi endelevu au yenye manufaa kwa nchi hii kwa mambo ya baadaye.

Kwa hiyo, kinachozingatiwa hapo kusema kweli ni kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanapata uwezo wa kufanyakazi yao ambayo ni ajira yao ya haki lakini kwa kuzingatia maslahi ya taifa kwa upande wa mazingira na upande wa masuala ya kijamii.

Kwa hiyo, kusema kweli Serikali imeweka utaratibu tumeeleza wakati wa Bajeti kwamba tunafanya mkakati wa kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanafanyakazi yao katika utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi juzi kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini wiki mbili/tatu zilizopita nilikwenda kwenye maeneo ya Shinyanga Wilaya ya Kahama na Geita kwa makusudi maalum ya kuwahimiza wachimbaji wadogo wadogo wajiweke kwenye utaratibu huu wa makundi ili waweze kuwezeshwa na kupatiwa msaada wa Serikali. Lakini pia na taasisi zingine za kifedha kwa uwezo wa kuweza kukopesheka.

Na. 23

**Ongezeko la Vitendo vya Ubakaji**

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la baadhi ya wanaume wasiokuwa na huruma kuwabaka wanawake na watoto wadogo na hususani wanafunzi wa shule za msingi na kwa kuwa ongezeko hilo linaweza kuchangiwa pia na adhabu ndogo zinazotolewa kwa wanaopatikana na hatua hiyo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inaweza kudhibiti ongezeko hilo kwa kutotoa dhamana kwa watuhumiwa wa ubakaji na kuwapa vifungo vya maisha?

(b) Je, kwa nini sheria ya bodi ya *Parole* inatoa msamaha kwa wafungwa waliohukumiwa kwa makosa ya ubakaji?

(c) Je, Serikali inawaeleza nini wanawake wa Tanzania kuhusu hali hiyo kuwa wao ndio wenye majukumu mengi ya familia na uzazi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (a) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri kuwepo kwa taarifa za ongezeko la vitendo vya ubakaji katika jamii mbalimbali nchini mwetu. Serikali imeendelea kuzifanyia kazi taarifa hizo kwa kutumia vyombo mbalimbali kuhakikisha kuwa watuhumiwa wa makosa haya wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria na kushughulikia kwa mujibu wa sheria.

Ubakaji ni kosa la jinai lililoainishwa chini ya sheria ya Kanuni za Adhabu sura ya 16 toleo la 2002. Tuhuma ya ubakaji kama ilivyo kwa makosa yote ya jinai lazima ithibitishwe bila shaka na upande wa Jamhuri. Sambamba na hilo, kwa makosa ambayo sheria inaruhusu kutolewa kwa dhamana, basi dhamana ni haki ya mshtakiwa iwapo atakidhi matakwa ya sheria yaliyoainishwa kisheria. Kosa la kubaka ni mojawapo ya makosa ambayo mtuhumiwa anaweza kudhaminiwa kisheria.

Ieleweke kuwa haki ya dhamana siyo ya moja kwa moja, kwani katika kila kesi mahakama inayo mamlaka ya kuweka masharti ya dhamana au kuamua kutoa au kutokutoa dhamana kulingana na mazingira ya kesi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya *Parole*, yaani *Parole Boards Act Cap. 400 (R.E.2002),* chini ya kifungu cha 4(b) imeweka bayana kuwa mfungwa ambaye anatumikia kifungu cha miaka 4 au zaidi anaweza kuomba msamaha wa Bodi hiyo. Sheria inazuia mfungwa anayetumikia kifungo kwa kosa la kubaka kufaidika na *Parole*. Hivyo basi wafungwa waliohukumiwa kwa makosa ya ubakaji hawapati msamaha wa *Parole*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imelipa uzito suala zima la ubakaji, kwanza kwa kutambua kwamba suala hilo siyo tu linapingana na maadili ya jamii ya Tanzania, bali pia linapingana na misingi ya kimataifa ya haki za binadamu. Mbali na suala la uelimishaji wa haki za msingi zihusikanazo na kosa hili, kwa hivi sasa Serikali chini ya Tume ya Kurekebisha Sheria inasimamia zoezi la mchakato wa kuboresha na kurekebisha sheria husika ili kusimamia zaidi haki za walalamikaji ambao wengi ni wanawake na watoto. (*Makofi*)

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali langu la msingi limelenga hali halisi iliyojitokeza kwenye gereza mojawapo hapa nchini ambalo lilimwachia huru mfungwa wa kiume aliyehukumiwa miaka 15 kwa kosa la kumbaka mtoto wa kike wa miaka mitatu kwa kumchanachana sehemu zake za siri. Baada ya hukumu hiyo alitumikia miaka 2 tu mwaka 2007 Aprili akaachiwa kwa msamaha wa chini ya Sheria ya Bodi ya *Parole* ingawa Mheshimiwa Waziri amesema hakuna sheria ya namna hiyo. Lakini aliachiwa na mimi niko tayari kukutana naye nimpe jina la hilo Gereza na jina la Mfungwa.

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu sheria hii?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema sheria hii ikaondolewa ya kuwaachia huru wafungwa ambao wanahukumiwa kwa kosa la ubakaji kwa sababu linaleta uhasama kama wananchi na Serikali yao na inaumiza sana matumbo ya wanawake ambao ndiyo wazazi watoto wanaobakwa? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba katika swali lake halikutajwa Gereza hilo. Kwa hiyo, ilikuwa vigumu kuweza kufuatilia kesi hiyo. Namshukuru kwamba sasa atanitajia gereza hilo na mfungwa ambaye aliachwa baada ya muda. Kwa hiyo, suala hilo kama alivyozungumza yeye mwenyewe tutakaa atanipa jina la Gereza ili tufuatilie kwa karibu.

Swali la pili anazungumzia kwamba tufute sheria ya kuwachia huru, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba sheria ya *parole* haiwahusu kabisa wabakaji. Kwa hiyo, itaendelea kuwa wabakaji hawapati huruma ya *parole* hata kidogo hawatahusika kabisa. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja kama ifuatavyo:-

Wakati ambapo yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri alipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na wakati ambapo Mheshimiwa Bakari Mwapachu, alikuwa Waziri wa Sheria na Katiba niliuliza swali kama hili ili watuhumiwa wote wakishapata hatia ya ubakaji hasa watoto waliokuwa wadogo sana waondoshwe sehemu zao zote za siri jibu nililopata wakati ule niliambiwa haki za binadamu sasa je, ipi haki za binadamu kumharibu mtoto mdogo wa miaka mitatu akawa na kilema cha sehemu zake za siri akashindwa kutumia zake vilivyo pale anapobalehe.

Je, nani anaonewa zaidi *between* yule mtuhumiwa au mfungwa au yule mwingine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka ni kweli alileta ushauri huu wakati ule wa kuondoa sehemu za siri za yule ambaye ametenda kosa hilo. Lakini Mheshimiwa Sheria yetu haionyeshi kwamba tunaweza kufanya hivyo, kwa hiyo kwa vile tunafuata utawala wa sheria hatuwezi mahakama zinafuata zile adhabu ambazo zimo katika sheria.

Lakini pia ni kweli ni kinyume cha haki za binadamu na kwamba si vema baadaya huyu kufanya kosa na sisi tuvunje haki za binadamu eti kwa sababu yeye amemuondoa sehemu za siri na huyu mwingine aondolewe shemu za siri. Nadhani mpaka sasa tufuate sheria tutatumia sheria ambayo imetungwa na Bunge hili mpaka hapo Bunge letu litakapoamua kufanya hivyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri mazuri mimi nilikuwa na swali pia la nyongeza. Kwa kuwa, sheria ya mtu aliyeua anahukumiwa kunyongwa na je Mheshimiwa Waziri haioni sasa iko haja ya kuleta sheria hiyo hapa Bunge ili tuje tuikerebishe kwa sababu sheria iliyopo sasa hivi inawatetea wabakaji iletwe hapa ili tuje tuirekebishe wanaobaka nao wahasiwe? Asante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali lililotangulia ni bado ni Bunge hili ambalo linaweza kuamua kwamba wabakaji wanyongwe. Lakini nitoe tahadhari tu kwamba hata tukitoa masuala ya ubakaji matatizo yake yapo ndani ya jamii Serikali ilipotunga sheria ya wabakaji kufungwa maisha kesi za ubakaji zimezidi zaidi. Kwa hiyo kubwa kwamba sisi ndani ya jamii tujitahidi kuwaelimisha zaidi ili kusudi ubakaji upungue.

Lakini hata tukizungumzia masuala ya kunyongwa bado watabaka na ikumbukwe kwamba hivi sasa tukiwa na hii sheria kali wengi wabakaji kwa kuogopa kufungwa maisha wamekuwa wakiwauwa wale waliowabaka ili wapoteze ushahidi. Kwa hiyo mpaka kwa wakati huu mpaka hapao tutakapofikia masuala ya kuwanyonga wabakaji ambao tukumbuke nao pia wana haki zao watajitetea mpaka sasa tutatumia ile sheria ya kuwafunga kifungo cha maisha.

Na. 24

**Ukosefu wa Waganga na Wauguzi Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma unakabiliwa na tatizo sugu la ukosefu wa waganga na wauguzi kutokana na miundombinu mibovu ya Mkoa huo:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Kigoma kwa kuhakikisha kuwa waganga na wauguzi wanapatikana?

(b)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka *hardship allowance* kwa waganga na wauguzi ili iwe kivutio kwa watumishi mbalimbali kukaa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Kigoma pamoja na Mikoa mingine ya pembezoni inakabiliwa na tatizo la upungu wa watumishi kada mbalimbali za afya wakiwemo waganga na wauguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Serikali kusitisha ajira miaka ya 90 iliathiri hali ya upatikanaji wa watumishi nchi nzima ukiwemo Mkoa wa Kigoma. Aidha, masharti ya Sheria ya utumishi wa umma Na. ya mwaka 2002 kuhusu ajira, hususan sharti la kutangaza nafasi wazi na kusaili waombaji yalisababisha baadhi ya mamlaka za ajira kuendelea kukosa watumishi wakiwemo watumishi wa afya kutokana na mamlaka hizo kutokuwa na uwezo wa kutosha kushughulika masuala ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo mwaka 2006 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipata kibali cha kuwapangia vituo vya kazi moja kwa moja kwenye sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya watalaam wa afya.

Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita 2006/2007 na 2007/2008 Mkoa wa Kigoma ulipangiwa jumla ya watumishi wa afya 94 kati yao waganga wakiwa ni 26 na wauguzi 28. Aidha, kwa mwaka 2008/2009 Mkoa wa Kigoma umepata kibali cha kuajiri jumla ya watumishi 154 waganga wakiwa ni 30 na wauguzi 82. Pamoja na juhudi hizi za Serikali natambua kuwa baadhi ya watumishi wanaopangiwa vituo vya kazi ama hawaendi au hawakai kwa muda mrefu kwenye vituo walivyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kushirikiana na Halmashauri zao ili kuweka walau vivutio vichache (*incentives*) kwa ajili ya kuwavutia watumishi kudumu katika vituo walivyopangiwa.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, posho mbalimbali ikiwemo posho ya mazingira magumu zilijumuishwa pamoja ili kuongeza kiwango cha mishahara ya watumishi wakiwemo waganga na wauguzi. Hata hivyo, Wizara bado inaona kuwa utaratibu wa kuwa na posho ya mazingira magumu kama kivutio kwa watumishi kufanyakazi katika mazingira hayo ni muhimu. Wizara inaendelea kulishughulikia suala hili kwa kujadiliana na mamlaka husika. (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

**MHE. JOSEPHINE J. NGEZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili (a) na (b).

1. Kwa kuwa pamoja na Serikali kuwapangia waganga hao wachache wenye fani mbalimbali na wauguzi sehemu za kazi. Wengi hawafiki kabisa na hata wakifika kutokana na maeneo mengine ambayo yako mbali hayafiki kiurahisi wengine hukaa na kuondoka na kutokana tena na ukosefu wa nyumba waganga wanapotelekwa kule hawakai. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili haraka?

2. Kwa kuwa mazingira ya sasa ni muhimu kuwa na *hardship allowance* na kwa kuwa waganga na watumishi wengine wanastahili kupata hizo. Je, Serikali mna mpango gani kuweza kuharakisha kuweza kuwasaidia waganga hawa na watumishi ili waweze kuwa na moyo wa kuendelea kufanya kazi vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimesema katika jibu langu la msingi ni kweli kabisa kwamba wafanyakazi wengine waliondoka lakini nimesema kwamba waganga wengi na watumishi wengi kwa ujumla wanapokwenda katika maeneo husika mara nyingi huwa jukumu la kuwapati nyumba ni Halmashauri husika. Kwa maana hiyo ndiyo maana nikasema Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zetu ziandae utaratibu wa kuwapatia nyumba wafanyakazi hawa ili waendelee kwenda kukaa pale. Kwa hiyo ninapenda kutoa wito kwamba sisi kama wajumbe katika Halmashauri zetu basi tuhakikishe kwamba zinapojengwa Zahanati au kituo cha kutolea huduma yoyote ya afya na nyumba ya mganga au muuguzi iwepo pale ili hao wafanyakazi waweze kuendelea kubaki pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *hardship allowance* nimeshazungumza kwamba hapa mwanzo iliunganishwa ili kuweza kuhakikisha kwamba ule mshahara anaostafia mtumishi unakuwa ni mkubwa. Lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali inakaa kuweza kuona ni utaratibu gani kuona kwamba wanaweza kupata hii *hardship allowance* kama itawezekana. Kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri. Je, Serikali inaelewa kwamba baadhi ya hawa watumishi wa afya ambao wanapelekwa katika wilaya zetu huwa hawana sifa zinazohitajika na kwamba suala hili tayari liko katika Wizara yao na linatokana nini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Wizara yangu inapeleka wafanyakazi ambao hawana sifa katika maeneo husika sisi utaratibu unaokuwepo ni kwamba tukipata wale wataalam wanaokuja pale Wizara ya Afya kabla hatujawapeleka maeneo husika kwanza tunahakiki vyeti vyao na sasa hivi utaratibu uliopo ni kwamba vinahakikiwa mahakamani wanapoleta pale vimeshahakikiwa ndiyo tunawapeleka katika maeneo husika. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge ameona kwamba kuna mfanyakazi yoyote ambaye tumempeleka ambaye hana sifa au pengine amepelekwa kule tofauti na walivyoomba basi tunaomba tuonane ili aniambie ni wafanyakazi gani ambao tumewapeleka kule na kwamba hawana sifa tunaweza kuona tutayatatua namna gani.

Na. 25

**Maofisa Wanaoshughulikia Usafi wa Mazingira**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA (K.n.y. MHE. ATHUMANI SAID JANGUO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina Kitengo cha Afya kinachosimamia usafi wa Mazingira na kwamba maofisa wa Kitengo hicho walikuwa wakipita mitaani kukagua hali ya usafi na kwamba siku hizi ukaguzi huo haufanyiki.

(a) Je, Maofisa hao wamekwenda wapi?

(b) Je, ni nini jukumu la Serikali za Mitaa na Serikali Kuu katika usafi wa Mazingira?

(c) Je, Serikali haioni uchafu hasa mtiririko wa maji machafu ambayo inahatarisha maisha ya watu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu A, B, na C kama ifuatavyo:

Wizara yangu ina Kitengo cha Afya ya Mazingira kinachosimamia huduma ya usafi na afya mazingira. Maafisa Afya wanafanya kazi Makao makuu ya Wizara na katika Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na mitaa kwenye maeneo ya Mijini.

Majukumu ya Wizara katika masuala ya usafi wa mazingira ni kuandaa na kupitia mijini. Majukumu ya Wizara katika masuala ya usafi wa mazingira ni kuandaa na kupitia sera na miongozo mbalimbali, kufanya usimamizi na ufuatiliaji na kuhakikisha ubora wa viwango vinafikiwa.

Aidha, Wizara yangu pia inahusika na masuala ya Sheria zinazohusu Afya ya Mazingira. Utekelezaji wa Sera, Sheria na miongozo mbalimblai ni wajibu wa Halmashauri zote nchini. Baada ya kutoa utangulizi huu sasa napenda kujibu sehemu zote za swali la Mheshimiwa Mbunge yaani A, B na C kama ifuatavyo:-

(a)Maafisa wa Afya na Wasaidizi wao hufanya kazi za ukaguzi wa mazingira katika Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji, Wilaya, Kata na Vijiji na wanapokibaini chukizo huchukua hatua kwa kutumia Sheria za Afya. Hata hivyo, kuna uhaba mkubwa wa watenda kazi katika Sekta ya Afya. Upungufu huu ni pamoja na maafisa wanaojishughulisha na afya ya mazingira katika ngazi ya kata na Wilaya.

(b)Kama nilivyosema katika utangulizi wangu ni kwamba, majukumu ya Serikali Kuu ni kuandaa na kupitia Sera, mwongozo, ubora wa viwango vinafikiwa na kufanya ufuatiliaji na usimamizi. Aidha, Serikali pia hushirikiana na vyombo na taasisi mbalimbali. Majukumu ya utekelezaji na kuhakikisha kwamba huduma za usafi wa

mazingira inatekelezwa katika kiwango cha kuridhisha ni la Halmashauri zote nchini. Serikali za Mitaa mijini zina kamati za afya mazingira na vijijini zina kamati za afya wakiwemo wahudumu wa afya msingi ambao hushiriki kwenye kupanga na kusimamia mipango ya usafi wa mazingira, kuelimisha jamii na kuandaa sheria ndogo ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

(c)Serikali inatambua huduma za usafi wa mazingira kwenye halmashauri nyingi haitolewi kwa kiwango kinachorishana kutokana na sababu kuu zifuatazo; kuwepo kwa uhaba mkubwa wa watumishi wa Sekta ya Afya, ujenzi holela, usiozingatia mipango miji, biashara holela zinazoongeza uchafuzi na ongezeko kubwa la watu katika miji.

Ili kuondoa kero ya uchafuzi, kwa mfano mtiririko wa maji machafu halmashauri zote nchini ziweke mipango bora na kusimamia uekelezaji na kutenga fedha za kutosha ili kutekeleza mipango yao. Halmashauri zitumie pia sekta binafsi na asasi za kijamii kutoa huduma hizi. Halmashauri ziimarishe ufuatiliaji na usimamizi katika utekelezaji. Aidha, wananchi waelimishwe umuhimu wa kulinda mazingira yao kwa kutoyachafua kwa taka kwa makusudi.

Halmashauri ziombe vibali vya ajira za Maafisa Afya na Maafisa Afya Wasaidizi, ili waajiriwe kukidhi mahitaji ya kila kata na vijiji, kama Sheria inavyoelekeza ili kukidhi mahitaji ya ukaguzi na uchukuaji wa hatua za kisheria kwa wanaokiuka kamuni, taratibu na sheria. Ili kufanikisha utendaji kazi wa Maafisa hawa Halmashauri zote ziandae vitendea kazi iil kuwezesha maafisa hawa kutekeleza majukumu na kazo zao.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri niulize swali moja kama ifuatavyo:- Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba baadhi ya Halmashauri au Halmashauri nyingi hazitekelezi wajibu wake katika kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, katika vyombo vya habari mara kwa mara kumekuwa na malalamiko ya maji machafu kufurika ovyo. Wananchi wanalalamika sana kwamba Halmashauri zinashindwa kufanya hivyo kutimiza wajibu wake. Je, Serikali kuu inachukua hatua gani kuona kwamba mazingira yanatunzwa sawa sawa na wananchi wanapata afya safi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malalamiko la kutiririsha maji machafu ovyo inatokana na mipango ambayo haiko sahihi katika miji yetu. Lakini Serikali sasa hivi inaandaa utaratibu ambao utaleta Muswada ambao utazungumzia afya ya jamii na katika Muswada huo ndiyo utazungumzia nini kitafanyika kwa wale ambao watakuwa wanakiuka masuala yote haya ambayo wanachafua mazingira. Kwa hiyo, naomba wakati tukisubiri hii wakati Muswada utakapopita katika Bunge lako Tukufu ndiyo hapo sasa kutakuwa na marekebisho mengi ambayo yatajumuisha na ile Miswada au Sheria ambazo zina mapungufu tutaweza kuwakaba wale ambao wanavunja utaratibu huu.

Na. 26

**Mvua za Kutengeneza**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR (K.n.y. MHE. KIDAWA HAMID SALEH)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikikumbwa na janga la ukame kila baada ya muda na kuathiri sekta nyingi ikiwemo ukosefu wa umeme wa kutosha:-

(a) Je, Serikali itatekeleza lini mpango wa Mvua za kutengeneza kwa kutumia utaalam kutoka *Thailand*?

(b) Je, wananchi wategemee mvua hizo zitanyesha lini hapa nchini ili kusaidia kuondoa ukame?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukabiliana na tatizo la ukame linaloikumba nchi yetu mara kwa mara, Serikali ilijaribu kufuatilia utalaam wa teknolojia ya kurutubisha mawingu na kutengeneza mvua. Katika kufuatilia utalaam huo, Serikali ya Tanzania ilifanya mazungumzo na Serikali ya Thailand ili iweze kusaidia Tanzania katika utalaamu wa kutengeneza mvua kwa kurutubisha mawingu kwa lengo la kuondokana na tatizo la ukame katika nchi. Hii ilitokana na ukweli kwamba Thailand ni moja kati ya nchi zenye utalaam wa hali ya juu katika tenkonojia ya kurutubisha mawingu na kutengeneza mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam kutoka Thailand waliwasili nchini mwezi Septemba, 2007 na kufanya mazungumzo na watalaam wa Tanzania na kutembelea baadhi ya maeneo ambayo zoezi la kurutubisha mawingu lililenga kufanyika kwa majaribio. Serikali pia iliteua Kamati ya watalaam na kuitaka ifanye uchunguzi juu ya gharama za zoezi hilo na athari zake katika mazingira.

Baada ya uchunguzi huo gharama za zoezi hilo zilionekana kuwa kubwa na pia rasilimali nyingi zilikuwa zinahitajika ili kufanya mradi huu kuwa kubwa na pia rasilimali nyingi vilikuwa zinahitajika ili kufanya mradi huu kuwa endelevu. Aidha, athari za matumizi ya aina hii ya mvua katika mazingira ya nchi yetu ilionekana kuwa bado kufanyiwa utafiti wa kutosha. Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo Serikali ilisitisha zoezi hilo na kwa hiyo wananchi kwa sasa wasitegemee upatikanaji wa mvua za kutengeneza kwa kurutubisha mawingu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwanza Mheshimiwa Waziri kwa jawabu zake lakini na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa wakati akijibu swali mama alisema kwamba kuna rasilimali nyingi zingetumika kama uamuzi huu ungefanyika anaweza kuliambia Bunge hili ni Rasilimali gani hizo ambazo zingeleta athari.

Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba hivi majuzi tu katika mlima Kilimanjaro kulitokea moto na kunaendelea kutokea moto kila baadhi ya wakati na kuleta athari kubwa katika mlima huu ambao ni kigezo na kielelezo cha nchi yetu Tanzania, MheshimiwaWaziri haoni bado kuna haja ya kufikiria zaidi hasa katika sehmu zile katika suala hili la kutengeneza mvua ili kupunguza moto katika sehemu zetu mbalimbali hasa katika Kilimanjaro?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali nilizokuwa ninazilenga katika kujibu swali la msingi hapa ni rasilimali ambazo zilikuwa zinatakiwa ziweze zikatumika katika kuyaunganisha hayo mawingu ili yaweze yakatengeneza mvua. Mali hizo ndiyo nimesema kwamba zina gharama kubwa kiasi ya kwamba isingewezekana kwa rasilimali tulizonazo zikaweza tukazielekeza huko kuliko kuweza kutumia katika kutekeza miradi mingine.

Sasa katika hili la kupamba moto Kilimanjaro unatokea na hali hiyo ya kuhitaji tuwe na mvua za kutengeneza kwa mawingu nimesema kwamba Serikali iliona umuhimu huo ndiyo maana ikaona kwamba ifuatilie ione kama uwezekano upo.

Kwa hiyo kama uwezekano huo ungekuwa umekubalika na unawezekana hilo lingeweza likatekelezwa lakini kwa hivi sasa kama nilivyokuwa nimesema unaonekana kwamba mradi huo sasa hivi ni mgumu na kwa hiyo kwa sasa hivi tuweze tukawa na subira pengine hapo baadaye miaka inayokuja kama kutakuwa na haja hiyo tutaliendeleza zoezi hilo.

Na. 27

**Huduma ya Maji Tarafa ya Pande**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. HASNAIN GULAMABAS DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa ina matatizo makubwa ya maji hususani katika Tarafa ya pande:-

Je, kuna mpango gani wa kuvipatia maji safi vijiji vya Limaliyao, Ruyaya, Kisongo, Namakongoro na Pande-Namwedo na mradi wa *Quick win?*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imechagua Vijiji Kumi. Kijiji cha Limaliyao ni moja ya Vijiji hivyo. Hivi sasa, zoezi linaendelea kupata mtaalam mshauri ambaye atasaidia Halmashauri kusanifu mradi wa Limaliyao na vingine tisa na kusimamia ujenzi ambao utafanywa na mkandarasi atakayeteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ambapo mchakato wa kupata mataalam mshauri unafanyika, utekelezaji wa programu unaendelea katika Kijiji cha Ruyaya, ambapo mwezi Juni, 2008 Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ilipewa shilingi 103,951,000. Kati ya hizo, kiasi cha shilingi 44,475,500 kimetengwa kwa ajili ya mradi wa maji katika kijiji cha Ruyaya.

Kisima kirefu kitachimbwa na mradi wa maji ya bomba kuanza kujengwa. Mahitaji ya fedha zaidi ya kukamilisha mradi yatajulikana baada ya kisima kuchimbwa na usanifu kufanyika. Katika kijiji cha Namakongoro, kisima kirefu kilichimbwa mwezi Mei, 2008. Maji yaliyopatikana ni kidogo; kisima kingine kitachimbwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001, kisima kirefu kilichimwa na mradi wa maji ya bomba kujengwa katika kijiji cha Pande-Ploti kwa msaada wa fedha (*grant*) kutoka Serikali ya Japan (kupitia Shirika la *Japan International Cooperation Agency*). Mradi huo unafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009, kiasi cha shilingi 31,225115 zimetengwa kupitia Tanzania *Social Action Fund (TASAF)* kwa ajili ya mradi wa maji ya Kijiji cha Namwedo. Hivi sasa, maandalizi yanafanyika ili kupima eneo la kuchimba kisima kirefu. Upimaji utafuatiwa na uchimbaji wa kisima, usanifu na ujenzi wa mradi wa maji ya bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 4091,168,000 kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira wilayani kilwa. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 105,004,096 zimetumwa tayari. Vipao mbele za mradi hupangwa na Halmashauri yenyewe kwa

maana hiyo kijiji cha Kisongo kinaweza kikaingizwa katika utekelezaji wa programu ya maji vijijini Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nilizoeleza ni juhudi za Serikali za kutatua tatizo la maji katika wilaya ya Kilwa, hususan katika Tarafa ya Pande.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya ya Kilwa imepakana na wilaya Lindi, Lwanga na Nachingwea na Wilaya hizi zote zipo katika mkoa mmoja na wilaya ya Kilwa na wilaya hizi zote zina matatizo hayo hayo sawa ya maji. Sasa wilaya hizi zina miradi ile ya *Quick wins* pamoja na mradi wa *World Bank* sasa nilitaka kufahamu tu kwa ujumla kwamba hii miradi ya *Quick Wins* na *World Bank* inaendeleaje?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkoa wa Lindi kati ya mwaka 2007/2009...…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi kabisa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Fedha zifuatazo zimetumwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *Quick Wins*, wilaya ya Kilwa zaidi ya milioni 900, Nachingwea zaidi ya milioni 800, Liwale zaidi ya milioni 400, Lindi vijijini milioni 600, Lindi mjini milioni 250, Narwangwa milioni 473.

Kwa hiyo, ni fedha nyingi ambazo zimetumwa na zinaendelea kutumika kwa ajili ya *Quick Wins*, kwa upande wa ule mradi unaojulikana kama mradi wa Benki ya Dunia yaani vijiji 10 taarifa nitaitoa hivi karibuni kuhusu utekelezaji wa mradi huu kwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na mkoa wa Lindi.

Lakini tumefika mahali pazuri na niseme tu kwa mkoa wa Lindi nahisi hii wilaya ya Liwale itimize masharti haraka iwezekanavyo.

Na. 28

**Ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Bahari-Zanzibar**

**MHE. USSI AME PANDE** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari unaoendelea huko buyu Zanzibar unasua sua; na kwa kuwa Serikali inaweza kupata hasara endapo mkandarasi husika atakwenda kwenye vyombo vya sheria.

Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili hasa pale iliposhindwa kutoa dhamana ya mkopo kutoka *CRDB Bank* kwa ajili ya kumalizia ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari, sehemu ya Buyu Zanzibar, ulianza Machi, 2006. Hadi kufikia mwaka wa fedha 2007/2008 awamu ya kwanza ya ujenzi huo ilifikia ngazi ya kukamilisha msingi na kuweka jamvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali haikutoa dhamana ya mkopo kutoka *CRDB Bank.* Hata hivyo Serikali imekuwa ikiendelea na ujenzi huo kupitia Bajeti ya Maendeleo (*Capital Budget*) kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Katika mwaka wa Fedha 2007/2008 kiasi kilichotolewa kwa ujenzi huo ulikuwa shilingi za Tanzania 1,000,000,000 (Bilioni moja) na mwaka 2008/2009 ujenzi wa chuo hicho umetengewa shilingi 1,212,000,000/= (bilioni moja na mia mbili kumi na mbili milioni).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Ussi Ame Pandu Mbunge wa Jimbo la Mtoni kwamba ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari sehemu ya Buyu Zanzibar utaendelezwa na fedha zitakazotengwa katika bajeti ya Serikali mwaka hadi mwaka.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ujenzi huu huwa unaenda kwa kusuasua nilitaka kujua kwa mujibu wa mkataba ujenzi huo ulikuwa unamalizika lini?

Kama muda wa mkataba utakuwa umekwisha. Je, haoni Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa kuna haja ya kutafuta fedha mbadala kwa ajili ya kumaliza ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu ulikuwa unamalizika sina hakika lakini nafikiri ndani ya kama 2010.

Lakini ukweli ni kwamba pamoja na kwamba unasua sua sisi tutaendelea kuzungumza na mkandarasi kusudi Bajeti au pesa zinazotengwa kila mwaka katika Bajeti ziendeleze jengo hili.

Hadi sasa taarifa tulizonazo kwa mwaka huu wa fedha lile jamvi sasa hivi ukuta umeshaendelezwa umefikia nusu na sidhani kama mkandarasi atatupeleka mahakamani kwa sababu tutaendelea kuwa na maongezi naye kama tunavyoendelea kila mara.

Na. 29

**Ongezeko la Kampuni za Simu za Mikononi**
**na Madhara Yake**

**MHE. MUHAMMAD A. CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na ongezeko la Kampuni ya Simu hapa nchini; ambazo kwa namna moja zinaharibu mandhari ya miji yetu kwa kujenga minara mingi mahali pamoja:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni vema kampuni hizo zikatumia mnara mmoja kwa kushirikiana, badala ya kila Kampuni kujenga mnara wake?

(b) Je, ni Watanzania wangapi wameajiriwa kwa kila Kampuni hizo za simu?

(c) Je, ni kiasi gani cha kodi kilicholipwa na kila kampuni kwa *TRA* kutokana na mapato ya barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge umuhimu wa Makampuni ya Simu kushirikiana katika kutumia mnara mmoja badala ya kila kampuni kujenga mnara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, ndio maana Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imekuwa ikiendelea na jitihada za kuwashawishi wenye makampuni hayo kushirikiana katika ujenzi na matumizi ya minara, ili kupunguza gharama za ujenzi, uendeshaji na pia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi hizo tayari yapo Makampuni ya Simu ambayo yanashirikiana katika matumizi ya minara, nayo ni *Vodacom* na *Zantel*. Ushirikiano huu ni maamuzi yao binafsi na si ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliona hilo, Serikali inajipanga kuleta mapendekezo mbalimbali Bungeni yakiwemo ya kurekebisha sheria za mawasiliano ili kuweka matakwa ya utaratibu wa kushirikiana minara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Watanzania walioajiriwa kwenye kampuni za simu za mikononi ni kama ifuatavyo:-

(I) Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) watu 1694.
(II) Kampuni ya Simu ya *Zain* watu 790.
(III) Kampuni ya Simu ya *TIGO* watu 260.
(IV) Kampuni ya Simu ya *Vodacom* watu 620.
(V) Kampuni ya Simu ya *Zantel* watu 560.

(c) Katika kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 hadi 2007/2008 Makampuni ya simu yalilipa kodi kiasi cha shilingi 576.7616 Bilioni kama ifuatavyo:-

(I) Kampuni ya Simu ya *TTCL* ililipa Tsh.97.4917 bilioni.
(II) Kampuni ya Simu ya *TIGO* ililipa Tsh.81.6309 bilioni.
(III) Kampuni ya Simu ya *Vodacom* ililipa Tsh.210.4865 bilioni.
(IV) Kampuni ya Simu ya *Zain* ililipa Tsh.187.1525 bilioni.

**MHE. MOHAMMED A. CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake yameonyesha kwamba kuna Kampuni ya *Zantel*, sikuona kodi yake waliyolipa kwa kipindi cha miaka mitano.

Je, Kampuni hii imelipa kiasi gani na kama imelipa, imelipa wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi

na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Chomboh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli niliiacha Kampuni ya *Zantel*, Kampuni ya *Zantel* inalipa kodi zake *TRA* kama makampuni mengine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umeisha na maswali yenyewe yameisha.

Matangazo, kwanza tunao wageni wafuatao, wageni tuliona Bungeni leo wako wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Musoma ambao ni bwana Antony Warioba Nyakimori na Bwana Joel Kamanjo, mkwe wake, karibuni sana.

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Severina Mwijage ambaye ni Ndugu Alone Kaiza ni Mwenyekiti wa Vijana, Kata ya Kashai Bukoba Mjini, ahsante, karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa *Dr*. Luka Siyame ambao ni timu ya wanamichezo 27 wanawake na wanaume kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, wanashiriki michezo ya SHIMISEMITA wanaongozwa na Bwana Hemed Mwanda, hao wenyewe wako wapi? Karibuni sana.

Kwa hiyo, na pia ninayo heshima ya kuwatangaza wageni wa Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Benito Malangalila ambao ni timu ya wanamichezo 44 wanaotoka Mufindi walioshiriki mashindano ya SHIMISEMITA ambao wameshika nafasi ya kwanza kiujumla. Wanaongozwa na Bwana Juma Fulge, naomba wasimame, naona na makombe mnayo, nyie majirani zangu nawapa pongezi sana. Kwa hiyo kazi mliyofanya sasa kumbe na hao wote mmetoka mchezo huo huo, basi ninawapongeza walioshinda na walioshiriki pia ninawapongeza, ahsante. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi za Kamati. Kwanza kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 29 mwezi Oktoba, kutakuwa na kikao cha Kamati saa tano asubuhi katika chumba namba 231.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala Bora ndugu George Malima Lubeleje anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa saba mchana, katika ukumbi namba 219 katika jengo la utawala. Pia Mwenyekiti wa Tawi la *CPA Branch* Tanzania Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania kuwa leo hii saa tano kutakuwa na mkutano katika chumba namba 227.

Naomba kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Mheshimiwa Grace Kiwelu. Wageni kutoka Kanisa la

Mtakatifu Augustino, Kanisa Katoliki Basutu, Wilaya ya Hanang kama ifuatavyo, Padri Marco Diami na Sister Vicky, karibuni sana. (*Makofi*)

Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa Wabunge nilitumia kifungu 47 (3) cha Kanuni zetu za Bunge kwamba swali Namba 20 lijibiwe tena na bahati nzuri Waziri akauliza hajui cha kujibu. Sasa napenda kusema kwamba ile Kanuni inahusu swali la msingi au la nyongeza. Maneno aliyosema Mheshimiwa Lekule Laizer ndani ya Bunge alikuwa *serious*. Alisema walikula huko, walilala huko, walisafirishwa, walizungushwa na yeye alikuwa *serious*. Ili tuweze kuwapa upeo watu kuelewa ukweli wa yaliyosemwa yalikuwa kweli basi wachunguzi wafanye wajibu wao tena, ndiyo maana yake. Kwa hiyo ni *serious*, *I mean* vitu kama *allegation serious*, mkajibishane nyie tu na sisi tuliosikia tusemeje?

Ndio maana nikaomba jibu. Lakini Waziri anasema anaweza kujibu Bunge hili, kama una muda wa kujibu Bunge hili tutakupa nafasi kama itakuwepo. Kwa hiyo, ndio sababu ya kufanya vile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge la pili, kama mnaniandikia barua ninawaombeni msaini kwa kweli. Msiposaini mimi pia ninaita ni majungu na kama ni *allegation* ninaziweka kwenye debe. Kuna debe hapa. Heshima ya mtu ukimwandia barua msaini kama ni uwazi, asaini halafu itakuwa inajulikana nani kaandika. Kama hamsaini mimi nitakuwa naweka katika *dust bin* kwa sababu nitakuwa mimi sijui ni nani anasema. Kwa hiyo, ninadhani tunaelewana. Tuendelee na hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kushauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka Bunge lililopita lilikuwa Bunge la Bajeti, wakati Waziri wa Nishati na Madini anatoa hotuba yake ya Bajeti waliweka mezani Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Sasa iliwekwa mezani na ilikuwa ni wakati wa Hotuba ya Waziri, asingeweza kuijadili au kuizungumza hotuba ile pale, ingawa kuna Wabunge waliotoa hoja kwamba wangeomba hii taarifa ijadiliwa ilikuwa Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa waliomba hivyo, tukasema kwamba hiyo taarifa Serikali ime-*lay on the table* lakini ni vizuri wananchi nao wakajua, tuliopata nakala ya ile taarifa ni sisi Wabunge waligawa humu ndani, lakini wananchi pia wangependa kusikia kwa sababu Rais aliitangaza bayana.

Kwa hiyo utaratibu ni kwamba Waziri atatoa *summary* ya kila kitabu ambacho ni hiki halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Madini atatoa pia maana yake wao tuliwapa nafasi ya kwenda kukisoma hiki kitabu kwa uzuri zaidi Morogoro, naye atatoa *summary* yake. Kwa hiyo baada ya hapo ni mchango, kumbukeni Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi Sekta ya Madini, Rais aliunda Kamati kumshauri yeye kwa

hiyo hapa siyo Kamati ya uchunguzi, ya utafiti, ya nini, hapa ni kumshauri na nyie mtakachokuwa mnafanya mnaongezea ushauri ndani ya hii ripoti.

Kwa hiyo, hatuna upande wa Upinzani au upande wa nini, ni upande wa ushauri tu kwa Rais. Kwa hiyo Mwenyekiti wa Kamati atatoa maoni ya ile Kamati halafu mtaendelea kujadiliana, halafu tuta-*conclude* maana yake Serikali bado ina nafasi yake ya kupokea maoni yenu pamoja na yaliyoko humu ndani na kuleta hatua nyingine zinazofaa, baada ya kusema hivyo ninamwita Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini atoe *briefing*. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kwa dhati kabisa nikushukuru kwa kunipa muda nami nichangie hoja iliyo mbele yetu ambayo kwa kweli ni kujadili Mapendekezo ya Kamati ya Rais Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ninajua kabisa wamesoma Taarifa ya Kamati ya Rais na tunatarajia watatoa ushauri utakaotusaidia kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tunayoijadili leo ni matokeo ya juhudi za Serikali ya Awamu ya nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana pia na Bunge lako Tukufu. Kama tunavyokumbuka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alionyesha dhamira ya Serikali yake kuiboresha Sekta ya Madini kuanzia tarehe 30 Desemba, 2005 alipolihutubia Bunge lako Tukufu hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Sekta ya Madini kuchangia katika Pato la Taifa inaanzia miaka ya kabla ya Uhuru wa Tanzania, Sekta ya Madini kabla na baada ya Uhuru hadi mwishoni mwa miaka ya 1960 ilikuwa ikichangia katika Pato la Taifa kwa kiasi cha kuridhisha, hata hivyo mchango huo ulianza kupungua hadi kufikia chini ya asilimia moja ya Pato la Taifa hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Ili kuibua Sekta ya Uchumi katika kuchangia ukuaji wa uchumi mwaka 1979 Bunge lilipitisha Sheria ya Madini ya 1979, Sheria hiyo iliruhusu wawekezaji binafsi wa ndani na kutoka nje ya nchi kushirikiana na Serikali kwa ubia wa asilimia 49 kwa 51 sawia. Pamoja na juhudi hizo mazingira yaliyokuwepo hayakuvutia sana wawekezaji wakubwa na hasa wa kutoka nje ya nchi, katika kipindi hicho hatukuwa na sera ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipofika katikati ya miaka ya 1980 Serikali ilifanya marekebisho ya kisera na kimuundo kwa lengo la kuinua na kuhamasisha ukuaji wa uchumi wa Taifa, kufuatia marekebisho hayo Serikali ilitambua uwezo wa Sekta ya Madini kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo nchini, hivyo Serikali ikabuni Sera ya Madini ya mwaka 1997 iongoze na kuelekeza Maendeleo na uchumbaji wa madini nchini. Sera hii ilisisitiza juhudi za Sekta Binafsi kwa maana ya washiriki wa ndani na nje

ya nchi na umuhimu wa kuvutia teknolojia ya kisasa na mitaji inayohitajika katika uwekezaji kwenye uchimbaji mkubwa wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji na Mafanikio ya Sera ya Madini ya mwaka 1997, mwaka 1997 Bunge lako Tukufu lilipitisha marekebisho ya sheria mbalimbali za fedha yaani *the Financial Laws Miscellaneous Amendment* ya mwaka huo 1999 kwa lengo la kuweka vivutio vya uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, mwaka 1998 Bunge hili Tukufu lilipitisha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ili kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Madini. Mafanikio makubwa yaliyopatikana kati ya mwaka 1997 hadi mwaka 2007 na kwa ujumla mpaka sasa ni pamoja na yafuatayo.

Kwanza, kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 1.4 mwaka 1996 hadi asilimia zaidi ya 3.5 kwa mwaka 2007.

Pili, kukua kwa Sekta ya Madini kutoka asilimia 9.7 mwaka 1996 hadi asilimia 15.6 hadi kufikia mwaka 2006.

Tatu, kuongezeka kwa mapato ya Serikali yatokanayo na uchimbaji mkubwa wa madini kutoka jumla ya Dola za Marekani chini ya milioni mbili kwa mwaka 1996 kufikia Dola za Marekani milioni 85.7 hadi kufikia mwaka 2007.

Nne, kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu kutoka tani moja kwa mwaka 1996 hadi takriban tani 50 za dhahabu katika mwaka 2006.

Tano, kuongezeka kwa ajira katika Sekta ya Madini kutoka takriban wafanyakazi 1,700 kwa mwaka 1996 hadi zaidi ya wafanyakazi wapatao 13,000 kufikia mwaka 2006 walioajiriwa kwenye migodi mikubwa.

Sita, kuongezeka kwa idadi ya wachimbaji wadogo kutoka takriban wachimbaji 500,000 waliokuwepo kwa mwaka 1996 hadi kufikia wachimbaji wapatao 1,000,000 kwa mwaka 2006, hivyo kuwa tegemeo la maisha kwa watu waishio maeneo ya machimbo.

Saba, kutenga maeneo maalum kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto Katika Utekelezaji wa Sera ya Madini, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Sekta ya Madini imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali na hususan zifuatazo.

Moja, mchango mdogo wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa Sekta yenyewe.

Mbili, uwezo mdogo wa Serikali kusimamia shughuli za madini hususan kubaini gharama halisi za uwekezaji, utafutaji, uzalishaji na biashara ya madini, utunzaji wa mazingira na usala migodini.

Tatu, madini mengi kuendelea kuuzwa nje ya nchi yakiwa ghafi.

Nne, kasi ndogo ya kurekebisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

Tano, kiwango kidogo cha kushirikisha na kuwianisha Sekta ya Madini na shughuli nyingine za uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Kukabiliana na Changamoto Zilizopo, kwa nyakati mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa hapo juu, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha Sekta ya Madini, miongini mwa hatua hizo ni kuunda Kamati mbalimbali ili kuishauri Serikali namna ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hizo ni pamoja na zifuatazo, kwanza, kulikuwa na Kamati ya kuchunguza chanzo cha migogoro baina ya Kampuni iliyokuwa ya *AFGERM* kwa sasa hivi ni *Tanzanite One* na wachimbaji wadogo wa Merelani iliyoundwa mwaka 2002 na hii Kamati ni maarufu kwa jina la Kamati ya Mboma. Kamati hii ilitoa maoni na mapendekezo kuhusu uhusiano kati ya wachimbaji wadogo wa *Tanzanite* na Kampuni iliyokuwa inaitwa *AFGERM* sasa hivi ni *Tanzanite One*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, iliishauri Serikali isisitishe utoaji wa leseni za uchimbaji mkubwa wa *Tanzanite* kwa wawekezaji wa nje na badala yake eneo lililobaki limilikishwe kwa wachimbaji wadogo, kufuatia pendekezo hilo sehemu ya eneo la Merelani ilitengwa kuwa eneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo pekee.

Pili, Kamati ya Kuruhusu Sera ya Madini ya mwaka 1997 ambayo inajulikana zaidi kama Kamati ya Kipokola ambayo iliyoundwa mwaka 2004. Kamati hii ilitoka maonai na mapendekezo kuhusu uboreshaji wa Sera ya Madini na mfumo wa usimamizi wa Sekta ya Madini, baadhi ya mapendekezo ni pamoja na ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi kupitia mashirika yake ya *STAMICO* na *National Development Corporation* yaani *NDC*, Shirika la Maendeleo la Taifa, pia kulikuwa na ushauri wa Tanzania kuwezeshwa kushiriki katika uchimbaji mkubwa wa madini na kupitia upya mfumo wa kodi katika Sekta ya Madini hususan kuondoa misamaha ya kodi isiyokuwa ya lazima, utekelezaji wake utazingatiwa katika Marekebisho ya Sera ya Madini ambayo rasimu yake imeanza kuandaliwa.

Tatu, kulikuwa na Kamati ya Kupitia Mikataba na Mfumo wa Kodi katika Sekta ya Madini ya mwaka 2006 maarufu kama Kamati ya Masha. Kamati hii ilipitia mikataba na kutoa maoni na mapendekezo kuhusu mikataba ya madini na mfumo wa kodi na kufanya tathmin ya utendaji wa taasisi zenye majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini.

Aidha, Kamati ilipendekeza kuanzisha majadiliano kati ya Serikali na Kampuni zenye midogo hususan kwenye vipengele vya mikataba vinavyohusu mifumo ya kodi katika Sekta ya Madini, utekelezaji wake ulishaanza na baadhi ya mambo yanazingatiwa

katika marekebisho ya Sera na Sheria ya Madini yanayoendelea kufanyiwa kazi kwa sasa.

Nne, kulikuwa na Kamati ya Majadiliano ya Mikataba baina ya Serikali na Kampuni za Madini maarufu kama Kamati ya Bukuku. Kamati hii iliundwa kutekeleza mapendezo ya Kamati ya Masha, matokeo ya majadiliano haya hadi sasa ni pamoja na baadhi ya kampuni kukubali kuondoa unafuu wa ziada wa asilimia 15 ya gharama ambazo hazijakombolewa yaani *additional capital allowance on undimmed qualifying capital expenditure* katika mikataba yao na kampuni kuanza kulipa tozo ya Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri zinazozunguka midogi hiyo.

Tano, Kamati ya Mheshimiwa Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini ya mwaka 2008 Kamati ambayo iliundwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2007mwezi Novemba na hii ni maarufu kama Kamati Mheshimiwa Jaji Mark Bomani na ndio hii ambayo imepelekea leo tunajadili suala hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ilichambua mapendekezo ya Kamati zilizotangulia na kutoa mapendekezo juu ya usimamizi wa Sekta ya Madini kwa ujumla, miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kwanza, kufanya marekebisho ya Sera na Sheria ya Madini, kufanya Marekebisho ya Mfumo wa Kodi katika Sekta ya Madini, Ushiriki wa Serikali hususan katika Madini Mkakati, kuimarisha usimamizi wa Sekta ili iweze kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi. Ninayotaja haya ni baadhi tu mambo ambayo yamependekezwa lakini ninaamini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu walipata taarifa hizi na vitabu husika naamini kwamba watakuwa wameyapitia na kuona yale ambayo yamependekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ni pamoja na kwanza, mwaka 2003 Serikali iliajiri mkaguzi aliyekuwa anaitwa *Alex Stewart, Asias Government Business Corporation* kwa ajili ya kuhakiki uzalishaji na usafirishaji wa dhahabu na gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa ya dhahabu nchini, ukaguzi huo uliendelea hadi mwezi Agosti mwaka 2007 ambapo jukumu hilo lilirejeshwa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mwaka 2004 Serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambapo viwango vya mrahaba katika madini ya vito vilirekebishwa kutoka asilimia tatu hadi asilimia sifuri kwa madini ya vito yaliyosanifiwa na kutoka asilimia tatu hadi asilimia tano kwa madini ya vito yasiyosanifiwa.

Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali iliongozwa na Mheshimiwa Bomani kuhusu usimamizi wa sekta ya madini kama nilivyoeleza iliteuliwa mwezi Novemba mwaka 2007 na kukamilisha jukumu lake mwezi Aprili mwaka huu 2008. Kamati ilifanya kazi nzuri ambayo tunatarajia itatusaidia katika usimamizi wa Sekta ya Madini, Serikali imeanza kuyafanyia kazi mapendekezo ya Kamati hii Kikosikazi kimeundwa kutoa ushauri na namna ya kutekeleza mapendekezo hayo. Mapendekezo ya Kikosikazi yatazingatiwa katika marekebisho ya Sera ya Madini ya Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali Sekta ya Madini imeendelea kukua lakini bado inazo changamoto nyingi hasa kubwa zaidi ni namna ya sisi kama Taifa tunavyoweza kufaidika zaidi na sekta hii kuliko ilivyo sasa. Hata hivyo kitakwimu uwekezaji uliopo sasa hauwezi kuleta matokeo na uweze kuonekana haraka kwa mfano, thamani ya madini yaliyouzwa nje kwa mwaka 2007 kwa Dola za Kimarekani ni Dola milioni 857,309,000 ikilinganishwa na Pato la Taifa ambalo lilikuwa ni shilingi milioni 20,948,403 kwa bei ya 2007. Takwimu hivi zinabainisha kuwa thamani ya madini inayouzwa nje ya nchi ikilinganishwa na Pato la Taifa ni takriban asilimia 4.5 tu, ni wazi si rahisi mchango wa sekta ya madini kuonekana moja kwa moja na matokeo yake kama ambavyo tungetarajia. Kwa kuzingatia hizo takwimu mchango wa Sekta ya Madini katika uchumi wa Taifa utaonekana endapo uwekezaji na uzalishaji wa madini utaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua ambazo tumefikia kama Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais bado tuko wazi kupokea ushauri wenu kuhusu namna bora ya kusimamia Sekta ya Madini kama ambavyo mmekuwa mkichangia katika mjadala wetu unaohusu sekta hii humu Bungeni na wakati mwingine nje ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoona wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara yetu mwezi Julai mwaka huu 2008, ratiba ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Rais iliyoongozwa na Mheshimiwa Bomani ni kwamba marekebisho ya Sera na Sheria ya Madini yatakamilika ifikapo mwezi Aprili mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa mara nyingine kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika, kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, niishukuru sana Kamati ya Nishati ya Madini chini ya Uongozi wa Mheshimiwa William Shellukindo pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa *Dr*. Harrison Mwakyembe. Lakini pia tunatambua ushiriki wa Taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizokuwa za Kiserikali, vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla kwa jinsi ambavyo kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakishiriki na wameendelea kushiriki kutoa maoni yao ambayo tunaamini kwamba kwa pamoja tukiyazingatia yatatusaidia sana kuimarisha Sekta ya Madini ambayo hatimaye mchango wake katika Pato la Taifa utaongezeka.

Baada ya kusema hayo kama ulivyosema na kama ulivyofafanua wakati unanielekeza nije nitoe hotuba ya maneno ya utangulizi katika uchangiaji wa mjadala huu tunategemea michango mizuri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha taarifa, naomba kwa kutumia Kanuni ya 150 ya Kanuni za Bunge za Kudumu, kutengua Kanuni ya 62 (h) ili niwezeshe kuweza kusoma taarifa na kuimaliza. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa hapo juu)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu yaliyomo katika Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) Toleo la 2007 napenda kukushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ili kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini niwasilishe taarifa hii ambayo ni ya uchambuzi wa Taarifa ya Kamati ya Rais iliyoundwa kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini. Kwa niaba ya Wajumbe wenzangu napenda nikushukuru kwa kuipa Kamati jukumu la kuipitia na kuichambua taarifa hiyo. Napenda kukuhakikishia kuwa Kamati yangu ilifanya kazi kwa umakini na uadilifu mkubwa bila kuathiri yaliyomo katika Taarifa hiyo.Aidha, Kamati ya Nishati na Madini inapenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa busara wa kuunda Kamati hiyo maalum kwa lengo la kuboresha Sekta ya Madini hapa nchini. Vilevile, tunamshukuru Rais kwa kulihusisha Bunge lako Tukufu katika hatua za mwanzoni kabisa za kuichambua taarifa hii. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa mapendekezo yote ya Kamati ya Rais yatatekelezwa na Serikali kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo yote yaliyotolewa kwenye Taarifa ya Kamati ya Rais. Hata hivyo yapo mapendekezo ambayo Kamati inaona yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi. Hii ni kutokana na unyeti wa mapendekezo hayo ikilinganishwa na hali halisi ya Sekta ya Madini na hali ya uchumi wa nchi kwa wakati huu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeichambua Taarifa ya Kamati ya Rais ukurasa kwa ukurasa hatimaye kuchagua baadhi ya maeneo ambayo Kamati ya Rais iliyapa uzito. Kamati yangu imeridhika kuwa maeneo hayo ni ya msingi na yanatakiwa kujadiliwa kwa kina ili kuyapatia ufumbuzi wa haraka. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Sera ya Madini;
(ii) Sheria ya Madini;

(iii) Mikataba ya Madini;
(iv) Umiliki wa Migodi;
(v) Uharibifu wa Mazingira na Uhuishaji wake;
(vi) Vivutio kwa Wawekezaji;
(vii) Ulipaji wa fidia kwa Wananchi wanaopisha shughuli za uchimbaji;
(viii) Wachimbaji Wadogo;
(ix) Madini ya Vito; na
(x) Ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini. Sera ya Madini ya Mwaka 1997 inatamka bayana kwamba, Serikali katika kuendeleza Sekta ya Madini italenga kuvutia na kuiwezesha sekta binafsi kushika hatamu katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Aidha, dhima ya sekta ya umma itakuwa ni kuchochea na kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi katika madini kwa kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa sera uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, Sera hii inaeleza juu ya mikakati ambayo imeandaliwa na Serikali kwa lengo la kutimiza malengo yake kama ifuatavyo:-

-Kujenga mazingira bora na imara ya kiuchumi;
-Kubuni na kutekeleza mfumo wa kodi ambao unafaa kwa Wawekezaji;
-Kuwa na mfumo wa sheria na udhibiti unaokubalika Kimataifa;
-Kuboreshwa kwa huduma za kifedha zitakazotolewa kwa Sekta ya Madini;
-Kuweka utaratibu bora wa Uchimbaji Mdogo wa Madini;
-Uanzishaji wa Mifumo Rasmi ya Masoko;
-Kushirikisha Uchimbaji Madini katika Uchumi wa Taifa;
-Kuhamasisha maendeleo ya Watumishi katika Sekta ya Madini;
-Kuunganisha mambo muhimu yanayohusu hifadhi ya mazingira na jamii; na
-katika mipango endelevu ya maendeleo ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na misingi na mikakati muhimu ya Sera ya Madini kuanishwa, Kamati imebaini upungufu ambao unapaswa kuangaliwa upya kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Madini ili iweze kuleta manufaa zaidi kwa Taifa. Upungufu uliobainishwa ni kama ufuatavyo:-

Sera kutoeleza bayana ushiriki wa Serikali katika uwekezaji na badala Serikali kujiwekea jukumu la kuwa mhamasishaji tu wa sekta binafsi. Kamati inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza kuwa Sera ianishe bayana nafasi ya Serikali kushiriki katika uwekezaji kwenye Sekta ya Madini kwa kuweka msisitizo kwenye madini yenye umuhimu kimkakati *(strategic minerals)* kama vile chuma, nikeli, uraniamu na makaa ya mawe ambayo yanatoa fursa ya ujenzi wa viwanda vya msingi. (*Makofi*)

Sera kutoeleza bayana dhana ya uchimbaji au uvunaji endelevu, hasa ikizingatiwa kuwa madini ni rasilimali inayokwisha, hivyo italeta madhara kwa Taifa kutokana na rasilimali hii kumalizika haraka. Kamati yangu inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza juu ya sera kutambua umuhimu wa kuweka mkakati wa uchimbaji endelevu wa madini yaliyopo na mapato yatokanayo na madini kutumika kwa shughuli za maendeleo ya Taifa letu.

Sera kusisitiza zaidi mfumo wa kodi kama njia pekee ya kuvutia Wawekezaji hali ambayo imesababisha Serikali kukosa mapato stahili na hivyo kuzua malalamiko mengi kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo, Kamati yangu inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza kuwa sera ielekeze kuwa vivutio vingi vitolewe kwa utafutaji wa madini na siyo kwa uchimbaji au wachimbaji wa madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini. Jambo lingine lililobainishwa katika Taarifa ya Kamati ya Rais ni suala la Mikataba ya Madini (*Mineral Development Agreements- MDA*s) ambayo baadhi ya masharti yake yanakiuka Sheria za Nchi. Kwa mfano, kifungu cha 83 (1) (a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinataka malipo yote yanayofanywa na Kampuni za Madini kwa Kampuni za ndani na za kigeni zinazotoa huduma za menejimenti na utaalamu *(Management and Technical Services)* kwa Kampuni hizo za madini, zikatwe kodi iitwayo Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwango vya Kodi ya Zuio vimeelezwa kwenye Jedwali Na. 1 la Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004 kuwa asilimia tano (5%) kwa Kampuni za ndani na asilimia kumi na tano (15%) kwa Kampuni za kigeni. Lakini baadhi ya Kampuni zenye Mikataba ya Madini (*MDAs)* zinakata Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia (3%) tu kwa Kampuni zote, kiwango ambacho kimeainishwa kwenye Mikataba yao.

Vilevile, zipo Kampuni zenye Mikataba zisizokata kodi hiyo kabisa. Mfano ni kodi kwenye riba itokanayo na mikopo kutoka kwenye Kampuni zenye uhusiano *(related or affiliated companies)* ambapo baadhi ya Mikataba ina kipengele kinachozuia kodi hiyo kukatwa.

Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na Kamati ya Rais kuwa huu ni ukiukwaji wa Utawala wa Sheria ambapo Mikataba ya kibiashara inajidhihirisha kuwa na nguvu zaidi ya sheria ya nchi! Hali hii haikubaliki kabisa.

Hivyo basi, Serikali ihakikishe kuwa viwango mahsusi vya Kodi ya Zuio vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 vinatumika mara moja na kuhakikisha uvunjifu wa sheria za nchi hauendelei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Kamati ya Rais inataka Serikali ijadiliane na baadhi ya Kampuni za madini zenye Mikataba kwa lengo la kukiondoa kipengele kinachokataza ukataji wa Kodi ya Zuio kwenye malipo ya riba inayolipwa kwa Kampuni zenye uhusiano *(related or affiliated companies),* Kamati ya Nishati na Madini haioni sababu za mjadala kwenye suala lililo wazi na la kisheria na kusisitiza kuwa kipengele hicho batili kimejifuta chenyewe. Mjadala wa aina hiyo hautakuwa na tija yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la Mikataba limeonekana kugubikwa na matatizo makubwa ya usiri, utata na ina vipengele vinavyokiuka taratibu na Sheria za Nchi, Kamati ya Nishati na Madini inaona kuwa kuna haja sasa ya kuondokana kabisa na Mikataba ya aina hiyo na kuiandika upya Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ili ijumuishe mambo yote ambayo yangeingia kwenye Mikataba. Sheria hiyo ifuatwe na mchimbaji yeyote atakayeonesha nia ya kuchimba madini hapa nchini. Kuwepo kwa sheria hii kutaondoa kwa kiasi kikubwa matatizo ambayo Serikali inayapata sasa kuhusiana na Mikataba iliyopo sasa.

Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na Kamati ya Rais kuwa ili Kampuni iweze kuwa na Mkataba *(MDAs)* binafsi na Serikali, uwekezaji wake lazima uwe mkubwa. Kamati ya Rais imependekeza kuanzia dola za Marekani milioni 200. Kwa upande wake Kamati ya Nishati na Madini inaona haja ya kukiongeza kiwango hicho kuwa dola za Marekani milioni 600 na zaidi.

Taarifa ya Kamati ya Rais pia imetamka kuwa kiwango cha uchakavu *(depreciation rate)*, kwa ajili ya vifaa vinavyotumika katika utafutaji na uchimbaji wa madini ni asilimia 20 kwa mujibu wa Daraja la Nne la Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na Kamati ya Rais kuwa nafuu ya uchakavu wa mitambo (*depreciation allowance*) kwa kawaida hutolewa kwa kiasi kinacholingana na matumizi ya mitambo kwa mwaka husika wa mapato na hivyo gharama yote kukombolewa kwa miaka kadhaa na siyo mara moja kama inavyofanyika kwenye Sekta ya Madini. Kwa kutumia nafasi hii, Kampuni za madini huweza kukomboa gharama ambazo hazina uhusiano na mapato ya mwaka wa kodi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano wa udanganyifu katika uingizaji wa mitambo ya madini ni mkubwa. Upo uwezekano wa mitambo hii kupitishwa pamoja na vitu visivyohusiana na uchimbaji na uwezekano wa kuingizwa mitambo chakavu. Kamati ya Nishati na Madini inaona ulazima kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kukagua vifaa au mitambo yote inayoingizwa nchini kwa utafutaji na uchimbaji wa madini ili kuzuia udanganyifu kwa vifaa vinavyoingizwa na katika kukokotoa kwa usahihi viwango vya uchakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Rais katika Taarifa yake imeeleza kuwa Kifungu cha 145 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kinaruhusu kutumika kwa Sehemu ya Tatu ya Jedwali la Pili la Sheria ya Mapato iliyofutwa ya mwaka 1973. Jedwali hilo linatoa fursa kwa Kampuni za Madini kukomboa gharama zinazohusiana na shughuli za madini. Kwa maneno mengine, Wawekezaji wanapewa unafuu wa asilimia 100 wa gharama za uwekezaji katika kukokotoa mapato yanayotozwa kodi kwa mwaka wa uwekezaji *(100% capital allowance in the year of expenditure).* Aidha, Wawekezaji wanapewa unafuu wa ziada wa asilimia kumi na tano (15%) kwenye gharama za uendelezaji wa migodi ambazo hazijakombolewa *(additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure).*

Mheshimiwa Naibu Spika, unafuu huu kwa njia ya kodi ni mbaya na unasababisha upungufu mkubwa kwenye mapato ya nchi yatokanayo na kodi ya mapato. Mwaka 2001, Kifungu hicho kinachotoa unafuu huo wa kuikamua nchi, kilifutwa kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2001.

Lakini mwaka uliofuatia wa 2002 kipengele hicho hicho kikarejeshwa na Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2002. Mwaka 2004 Bunge lilipotunga Sheria mpya ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 ilifutwa.

Lakini kwa taarifa ambazo Kamati ya Rais ilizipata, Kifungu maalum (Kifungu cha 145) kikawekwa kwenye Sheria mpya ya Kodi ya mapato ili kuruhusu sehemu ya Tatu ya Jedwali la Pili la Sheria iliyofutwa kutumika kwa lengo la kuendeleza unafuu huo mkubwa kwa Wawekezaji na kuathiri maslahi ya Taifa. (Tafadhali soma Kifungu cha 145 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ambayo Kamati ya Rais iliyapata, kwamba Serikali ilishinikizwa kukirejesha tena Kifungu hicho cha Sheria ya mwaka 1973, hayafurahishi kusikia, hivyo Kamati ya Nishati na Madini inaungana na Kamati ya Rais kutaka Kifungu hicho cha 145 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kifutwe mara moja ili kuondoa unafuu huo wa kutisha na wa aibu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya Madini. Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo mengine yote kuhusu Mikataba ambayo Kamati ya Rais imeyatoa. Mapendekezo hayo ni pamoja na:-

Mikataba (*MDAs*) itakayoingiwa kwa miradi ya dola milioni 600 na zaidi ni lazima iwasilishwe Bungeni kwa Taarifa (kama Hati za Kuwasilisha Mezani).

Mikataba yote itakayoingiwa iwe wazi kwa wananchi na ipatikane katika Ofisi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri ambako migodi ipo. (*Makofi*)

Uhai wa Mikataba upunguzwe toka miaka 25 ya sasa ili itoe fursa ya kupitiwa *(reviewed)* kila baada ya kipindi cha miaka 10. Hata hivyo, Kamati ya Nishati na Madini imeona kwamba kuna haja ya kuipitia Mikataba hiyo katika kipindi cha miaka mitano - mitano baada ya miaka 10 ya kwanza ili kuleta ufanisi kulingana na mabadiliko yatakayojitokeza katika uchumi wa nchi na Dunia kwa ujumla. (*Makofi*)

Tozo za Halmashauri (Serikali za Mitaa) zifanane na Tozo zilizopo katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 ambayo inataka Kampuni za madini kulipa kwenye Halmashauri husika kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo yote. Hii ni kinyume na Sheria ya Serikali za Mitaa tunayotaja katika Kifungu hiki.

Kwa kuwa Mwekezaji kupitia Mikataba ya Madini (MDAs) anaruhusiwa kuweka fedha zake nje ya nchi kwa kibali cha Gavana wa Benki Kuu *(BOT)* ambaye hana budi kukitoa kibali hicho mara anapoombwa. Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na pendekezo la Kamati ya Rais kuwa Gavana aachiwe nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, bila mashinikizo nje ya Sheria.

Kuhusu utaratibu wa kumruhusu Mwekezaji kuweka fedha zake za mtaji na zile zinazopatikana kutokana na mauzo ya madini, katika benki za kigeni na kuzitumia atakavyo, ilimradi aweze kutimiza wajibu wake kwa kulipia gharama zake hapa Tanzania; imebainika kuwa utaratibu huu kwa sasa unawawezesha Wawekezaji kutumia takribani asilimia sitini (60%) katika matumizi hayo.

Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na Kamati ya Rais na kupendekeza kuwa angalau asilimia sabini (70%) ya fedha zinazotokana na mauzo ya madini zirejeshwe Nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani. Serikali iweke mkakati bayana wa kuwezesha Kampuni za Kitanzania kutumia fursa za kibiashara zinazotokana na kuwepo kwa migodi mikubwa Nchini; kwa mfano Kampuni za kutoa huduma ya chakula *(catering),* huduma za vifaa kama vile ulinzi, sare za wafanyakazi na kadhalika.

Katika kukokotoa mapato ya Kampuni za Madini kwa madhumuni ya kulipa kodi, Kampuni hizo zinaruhusiwa kuingiza kwenye mahesabu yao gharama za miradi yote inayoendesha sambamba na uchimbaji wa madini Nchini.

Kwa maneno mengine, hakuna *ring fencing* kwa msingi wa mgodi mmoja utozwe tofauti na mwingine wa Kampuni hiyo hiyo. Kukosekana kwa *ring fencing* ni moja ya sababu kubwa ya Kampuni za madini kuendelea kutangaza kupata hasara za kodi *(tax losses)* kwa kuwa zinaruhusiwa kuchanganya hesabu za miradi yao mbalimbali kwenye mapato ya kodi ya mwaka husika. Hii inatokea huku bei ya madini (hususan dhahabu) ikiendelea kupanda katika soko la dunia. Kwa mfano, mwaka 2006 mgodi wa Tulawaka ulipata faida ya dola za Kimarekani milioni 28.2.

Lakini mgodi huo haukulipa kodi ya mapato kutokana na mchezo wa kuchanganya gharama za miradi mbalimbali inayoendeshwa na Kampuni inayomiliki mgodi huo, ambayo imepata hasara. Kamati yangu inakubaliana na Kamati ya Rais na kuzidi kusisitiza umuhimu wa kuwa na *ring fencing* katika kukokotoa mapato ya kila mradi kwa madhumuni ya kodi inayostahili kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ya Madini ina upungufu mkubwa na imepitwa na wakati hapana budi irekebishwe haraka. Kwa hiyo, Kamati yangu inashauri kwamba Mikataba mipya isisainiwe mpaka hapo Sheria mpya ya Madini itakapopitishwa na Bunge. Hili likifanyika litasaidia kuondokana na matatizo ambayo tunayapata katika Mikataba iliyopo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Umiliki Wa Migodi. Taarifa ya Kamati ya Rais imeeleza kwa ufasaha jinsi umiliki wa migodi ulivyokuwa hapo awali na hali ilivyo sasa. Ni dhahiri kuwa Serikali imekuwa ikijitoa katika umiliki wa Kampuni za uchimbaji kwa kuuza hisa zake zote ama kwa Kampuni iliyoingia nayo ubia ama Kampuni nyingine mpya.

Kwa mfano, Kamati imebaini kuwa mwaka 1994, Serikali ilikuwa na hisa asilimia kumi na tano (15%) kwa ubia na Kampuni ya *Sutton Resources ya Canada* katika mgodi wa Bulyanhulu. Hata hivyo, mwaka 1999, Serikali iliachia asilimia kumi (10%) ya hisa zake baada ya kuanzishwa kwa kodi ya zuio. Pamoja na hili mwenendo wa uuzaji wa hisa hizi unatia mashaka na kudhoofisha nia hasa ya uuzwaji wa Hisa zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na matatizo na malalamiko mengi katika umiliki wa hisa katika migodi na jinsi hisa hizo zinavyouzwa, Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge lako Tukufu inapendekeza kufanyike uchunguzi maalum juu ya jinsi Serikali ilivyouza hisa zake na mahali fedha hizi zilipokwenda na kutumika katika Migodi ya Kiwira, Bulyanhulu na Mwadui na Taarifa itolewe mbele ya Bunge lako Tukufu.

Vilevile, Kamati ya Nishati na Maini inapendekeza usitishwaji wa Serikali kumiliki hisa katika migodi na badala yake shughuli hiyo zihamishiwe kwenye Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* na kutekeleza jukumu hilo kitaalamu kwa niaba ya Serikali. Pia, Serikali isitishe mipango yake ya kuendelea kuuza hisa zake katika ya Migodi ya *Buckreef Gold Mine (Geita), Kiwira Coal Mines Ltd, Williamson Diamonds Ltd* n.k mpaka hapo Serikali itakapojipanga vizuri zaidi kwa njia ya kuiwezesha *STAMICO* kusimamia hisa na kuiwezesha kushiriki katika kutoa maamuzi endelevu ya migodi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imeona umuhimu wa kuangalia kwa makini uwakilishi wake katika Bodi za Wakurugenzi wa Kampuni za Madini ambapo Serikali inahisa. Wawakilishi hawa ndio wanaotakiwa kutetea maslahi ya Serikali katika Migodi husika. Vigezo kama weledi *(professionalism)*, uadilifu na uzoefu katika nyanja za uchumi, fedha, madini, sheria n.k ni muhimu kuzingatiwa katika uteuzi wa Wawakilishi hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uharibifu Wa Mazingira Na Uhuishaji Wake. Taarifa ya Kamati ya Rais imebainisha kuwa Kifungu cha 15 (3) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kinawaruhusu Wawekezaji katika Sekta ya Madini kufanya makadirio ya fedha wanazotenga kwa ajili ya kuhuisha mazingira baada ya shughuli za uchimbaji kuisha. Hata hivyo imebanika kuwa fedha hizo zinakadiriwa tu bila kutengwa kwenye akaunti na hupunguzwa kama gharama halisi za matumizi wakati wa kukokotoa mapato yanayostahili kutozwa kodi. Kamati yangu inakubaliana na Kamati ya Rais kuwa utaratibu huu unatoa mwanya kwa baadhi ya Wawekezaji wasio waadilifu kufanya makadirio makubwa kuliko gharama zenyewe kwa lengo tu la kupata unafuu mkubwa zaidi kwenye kodi, hivyo kuinyima Nchi mapato halali ya kodi. Aidha, kwa vile hayo ni makadirio tu, hakuna uhakika wa fedha hizo zinazokadiriwa na kupewa unafuu wa kodi kuwepo kwenye akaunti ya Mwekezaji wakati wa mgodi kufungwa.

Hivyo basi, Kamati ya Nishati na Madini inakubaliana na Kamati ya Rais kuwa Kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Kodi ya Mapato kirekebishwe mara moja ili gharama za

kuhuisha mazingira ziwe halisi na ziwekwe kwenye Akaunti Maalum au kwenye Mfuko Maalum wa Dhamana (*Trust*) na kuthibitishwa na Kamishna wa Kodi ya Mapato.

Aidha, Kamati yangu haioni sababu za kusubiri mpaka shughuli zote za mgodi kumalizika ndipo shughuli za kuhuisha mazingira (ardhi) zianze. Kamati inaliomba Bunge liiagize Serikali kuanza kuwabana wachimbaji kufukia mara moja mashimo ambayo hayatumiki tena pale ambapo wanaendelea na shughuli za uchimbaji sehemu nyingine.

Vilevile, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* lipewe jukumu kisheria la kukadiria na kuhakiki gharama za kuhuisha *(renew)* mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ilivyo sasa, Mamlaka zinazosimamia udhibiti wa makubaliano ya kutunza mazingira hazipo katika maeneo ya machimbo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka na makusudi kuziwezesha za Mamlaka husika kama vile *NEMC*, kudhibiti maeneo yote ya uchimbaji ili kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Nishati na Madini inasisitiza na kuishauri Serikali kusimamia kikamilifu matumizi ya kemikali katika migodi ili kuepusha athari za mazingira na afya za Wafanyakazi Migodini na Wananchi wanaoishi maeneo jirani na Migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vivutio Vya Ziada Kwa Wawekezaji. Ushuru wa mafuta. Katika Sura ya Pili ya Taarifa ya Kamati ya Rais imebaini kwamba Kampuni za madini zinazozalisha dhahabu na ambazo pia zina Mikataba *(MDAs)* zinatakiwa kulipa ushuru huu kwa kiasi kisichozidi dola za marekani 200,000 kwa mwaka bila kujali kiasi cha mafuta kilichotumika. Hii ni kutokana na Tangazo la Serikali Na. 99 la Tarehe 15 Oktoba 2005 ambalo linazifutia Kampuni hizo ushuru wote unaozidi dola za Marekani 200,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa hiyo ya Kamati ya Rais, Takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa Fedha 2006/2007 Serikali ilizifutia Kampuni kubwa tano zinazozalisha dhahabu ushuru wa jumla ya shilingi bilioni 11.56 na katika mwaka wa fedha 2007/2008 kiasi cha bilioni 32.7 kilitarajiwa kufutwa. Kiasi hicho cha fedha ni kwa Kampuni tano tu.

Mathalan, jumla ya msamaha wa kodi ya mafuta kwa mwaka 2006/2007 ni shilingi bilioni 51.4 na kwa mwaka huu wa fedha inategemewa kufikia shilingi bilioni 91.6. ni dhahiri kuwa kiasi hiki cha fedha ni kikubwa mno na si busara kuendelea kukipoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa ushuru wa mafuta ni chanzo muhimu cha mapato ya Serikali hususan kwa ajili ya kujenga na kukarabati barabara. Mafanikio ya sekta ya barabara yanayoonekana hivi sasa, yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushuru wa mafuta.

Kamati yangu inaungana na Kamati ya Rais kutoa maoni kuwa, kufutwa kwa ushuru wa mafuta unaotakiwa kulipwa na Kampuni za Madini kumedhoofisha uwezo wa Serikali kujenga miundombinu ya barabara kwa kiasi kikubwa hivyo kupoteza manufaa makubwa ambayo Serikali na Taifa ingepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba inaweka kiwango cha juu cha tozo ya ushuru wa barabara kuwa dola za Marekani 200,000 kwa mwaka bila kuzingatia matumizi halisi ya mafuta katika mgodi. Kamati inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza kuwa msamaha wa ushuru wa mafuta *(fuel levy)* uondolewe kwa Kampuni ambazo hazijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa na zinatumia mafuta katika kuzalisha umeme unaotumika kwenye migodi tu. Tunasema hivyo kwa sababu hizo zinaweza kuingia katika gharama za mgodi badala ya kutoa msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushuru wa Forodha *(Customs Duty).* Kamati imetathimini msamaha wa ushuru wa Forodha unaotolewa kwa Kampuni za Madini na Makandarasi wao na haioni kuwa ni lazima ushuru huo uondolewe hususan kwa Kampuni zenye migodi iliyoanza uzalishaji ambapo ushuru huo unaweza kuchukuliwa kuwa ni gharama za kawaida za uendeshaji kama ilivyo kwenye *fuel levy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza kuwa:-

- Kampuni zinazozalisha zisipewe msamaha wa Ushuru wa Forodha.

- Msamaha wa Ushuru wa Forodha uwe ni kwa vifaa vya ujenzi vinavyoingizwa na kutumika katika ujenzi wa migodi tu.

- Serikali itengeneze orodha ya vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya Sekta ya Madini na kuiwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa majadiliano/mashauriano kwa lengo la kuwa na orodha moja ya Jumuiya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushuru wa Bidhaa. Pamoja na kuwepo kwa kipengele kinachoruhusu Wafanyakazi wa Kigeni wanapoingiza vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi binafsi ikiwa ni pamoja na gari moja bila kulipa Ushuru wa Forodha na kodi nyingine.

Kipengele hicho kinapunguza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi za ushuru. Kamati inaungana na Kamati ya Rais kupendekeza kuwa mkataba uwatake wafanyakazi wa Kigeni wanapoingiza magari na vifaa vingine kulipa ushuru na kodi nyingine kwa mujibu wa sheria husika kama ilivyo kwa wafanyakazi wa sekta nyingine.

Aidha, ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ufutwe ili Kampuni hizo zilipe Ushuru huo kwa viwango vilivyoidhinishwa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni ya Madini yenye Mikataba *(MDAs),* hutumia viwango vya Ushuru wa Stempu vilivyotajwa kwenye Mikataba husika, ambavyo ni vidogo ukilinganisha na vile vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189, wakati Mikataba iliposainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Rais kwamba, Mikataba yote itakayoingiwa kuanzia sasa, izingatie Sheria husika za Kodi, kwa tarehe husika. Pia Mikataba yote yenye upungufu huu irekebishwe kwa kuzingatia viwango vya ushuru wa Stempu, ambavyo vilikuwa kwenye Sheria husika tarehe ya kuanza kutumika kwa Mikataba hiyo

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Kamati ya Rais, suala la ukiukwaji wa taratibu za fidia limejitokeza. Suala hili linaanzia katika Sera yenyewe ya Madini, ambayo haijaeleza kabisa jinsi Wananchi wanaoishi sehemu zenye madini watakavyofidiwa kupisha shughuli za uchimbaji. Sera inaelezea tu fidia itakayotolewa endapo shughuli za utekelezaji wa Mradi wa Mwekezaji zitaharibu mali. Mwekezaji ndiye mwenye jukumu la kulipa fidia.

Malipo ya fidia kwa wanaopisha shughuli za uchimbaji yanalipwa kwa kutumia Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999, kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni za Ukadiriaji Fidia *(The Land (Assessment of Value of Land for Compensation) Regulations)* za Mwaka 2001, zilizotolewa kwa Tangazo la Serikali (*Government Notice*) Nambari 78 la Tarehe 4 Mei, 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Rais, kuhusu maboresho ya suala la ulipaji wa fidia kwa wanaopisha shughuli za madini. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ulipaji fidia kwa wanaopisha shughuli za migodi uwekwe katika Sera na ufafanuliwe katika Sheria ya Madini. Aidha, Sheria ya Madini iweke masharti kuwa ulipaji wa fidia hii uambatane na upatikanaji wa makazi mapya na ujenzi wa miundombinu katika makazi hayo. Sheria itamke bayana kuwa mwenye jukumu la kulipa fidia ni mwekezaji ambaye atajumuisha gharama hizo katika gharama za mgodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika Sheria ya Madini kuhusu ulipaji wa fidia ni pamoja na :-

(i) Fursa ya mmiliki wa ardhi kufanya majadiliano na Mwekezaji chini ya uangalizi, ushauri na usimamizi wa Mamlaka itakayoundwa;

(ii) Kuweka masharti kwamba Mwekezaji asianze shughuli za uchimbaji kabla hajakamilisha fidia na makazi mapya;

(iii) Tathmini ya fidia izingatie ongezeko la thamani ya ardhi kutokana na ugunduzi wa madini katika eneo husika;

(iv) Mali za mhusika pamoja na gharama nyingine zinazoambatana na uhamisho huo;

(v) Malipo ya fidia yafanywe na Mwekezaji/ Mmiliki wa Mgodi; na

(vi) Muda maalum wa kulipa fidia usizidi miezi sita tangu tahmini ilipofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ishirikiane na Wamiliki wa Migodi na kuhakikisha kwamba, madai ya Wananchi yanalipwa mara moja ili kupunguza kero na mvutano ambao unatishia amani na utulivu katika maeneo ya migodi; kwa mfano, Geita, Nyakabale, Kakola na Nyamongo, wapo wananchi ambao hawajalipwa fidia na makadirio yalikwishafanyika tangu mwaka 2001 migodi ilipoanzishwa na yamepitwa na wakati kwa sababu ukadiriaji unawekwa katika miezi sita, sasa toka mwaka 2001 mpaka sasa hivi ni muda mrefu kuzidi kung’ang’ania makadirio ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi ijayo, utaratibu uliotumika katika eneo la Buzwagi uboreshwe kwa kuwapatia wananchi maeneo ya kufanya shughuli za kiuchumi, huduma za jamii, miundombinu na burudani, badala ya kuwaacha wananchi wenyewe kujitafutia mahali pa kuhamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taarifa ya Kamati ya Rais pia inapendekeza kuundwa kwa Mamlaka ya Madini, basi Kamati yangu inashauri kuwa, kutokana na ukweli kwamba uwezo wa mwananchi wa kawaida kujadiliana juu ya thamani halisi ya mali *(Bargaining Power)* zake kwa ajili ya fidia ni mdogo, basi Mamlaka itakayoundwa iwe pia na jukumu la kuwasaidia wananchi hawa kupata haki stahiki kulingana na sehemu ya ardhi wanayomiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri na kusisitiza kuwa, Serikali itengeneze mazingira mazuri yatakayomwezesha mwananchi anayeonesha nia na uwezo wa kununua hisa katika mradi husika na kwamba Mamlaka husika iwasaidie kuwaelekeza kuhusu matumizi ya faida ya hisa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Rais imezungumzia kwa kirefu kuhusu Wachimbaji Wadogo, utengaji wa maeneo yao na mipango ya kuwasaidia wachimbaji hao. Kamati ya Rais pia imebaini matatizo mengi yanayowakabili Wachimbaji Wadogo, baadhi ya matatizo hayo ni kama vile:-

(a) Wachimbaji kutokuwa na mitaji ya kununulia vitendea kazi;

(b) Kutokuwepo kwa vyanzo vya mikopo;

(c) Kuondolewa maeneo yao kupisha Wachimbaji Wakubwa bila kuandaliwa utaratibu mzuri wa kuendelea na shughuli zao;

(d) Kutokuwepo kwa ushirikiano mzuri toka kwa wachimbaji wakubwa hasa kiufundi na kibiashara;

(e) Urasimu katika utoaji wa leseni;

(f) Tatizo la kuhawilisha (*transfer*) ya umiliki wa eneo kwa Wachimbaji Wadogo, kuwapa/kutoa leseni kwa Wachimbaji Wakubwa bila kufuata sheria na kusababisha usumbufu kwa Wachimbaji Wadogo;

(g) Kutokuwepo kwa soko la uhakika la madini kwa Wachimbaji Wadogo; na

(h) Vyombo vya ulinzi na usalama kuonekana kutumiwa na Wachimbaji Wakubwa kuwanyanyasa Wachimbaji Wadogo na pia Wananchi wanaotakiwa kuwapisha Wachimbaji Wakubwa hunyanyaswa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaungana na Kamati ya Rais katika mapendekezo yake mazuri sana kuhusu Wachimbaji Wadogo. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Wachimbaji Wadogo wawezeshwe kupewa mitaji ya kununulia vitendea kazi ili kuboresha kazi za uchimbaji wa madini. Katika hili Kamati yangu inapendekeza kuwa katika gawio la mrabaha, asilimia kumi iende katika kuwawezesha Wachimbaji Wadogo na asilimia hamsini badala ya asilimia sitini iende katika Mamlaka ya Madini itakayoundwa. Kamati inaamini hiki itakuwa chanzo kizuri cha mikopo kwa Wachimbaji Wadogo.

(b) Serikali iwasamehe kodi mbalimbali Wachimbaji Wadogo *(Small Scale Miners*) wanaoingiza vifaa na mitambo ya uchimbaji kama ilivyo kwa Makampuni ya Wachimbaji Wakubwa.

(c) Serikali ikubali kuchangia katika uanzishwaji wa Mfuko Maalum wa Mikopo ya Mitaji yenye riba ndogo kwa ajili ya kuwakopesha Wachimbaji Wadogo. Mfuko huo uchangiwe na Wadau mbalimbali wa maendeleo kama ilivyo katika Mifuko mingine.

(d) Serikali itekeleze uimarishaji wa mafunzo ya ufundi sanifu na kuanzisha mafunzo ya ujasiriamali ili kuwawezesha wazawa kushiriki vizuri katika shughuli za uchimbaji madini.

(e) Serikali isaidie kwa kadiri inavyoweza kuimarisha ushirikiano wa kiufundi au kibiashara baina ya Wachimbaji Wakubwa na Wadogo na hivyo kupunguza migogoro inayojitokeza mara kwa mara.

(f) Katika Muundo mpya wa Mamlaka ya Madini kiwepo Kitengo Maalum cha Kusimamia Wachimbaji Wadogo;

(g) Kuimarisha usimamizi kwa kuwepo Ofisi za Madini hadi ngazi ya Wilaya pale inapowezekana na Wilaya hizo zipewe uwezo *(resources)* na vitendea kazi.

(h) Serikali itekeleze mkakati wa Sera na Sheria inayotaka kutenga maeneo maalum kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo hususan katika maeneo ambayo shughuli kuu ya kiuchumi ni uchimbaji madini kama vile Nyamongo na Nyarugusu.

(i) Sheria na Kanuni za Usalama na Afya Migodini zisimamiwe ipasavyo ili kulinda afya ya Wafanyakazi migodini na kuepuka ajali za mara kwa mara kama ambavyo zimekuwa zikitokea katika maeneo mbalimbali ya Wachimbaji Wadogo, kwa mfano, hivi karibuni Mirerani, Chunya na kadhalika.

(j) Serikali iweke utaratibu wa kisheria utakaowalazimu Wawekezaji Wakubwa na Wadogo kuwakatia Bima za Afya na Ajali kwa Wafanyakazi wao.

(k) Sheria na Kanuni za Mazingira kwa ajili ya uchimbaji mdogo ziimarishwe. Aidha, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, iandae na kusimamia mpango wa utunzaji mazingira kwa maeneo ya uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, inaelekeza kuwa Mgeni haruhusiwi kuchimba Madini ya Vito isipokuwa kwa kushirikiana na Watanzania ambao kwa pamoja wanamiliki hisa zisizopungua asilimia ishirini na tano. Kuruhusiwa huku kwa wageni hakuwanufaishi Watanzania kwa madini waliyonayo. Kamati ya Rais imependekeza kuwa uchimbaji wa madini ya vito uwe ni kwa Watanzania kwa asilimia mia moja. Kamati yangu inaliunga mkono suala hili. Kamati ya Nishati na Madini inashauri na kusisitiza kwamba, uchimbaji huo unaokiuka sheria hiyo usitishwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la kusafirishwa madini ghafi nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za usafishaji na ukataji (uchenjuaji). Suala hili limezua mjadala sana, kiasi cha Kamati yangu kuhoji kama kweli Taifa letu halina uwezo wa kufanya shughuli hizi hapa nchini. Kamati yangu haioni sababu ya kuwaruhusu Wawekezaji hasa wa madini ya vito kusafirisha vito ghafi. Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu, kuiagiza Serikali kuleta Muswada wa Sheria ndani ya mwaka mmoja, ambao utazuia usafirishaji nje ya nchi madini ya vito ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kulipa uzito suala la kuhakikisha kuwa madini ghafi hayasafirishwi nje ili kujenga ajira nchini na hivyo kubakiza kiasi cha fedha ambazo zinapatikana kwa shughuli za madini hapa nchini. Nchi nyingi ambazo hapo awali zilikuwa na madini mengi na sasa madini yamekwisha, mfano

Japan, wanategemea sana shughuli za usafishaji wa madini kujipatia kipato na ajira kwa watu wao. Kamati inaamini kazi hizo zinaweza kufanyika hapa hapa nchini; ni kazi inayohitaji kuandaliwa tu. Ikifanyika hivi, itasaidia pia kujua kiasi halisi cha madini kinachosafirishwa, ikiwa ni pamoja na kuyaongezea thamani.

Imekuwa vigumu kujua kiasi halisi cha madini kitakachopatikana kutoka katika madini ghafi bila kuyasafisha kwanza na kuyahakiki. Kwa msingi huo, Serikali haipati gawio sahihi kwa sababu Mamlaka zetu zitakuwa hazifahamu kiasi halisi cha madini yaliyosafirishwa kwenda kuchenguliwa. Kwa kuanzisha shughuli za usafishaji nchini, kutasaidia hata kupata gawio stahili, kwa sababu Mamlaka zetu zikipewa uwezo zitaweza kufahamu kiasi gani cha madini yaliyosafirishwa nje kwa yale ambayo uchenguaji wake unahitaji rasilimali kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu pia imeguswa na suala la ajira za Wataalamu wa Madini na jinsi wanavyotumika, ikiwemo maslahi na maendeleo yao. Kamati ya Rais imebainisha kuwa kuna malalamiko ya upendeleo katika maslahi baina ya Wafanyakazi Wazalendo na wale wa Kigeni katika Kampuni za Madini bila kujali ujuzi. Pamoja na uchache wa Wataalamu wa masuala ya madini nchini, hao wachache waliopo wapatiwe ajira kwenye migodi iliyopo na wapatiwe stahili zao halali za malipo. Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Rais ambayo ni pamoja na:-

(a) Kutokana na hisia za ubaguzi na upendeleo zinazojitokeza miongoni mwa Wafanyakazi Watanzania, Serikali izipitie upya Sheria za Kazi na kuhakikisha kuwa ujira wa Wafanyakazi unazingatia sifa na uzoefu na si vinginevyo.

(b) Vibali vya ajira kwa Wageni vitolewe tu pale inapobainika kuwa kuna mahitaji na pia utaalamu huo haupatikani hapa nchini.

(c) Kuwepo uratibu *(coordination)* kati ya Mamlaka ya Madini itakayoanzishwa, Idara ya Uhamiaji, Wizara ya Kazi na Kampuni husika ili kufuatilia na kuhakikisha kuwa Wafanyakazi wa Kigeni wanafanya kazi kulingana na vibali vyao.

(d) Serikali ihakikishe kuwa vyombo vilivyoundwa kisheria vikiwemo Vyama vya Wafanyakazi Migodini vinakuwa huru kufanya kazi zake.

(e) Wawekezaji waelimishwe kwamba kuheshimu mifumo rasmi ya utatuzi wa migogoro ni kwa faida yao pia na si kwa faida ya Wafanyakazi tu; kwa sababu kama pana migogoro hata ufanyaji kazi unakuwa ni mbovu.

(f) Serikali iwahimize Wananchi na kuwahamasisha kuepuka vitendo vya uhalifu ili kujenga uhusiano mzuri na kuaminiana na Wawekezaji. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka itakayoundwa, itoe elimu kuhusu ujirani mwema, ulinzi shirikishi baina ya wenye migodi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaamini kwamba, kama Serikali itayafanyia kazi mapendekezo hayo kwa dhati, tatizo la ajira kwa Wazalendo na ubaguzi

wa kimaslahi utarekebishika kwa kiasi kikubwa. Hivyo Kamati inazidi kusisitiza kwamba, Serikali iyafanyie kazi mapendekezo haya mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi. Ipo migodi mingi hapa nchini, ambayo inamilikiwa kwa asilimia mia moja na wawekezaji wenyewe. Kamati yangu inaona hili si sahihi; kwa sababu madini ni mali ya nchi, si busara Serikali kuachia umiliki wake asilimia mia moja kwa Wawekezaji wa Nje. Kamati inaishauri Serikali imiliki asilimia kadhaa za migodi yote na hisa hizi zisimamiwe na *STAMICO*, kama ambavyo Kamati ya Rais imeshauri hapo juu. Vilevile kuna utaratibu wa Kimataifa wa Dola kuwa Hisa ya Heshima (*Golden Share*) isiyochangia, lakini inaipa Dola fursa ya kushiriki katika kutoa maamuzi muhimu. Serikali iangalie utaratibu huu na kuutumia inapokuwa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa ili kuwafanya wananchi nao waweze kuonja faida ya madini waliyonao nchini, ni vyema basi kiasi cha hisa za makampuni hayo zikauzwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Stock of Exchange)* ili wananchi watakaoweza kununua wanunue na kuwa sehemu ya wamiliki wa Migodi hapa nchini. Hili litaongeza hamasa kwa wananchi na itajenga mazingira mazuri kwa migodi hii kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Rais pia imezungumzia hali ilivyo kwa maampuni ya uchimbaji kuuziana hisa. Kamati yangu haina kipingamizi kwa Kampuni hizo kuuziana hisa kwa sababu ni biashara ya kawaida. Hata hivyo, suala ambalo Kamati ya Rais imependekeza lichukuliwe hatua na Kamati yangu kuliunga mkono ni mwenendo na madhumuni ya haya makampuni kuuziana hisa na kubadilisha majina wakati Serikali haipati chochote. Kama kuna unafuu wowote unaopatikana kwa biashara hii na ambao unalikosesha Taifa mapato ni lazima Serikali iliingilie kati. Vilevile Mamlaka inayokusudiwa kuundwa, pamoja na mambo mengine, iwe na jukumu la kuhakikisha kuwa maslahi ya wafanyakazi wa migodi hii yanatunzwa na Kampuni nyingine inayouziwa inazingatia maslahi yao katika Mikataba ya mauziano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuuziana leseni baina ya Wachimbaji Wadogo nalo ni muhimu kuangaliwa na kuratibiwa na Mamlaka inayokusudiwa kuundwa. Hii ni muhimu kwa sababu utafiti wa Kamati ya Rais umebaini kuwa, kuna tatizo pia la wamiliki kutojali hatma ya wafanyakazi wao, mara baada ya kuuza Leseni zao. Hao ni Watanzania, kwa hiyo, hili tusilipuuze; kama tunawabana wawekezaji wa nje hakuna sababu kwa nini wawekezaji hao wa Kitanzania nao wasibanwe na sheria na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uuzwaji wa hisa za migodi iliyopo Tanzania nje ya nchi, Kamati yangu inaunga mkono maoni ya Kamati ya Rais kuwa kufanyike marekebisho katika Sheria za Kodi hususan Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189 na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sura ya 332 ili mauzo ya hisa ambayo yanabadilisha umiliki, pamoja na udhibiti *(controlling interest)* wa makampuni ya nje ambayo kwa namna moja ama nyingine yanategemea rasilimali iliyopo Tanzania yatozwe kodi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu iaamini kuwa, mapendekezo haya sambamba na mapendekezo ya Kamati ya Rais, yataboresha na kuleta sura mpya katika Sekta ya Madini. Kamati ya Nishati na Madini, inaishauri Serikali iyafanyie kazi haraka na kwa umakini unaostahili ili Sheria ziletwe Bungeni kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, napenda kutoa shukrani zetu kwa kutuwezesha kufanya kazi ya uchambuzi wa Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni matumaini yetu kuwa, Bunge lako Tukufu litapata mwelekeo zaidi wakati wa kujadili Taarifa ya Kamati ya Rais, ambayo imewasilishwa humu Bungeni wakati wa Mkutano wa Bunge wa Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Mwenyekiti, Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati ya Rais, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. Kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru kabisa Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa John M. Cheyo, ambao walikubali kushirikana na Kamati yangu kwa siku tatu pale kwenye Hoteli ya Morogoro, kuchambua Taarifa ya Kamati ya Rais na kutusaidia kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo na hivyo kutuweka katika hali nzuri ya kuweza kukubaliana au kuhitilafiana na mapendekezo ya Kamati ya Rais. Hawa ni Wabunge Halisi *(Parliamentarians).* Wakati mwingine tunaposema *Parliamentarians*, wengine wanashangaa ni watu gani! Ningependa ninukuu kidogo kwa sababu nimewataja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa mambo ya *Parliamentary Systems* wanasema kuna aina mbili za Wabunge; kuna Wabunge wanaingia kwenye Bunge wanabaki Wabunge na wanatoka Wabunge, lakini Wabunge wanaoingia kwenye Bunge wanakaa wanakuwa Wabunge halafu wanabadilika wanakuwa Wana-Bunge *(Parliamentarians). Qualities* za *Parliamentarians* ni hizi zifuatazo: *"A Parliamentarian rises above party, focuses on issues, risks through ideas and stays positive."*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa msaada waliotupatia sisi kwenye Kamati, pamoja na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa maoni na michango yao mahiri waliyoitoa wakati wa kuchambua Taarifa hii. Nawapongeza sana kwa kazi kubwa waliyoifanya. Naomba niwatambue Wajumbe walioshiriki kwenye uchambuzi wa Taarifa ya Kamati ya Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo (Mb) - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida M. Bakar (Mb), Mheshimiwa Yahya K. Issa (Mb), Mheshimiwa Asha M. Jecha (Mb), Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya (Mb), Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa

(Mb), Mheshimiwa Mohammed Habib Juma Mnyaa (Mb), Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi (Mb), Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa (Mb), Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko (Mb), Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa (Mb) na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka (Mb).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru sana Kaimu Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashilillah, pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge, kwa kutuwezesha Kamati yetu kuweza kutekeleza jukumu lake bila matatizo. Vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati walioshiriki katika mchakato wa kuchambua taarifa hii ambao ni Ndugu Emmanuel Mpanda, Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Angumbwike Ngw’avi na Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuihudumia Kamati yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba, Kamati ilifanya kazi yake vizuri zaidi na imetupa upeo wa ile Kamati ya Kumshauri Rais ilivyofanya kazi yake. Kwa hiyo, ninao wachangiaji wengi na ningependa kusema hao wanaoitwa Wana-Bunge ndani ya Bunge wapo wengi. Sasa hao waliotambuliwa ni kwa sababu ya kazi maalum hii, lakini wapo wengi, isije ikafikiriwa kwamba wengine ni Wabunge tu. Wana-Bunge wapo wengi sana. *(Makofi)*

Tutaanza majadiliano kama nilivyosema ni kuongeza maoni yetu katika taarifa ile kusudi Serikali iweze kuwa na maoni angalau ya wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, kupata maoni yenu mnazidi kuiongezea nguvu hii Ripoti ya Tume ambayo Rais aliiunda Kamati yake ili iweze kumshauri na sisi tunafanya kazi ya ushauri.

Baada ya kusema hayo, napenda niwataje wafuatao kwa muda nilionao; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Said Amour Arfi, nafikiri tunaweza kumfikia pia na Mheshimiwa Mohamed Juma Mnyaa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru kwa kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Taarifa hii ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Rais kwa kuleta uamuzi huu mzito sana wa kuamua kuunda Kamati hii. Pia namshukuru kwa kuamua kutuhusisha na sisi Wabunge tutoe mawazo yetu katika hili. Nisisahau kuishukuru Kamati ya Jaji Mark Bomani, ambayo imetoa ushauri mzuri. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja mapendekezo yote japo sitaweza kuyazungumza kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekisoma kitabu chote na nimerudia mara tatu, lakini naomba nianze kwa kutoa mifano miwili. Kwanza, mimi ni kati ya wale watu ambao tunasema Tanzania sio nchi maskini lakini walio maskini ni Watanzania. Kwa sababu Tanzania tuna rasilimali nyingi tukiwa tunazungumzia pamoja na madini yetu, madini ni zawadi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, ambayo nchi nyingi hazikuweza kupewa zawadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa kwanza kabla sijazungumza. Naomba tukumbuke katika miaka ya 1960 karibu na mwisho, kule Mkoani Mara kulikuwa na mgodi wa Kiabakari. Ule mgodi ulikuwa wa madini ya dhahabu, wakati ule Rais alikuwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Alipoona mgodi ule ambao ulikuwa upo mikononi mwa Wakoloni hauisaidii nchi yetu ya Tanzania, alitoa amri mara moja ya kufunga mgodi ule na ninakumbuka kabisa Mkuu wa Mkoa alikuwa Mzee Luhangisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa pili, mfano huo ni Malaysia. Malaysia wana bahati ya kuwa na madini mengi sana ya *tin.* Katika miaka ya 1970, Waziri Mkuu mmoja aliyekuwa anaitwa Mahavil Mohamed, alipoona kwamba yale madini yameshuka bei katika soko la dunia na alikuwa anauzia madini yake zaidi Uingereza; akaamua kusimamisha, akafunga migodi yake, akakataa kabisa kuuza yale madini, kwa sababu aliona madini yale hayana faida kwa taifa lake la Malaysia. Akaacha mpaka alipoona amejizatiti vizuri yeye mwenyewe na kama taifa na bei ilipopanda ndipo akaanza kuendelea na uchimbaji wa madini ya *tin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba nijikite kwenye madini ya vito. Sitazungumzia sehemu zote, nitazungumzia madini ya vito kwa Tanzania kwa sababu wezangu wengine watagusia sehemu nyingine. Naomba niseme kwamba, mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia moja mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Mark Bomani kwamba, uchimbaji wa madini ya vito uwe ni kwa Watanzania kwa asilimia mia moja. Ninazo sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza, nikiangalia madini ya vito ya *tanzanite, off course* tuna vito vingi lakini nizungumzie *tanzanite*; ni madini ambayo Watanzania tumejaliwa kuwa nayo sisi peke yetu, ambayo Mwenyezi Mungu ametutunuku kwa wakati huu. Labda baadae yatapatikana nchi nyingine, lakini kwa wakati huu tunayo sisi Tanzania tu. Ukija kuangalia jinsi ambavyo madini haya ya vito yanachimbwa, asilimia 25 ndiyo anaingia Mtanzania, ina maana tulikuwa hatufaidi madini ya vito ya *tanzanite*. Kwa hiyo, naomba mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Mheshimiwa Bomani ya kumshauri Mheshimiwa Rais na mimi kama Mbunge ninayewakilisha wananchi, ninatia mkazo katika mapendekezo yao kwamba, kweli sasa hivi ni wakati muafaka madini haya yachimbwe asilimia mia moja na Watanzania.

Pia sababu inayonipa nguvu ni kwamba, kumbe madini haya yana uwezo wa kuchimbwa na mashine ndogo na vifaa ambavyo si vikubwa sana. Hii ikiwa ina maana kwamba, hata wachimbaji wadogo wa Kitanzania au hata sisi Watanzania wenyewe, tuna uwezo wa kupata *equipments* za kuchimbia madini ya vito. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu kifungu kidogo cha mapendekezo: *“Kutumika kwa mashine kubwa katika uchimbaji wa madini ya vito, kunapelekea kuwepo kwa kwa uchimbaji usio endelevu wa madini hayo. Aidha, madini hayo kuwekwa akiba nje ya nchi, jambo ambalo linaweza kuvuruga soko la madini yetu.”* Naomba nipazungumzie hapo. Hili jambo la kwamba madini hasa ya *tanzanite,* wenzetu wanapovuna kutoka kule Mererani wanakwenda kuweka kwao kwenye *stores* kubwa.

Watanzania wengi tumekuwa tunalifahamu, lakini lazima tuelewe kwamba, madini yanafika mwisho yanakwisha.

Kwa hiyo, kama mfano wa *Tanzanite*, wenzetu wageni wakiwa wanachimba wanakwenda wana-*store* kwenye nchi zao, wakati sisi tutakapokuwa tumeishiwa haya madini kabisa, yale maringo ya kwamba sisi Watanzania ndiyo hasa *supplier* wa *Tanzanite* tutakuwa hatuna tena. Wao walio-*store* kwenye nchi zao ndiyo watakuwa wanazungumza wakiwa wanatembea kifua mbele kwamba, wao ndiyo wenye *Tanzanite* na si Watanzania. Kwa hiyo ni vyema tukaona kwamba, mapendekezo ya Kamati ya Bomani ni mapendekezo endelevu na yanatusaidia sisi kama Watanzania, tuweze kuringa kwamba sisi pekee ndiyo wenye madini. Kwanza, hata ukiangalia jina *Tanzanite* linatokana na Tanzania. Kwa hiyo ni vyema tukaona ni muhimu sisi kumiliki madini haya ya vito bila ya kuwahusisha watu wengine wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna Kampuni ambayo sasa imehodhi kuchimba madini haya Mererani. Nimefanya utafiti wangu mwenyewe usio rasmi, nikagundua kwamba leseni yao inakwisha mwaka 2012. Mwaka 2012 bado ni mbali, ukiangalia hasara tutakayoendelea kuipata mpaka 2012 bado ni kubwa. Ningeshauri kwamba, tunaweza tukasitisha leseni hii tukakubali kuingia kwenye *compensation* ya kulipa *damages* ambayo huenda ikawa ni ndogo kuliko hasara ambayo tutaendelea kuipata mpaka 2012, iwapo hawa Wawezekezaji wataendelea kuchimba madini yetu. Lazima tufikirie jamani, wanaona sasa tupo kwenye Mkakati wa kufanya uchimbaji wa vito uwe *hundred percent* ni ya Mtanzania, lazima watafanya jitihada sana kuhakikisha kwamba huko tuendako tunaondoka sisi. Watayachimba kwa nguvu zao zote mpaka ikifika 2012 huenda yatakuwa yamekwisha.

Kwa hiyo, mimi ninaomba kwanza, niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja kwamba, uchimbaji wa madini ya vito uwe kwa asilimia mia moja, hili nitalirudia; mara mia moja na pia tufike mahali Watanzania tuwe na kitu chetu wenyewe na hawa wachimbaji wadogo nao wapate nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kitu kidogo hakipo hapa; hii mitambo ambayo itakuwa inachimba madini ya vito ni mitambo midogo, iwapo wachimbaji wetu wa Kitanzania itafika mahali watakuwa uwezo wao ni mdogo, Serikali iwakopeshe kwa sababu wanakopesheka. Msimamo wetu uwe palepale kwamba, sasa tuamue kwamba uchimbaji wa madini ya vito urudi mikononi mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote kutoa maamuzi magumu ndiyo kuendelea. Tukiogopa kutoa maamuzi magumu kwa sababu ni magumu, tutakuwa kila wakati nchi yetu inakuwa nyuma. Huu ni uamuzi mgumu, lakini tunaomba tumwambie Mheshimiwa Rais kwamba, uamuzi huu Wabunge wote tunauunga mkono kama ambavyo Kamati imemuunga mkono. Kwa hiyo, atakapotoa uamuzi huu ajue ana nguvu ya Bunge, ana nguvu ya wananchi hata kama *damages* hizo itabidi na sisi tuchangie shilingi elfu kumi kumi tutachanga, lakini turudishe madini ya vito mikononi mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na hoja yangu ilikuwa ni kuongelea madini ya vito. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango mdogo kutokana na hii Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani. Tanzania ni nchi ambayo imeneemeka sana, kama ni bahati basi Mwenyezi Mungu alitupendelea kwa kila namna. *(Makofi)*

Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutambua kilio cha Watanzania cha muda mrefu na ndiyo maana akaamua kuunda Kamati Mahususi kwa ajili ya kuangalia suala zima la madini hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania si nchi ya kuwa omba omba kwa rasilimali ambazo tunazo. Leo hii tumeshindwa kutumia rasilimali vizuri na ndiyo maana hata Bajeti yetu inakuwa inayotegemea michango ya Wahisani ili kuweza kukamilika. Sisi kama Watanzania, tunadhani hatupaswi kuwa huko. Ukitazama mwenendo wa nchi mbalimbali, zilikuwa zinafanya maamuzi mahususi, maamuzi ambayo ni mazito na si ya kaungalia mtu. Ni maamuzi kwa ajili ya maslahi ya Taifa. Sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania na tunamwomba Mheshimiwa Rais, kwa hili tunamuunga mkono na kwamba uamuzi wowote ule ambao una faida kwa Watanzania, sisi wananchi na Waheshimiwa Wabunge tunapaswa kumuunga mkono kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie tu sekta ya madini kwa upande wa dhahabu. Mimi nimepata nafasi ya kushiriki sana katika suala zima la ugunduzi na mpaka kwenye *mining production.* Kwa hiyo, ninaufahamu na uzoefu kiasi cha kutosha na naamini kabisa kwamba, Sheria hii au sera mpya ya madini itakapokuwa imepitishwa, itakuwa imetoa tija kubwa sana kwa Watanzania wote. Ni wapi katika dunia hii mgeni anakuja kumiliki mgodi kwa asilimia mia moja na haina tija katika nchi yoyote ile?

Sisi tumetoa nafasi hiyo. Kupitia Kamati hii, ninaunga mkono sana mapendekezo ya Kamati hii kwamba, huu mpango wa kuachia wageni wamiliki migodi yetu kwa asilimia mia moja lazima tuurekebishe. Tutoe ushiriki wa Tanzania kumiliki migodi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mimi nitakupa mfano kwa Mgodi wa Geita ambao nilifanya kazi. Mgodi wa Geita uliuzwa na Kampuni nyingine ya Ashanti ilinunua kutoka Samans Resources kwa Dola za Kimarekani milioni 232 wakati huo na *share* za ku-*transfer* mgodi huu zikafanyika New York. Tanzania haikupata hata shilingi moja! Nilimuuliza Kamishna wa Mamlaka ya Mapato, Ndugu Kitiliya kwamba, hivi mfumo wetu wa kodi leo hii mgeni anakuja anapata ile leseni ya kumiliki mgodi anaichukua anakwenda ku- *rise* fedha kwenye Masoko ya Mitaji na anasema kwamba amepata mali ambayo akishaanza kuwekeza hapa, yeye haiachii nchi kama faida.

Kwa hiyo, *transfer ownership* inafanyika bila Serikali kupata hata senti tano. Mimi nashukuru sana mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo na kuunga

mkono kwamba, sasa umilikaji wa hisa katika migodi hii lazima nchi iweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kingine ambacho ni cha kusikitisha kidogo ni kwamba, leo mmiliki anakuja kumiliki mgodi anakuta kuna wachimbaji wadogo pale na kuna wananchi wanamiliki ardhi na mali mbalimbali, wao wanafukuzwa au wanapewa fidia ambayo haioani na mali iliyopo hapo; hivi kweli tunawatendea haki Watanzania? Mimi naomba kusema kwamba, suala la umiliki wa migodi litazamwe upya na wananchi wapewe fursa na wao ya kumiliki migodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo siku zote wamekuwa ni kama wakimbizi ndani ya nchi yao, kitu ambacho tunapaswa kukiacha. Mimi nasema kwa sababu hawa watu wana haki yao ni wapiga kura, tuwape nafasi ya kufaidi matunda ya nchi yao. Ninaomba sana kupitia sera hii, watu hawa wawezeshwe. Iwapo mmiliki mkubwa anapewa unafuu wa kodi mbalimbali, unamwambia kwamba unajua wewe zalisha ukipata faida utalipa; hii biashara ya wapi? Haiwezekani; mimi nashauri kwamba unafuu wa kodi wanaoupata wawekezaji wakubwa kwanza tuufute. Kwa nini wapate unafuu wa kodi? Walipe kodi kama kawaida na gharama zao ziingie kama sehemu za uzalishaji ili tuondoe mwanya mkubwa sana wa kukwepa kodi na kuliingizia taifa hasara kubwa sana.

Tumesikia kwenye ripoti hapa kwamba, zaidi ya shilingi bilioni 91 ni msamaha wa kodi kwenye sekta ya madini. Hizi ni pesa nyingi sana zinakaribia zile za *EPA*. Kama zingeenda kuwaendeleza Watanzania na kujenga uchumi huu, tusingemfanya Rais wetu kuwa ombaomba na kwenda kuomba misaada nje. Tungezalisha pesa na kujitegemea wenyewe hapa nchini. Kwa hiyo, tunahitaji kuangalia sana mfumo mzima wa kuweza kutoza kodi zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa moja ya Watanzania tunapenda kuunda Tume nyingi lakini matokeo ya Tume hizi utekelezaji wake unakuwa ni mdogo sana. Ninaomba hii tabia tuachane nayo. Naomba tuwe *more objective* tunapounda Tume na kila Tume izae matunda tunayoyataka, vinginevyo hakuna sababu kutumia gharama kubwa kuunda Tume, lakini mwisho wa siku bado unakuta matokeo ya Tume yanawekwa kwenye makabati, utekelezaji wake unachukua muda mrefu kiasi kwamba unapitwa hata na matukio husika ambayo yalipaswa kuwa yametimizwa. Kwa hiyo, naomba kutumia Tume ya Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani, mapendekezo yake sasa yatekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tumekuwa na Maazimio mengi hapa Bungeni. Azimio la TICTS, Richmond na haya mambo ya EPA, lakini tunataka utekelezaji ufanyike. Taarifa hii ya Kamati ya Mark Bomani, itumike sasa kutoa changamoto ya kuchukua hatua za makusudi ambazo utekelezaji utafanyika mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Makampuni ya kuja kuwekeza hapa upande wa madini yakiwa na mtaji kidogo; mimi nafikiri wale ambao hawana uwezo wa kuja

kuwekeza hapa wasije kabisa. Hatutaki wawekezaji wa kuja na *briefcase*. Mtu anapokuja kuwekeza hapa katika sekta ya madini, basi awe na mtaji kweli. Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo imependekeza na inaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Jaji Bomani kwamba, walau wawe na mtaji usiopungua dola milioni 600. Mimi naunga mkono kabisa, kwa sababu hii itatoa nafasi ya kuwaengua wawekezaji ambao ni uchwara. Watu wameigeuza Tanzania kama Shamba la Bibi; wanakuja hapa wanavuna wanaondoka; huo mchezo ufe.

Naomba Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu sasa lazima tukae chonjo. Hii *Mining Development Agreement* ilikuwa inatufunga kamba na imetuingiza mkenge sehemu nyingi sana; ilikuwa Mwekezaji akishasaini *MDA* anaona sasa ameshamaliza kila kitu. Naomba sasa tuzingatie kwamba mtu anaposaini Mkataba huu, tuweke uhai wa Mkataba wake na tuweke nafasi ya kuweza ku-*review* Mkataba wake unakwenda namna gani, kwa faida na kwa maslahi ya nchi hii. Isiwe mtu anafunga Mkataba miaka 25 hakuna kumpandishia kodi. Wanafanya *tax immunization* kama mtu anavyochanjwa chanjo ya kinga ya kutokulipa kodi. Ninaomba hii biashara iishe, lazima itoe fursa ya kuweza kufanya *review* na pale ambapo ameshindwa ku-*perform* tuweze kubatilisha Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchangiaji eti Halmashauri husika inapewa dola 200,000 kwa mwaka; huu ni utani jamani, ndiyo maana hata wenzetu kule Tarime walikuwa wanagoma na wanaishambulia migodi. Tuangalie *irrelevance* ya mchango wa hawa watu katika mapato ya nchi hii. Hivi Halmashauri kama ya Geita leo hii unaipa dola 200,000 kwa mwaka eti mchango wa mgodi kwenye Halmashauri; dola 200,000 kwa mwaka ni kitu gani?

Rasilimali zilizopo pale na mali zilizozalishwa pale zinaoanishwa vipi na mapato ya wananchi wa eneo husika? Tungesema kwamba, walau *percent* fulani ya mapato yao ndiyo itumike kuilipa Halmashauri husika na sio kuweka dola 200,000; ni hela kidogo sana. Mimi naomba hili tujaribu ku-*review* na kuwa na kiwango ambacho kinakuwa kinabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni suala la ku-*control* hii *external accounts*. Hawa Wawekezaji wamepewa nafasi ya kuwa na akaunti nje ya nchi, ambayo inatumika kwa ajili ya kuuza na kugharimia gharama za uwekezaji. Hii ni sehemu mojawapo ambayo imejenga mwanya mkubwa sana wa watu kutorosha pesa kupeleka nje. Mimi nashukuru pendekezo la kwamba walau asilimia sabini ya fedha yote ya mauzo ya nje irudi hapa nchini, ikirudi hapa maana yake ni kwamba, Mabenki yetu yatapata kazi, Watanzania watapata kazi na kutakuwa na *variation* na *vibration* ya *circulation* ya pesa katika nchi hii. Benki tunazo ambazo zina hadhi ya kimataifa na zinaweza kuhudumia bila matatizo yoyote; kwa nini pesa ziwekwe nje badala ya kuwekwa hapa Tanzania? Mimi naunga mkono kabisa suala hili, tulikomalie na hapa hakuna mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Mikataba mipya. Mimi nakubaliana kabisa kwamba, sasa hivi jamani chonde chonde, hakuna Mkataba mpya wa madini mpaka Sheria mpya ya Madini imepita kwanza ili tuweze kuuendeleza uwekezaji

tutakavyotaka sisi wenyewe. Nchi kama Ghana ambayo ilikuwa inazalisha dhahabu, leo hii dhahabu imekwisha wamefaidika nini? Leo unakuta Ghana wanalia na wanajuta kwamba tulikuwa na dhahabu nyingi sasa hivi hatuna. Haya madini yanakwisha, sasa Tanzania tusiwe na sisi Shamba la Bibi kwamba, wanakuja wanavuna wanaondoka halafu tunakuja kulaumiana.

Mimi nashauri kwamba, Kampuni yetu ya *STAMICO* tuiwezeshe kiwe ni chombo ambacho kitasaidia kuangalia maslahi ya Watanzania katika Sekta ya Madini. Sasa usipokuwa na chombo chako wewe mwenyewe; *whom do you trust?* Unawaachia wageni waamue wanavyotaka wao na matokeo yake ndiyo hayo, wataweka wataalam wao watasafirisha nje wanavyotaka wao na bado Tanzania tunabaki tunalia. Huu sio muda wa kulalamika, umefika muda muafaka sasa tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sehemu ambayo inavujisha mapato ya nchi hii kama mafuta yanayokwenda kwenye migodi. Mafuta yanaingia; aidha nusu yanatumika kwenye migodi au nusu yanaingia kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, naomba niseme kwamba, nilikuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Rais ya kushughulikia suala la Sekta ya Madini, kwa hiyo ninaomba ni-*declare interest* kabisa.

Pili, napenda kupokea pongezi ambazo Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini imezitoa kwa Kamati ya Rais chini ya Uenyekiti wa Jaji Bomani. Wenzangu wote hawapo, kwa hiyo, kwa niaba ya wenzangu walio Wabunge na wasio Wabunge, napenda kuishukuru sana Kamati na pia Waziri kwa pongezi ambazo amezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naomba kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati, sitaweza kuwataja majina kwa sababu ya muda. Zipo nyakati ambazo zilikuwa ngumu sana kwa sababu tulikuwa tuna watu ambao wapo Serikalini, lakini baadae tuliweza kuweka maslahi ya taifa letu mbele na kuweza kufikia Ripoti hii ambayo tumeitoa, ambayo Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini imeonyesha kwamba ni Ripoti nzuri sana.

Pili, binafsi napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais si tu kwa kuunda Kamati ile bali kwa kuniteua. Kwa sababu alinipa fursa ya kuweza kuijua Sekta ya Madini na kuweza kutoa mchango wangu katika maendeleo ya taifa letu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na kama hasikii, Mheshimiwa Waziri Mkuu atampelekea shukrani zangu, hasa ukizingatia kwamba Rais aliniteua katika Kamati hii nikiwa nimesimamishwa Ubunge. Kwa hiyo, ilikuwa ni heshima kubwa sana kwangu kwa yeye kuweza kuniteua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wasemaji wawili waliopita kuhusiana na nafasi ya Sekta ya Madini katika uchumi wa taifa letu. Sekta hii imekuwa ni moja ya

sekta ambazo zinakua kwa kasi sana. Kati ya mwaka 2000 – 2006, Sekta ya Madini ilikuwa kwa wastani wa asilimia 15; mwaka jana sekta hii imekua kwa asilimia 10 na imeshuka kwa sababu mgodi wa Buhemba ulifungwa na vilevile hapakuwa na uwekezaji mpya ambao umepatikana baada ya kuwa migodi mingine yote imeshaanza uzalishaji.

Sekta hii inachangia asilimia 44 ya mapato ya mauzo ya nje ya taifa letu, lakini inachangia asilimia 3.5 ya pato la taifa. Sasa hapo ndipo swali hasa na kitendawili kinapokuja; inakuwaje sekta inayokua sana na inayochangia takriban nusu ya mauzo yetu nje, inachangia kidogo sana katika pato la taifa? Jibu rahisi ni kwamba, Sekta ya Madini ipo mbali sana na sekta nyingine za uchumi. Katika jambo ambalo Serikali lazima iliangalie kwa kina ni jinsi gani ya kuhakikisha kwamba Sekta ya Madini inakuwa na mahusiano na sekta nyingine za kiuchumi.

Taarifa ya Hali ya Umaskini Nchini *(Poverty and Human Development Report)* ya mwaka 2007, naomba ninukuu inasema: *"There is no indication that expansion in mining has triggered significant growth in local economies or influenced poverty reduction."* Hii ni kwa sababu ya *lack of forward and backward linkages*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo huwezi kusema toka tumeanza uwekezaji kwenye Sekta ya Madini ni kiasi gani imeweza ku-*stimulate* ukuaji katika sekta kwa mfano ya kilimo. Ni vipi ambavyo wakulima wanaotoka maeneo ambayo yana madini wanafaidika moja kwa moja na uwekezaji mkubwa? Mlisikia lawama mbalimbali za wananchi kuhusiana na makampuni ya madini kuagiza hata nyanya kutoka nje, kitu ambacho kwa miaka miwili iliyopita sasa kimebadilika. Kumekuwa na baadhi ya maeneo, kwa mfano, Kahama ambapo sasa akina mama wameanza shughuli za bustani kwa ajili ya kuweza kufanya ugavi wa baadhi ya vyakula kwenda katika migodi, lakini kuna baadhi ya maeneo bado ni tatizo; kwa mfano, nyama mpaka sasa migodi takriban yote Tanzania inaagiza nyama kutoka Kenya.

Nyama inayoagizwa kutoka Kenya ni ng'ombe ambao wamenunuliwa Tanzania, yaani Wakenya wamekuja kununua ng'ombe Tanzania wakaenda kwenye machinjio yao wakauza, waka-*park*, wakarudisha Tanzania. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo ni lazima tuliangalie na kuweza kuona ni vipi ambavyo Sekta ya Madini inahusiana na sekta nyingine. Hatuwezi kufaidika na madini kwa kodi peke yake, haiwezekani. Mnaweza mkakusanya kodi mtakavyo, lakini bado *impact* yake kwenye ukuaji wa uchumi mpana haitaonekana. Njia pekee ya kufaidika na ukuaji na Sekta ya Madini ni kuhakikisha kwamba, sekta nyingine za uchumi zinaendana na Sekta ya Madini. Hapa tuna mfano mzuri sana wa umeme; lawama ambazo tunazo sasa hivi, tunapoteza fedha nyingi sana kwa kuwasamehe kodi wawekezaji kwa sababu ya kuagiza mafuta ya kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Geita peke yake wakizalisha kwa kiwango cha asilimia mia moja, wanahitaji takriban *megawatt* 37 za umeme. Kanda ya Ziwa kwa ujumla wake na kama uzalishaji wa Kabanga Nickel ukianza, tutahitaji Megawatt 200 za umeme kwa ajili ya Kanda ile tu kwa Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Mwanza. Kwa hiyo, lazima tunapokuwa tunapanga tuweze kuangalia tunaisaidia vipi

*TANESCO* iweze kupeleka umeme kule, kwa sababu hili ni soko ambalo lipo tayari na hapo ndipo unapokuja kwenye hoja nzima ya kuangalia kwamba katika Kanda ya Ziwa wenzetu wanafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Rwanda wana gesi yao ile *methanol*, wana mpango wa kuzalisha *megawatt* 300 za umeme. Rwanda peke yake hata ikiwa *industrialized* namna gani, haitazidisha kutumia *megawatt* 150 kwa sababu sasa hivi wanatumia *megawatt* 38 mpaka 40 za umeme. Kwa maana hiyo ni kwamba, tayari Rwanda wameshaona kuna soko Kabanga Nickel kwa ajili ya umeme. Kwa hiyo ni lazima tuweze kupanga mambo yetu kwa kuangalia na upana wake na ndiyo jinsi ambavyo sekta hii itaweza kutusaidia.

Kuna mambo ambayo ningependa Waheshimiwa Wabunge wayatilie mkazo kiasi chake; kwa mfano, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, imependekeza kufanya uchunguzi maalum kuhusu uuzaji wa hisa za Mgodi wa Bulyanhulu. Mheshimiwa Dkt. Chegeni amezungumzia hisa za Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bulyanhulu ulikuwa ni Mgodi wetu uliokuwa unamilikiwa na *STAMICO*. Tukaiondoa *STAMICO* katika kufanya shughuli yoyote ile. Hisa asilimia 85 wakapewa Kampuni ya *Starton Resources*, asilimia 15 wakabaki nayo *STAMICO*, ambayo ikawa chini ya Msajili wa Hazina. Kampuni ya *Starton Resources* ikawekeza Dola milioni 20 katika Mgodi ule. Miaka mitatu baadae wakauza Mgodi wa Bulyanhulu kwa Kampuni ya sasa ya Barrick kwa Dola milioni 348. Mtu ambaye amewekeza Dola milioni 20, kapata ziada Dola milioni 328. Serikali ya Tanzania haikupata kodi hata senti tano kwa sababu zote hizi ziliuzwa kupitia Soko la Hisa la Toronto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono kabisa Kamati ya Nishati na Madini kuamua kufanya uchunguzi maalum, kwa sababu hata jinsi tulivyouza hizo hisa asilimia 15 zilizobakia, kunatia mashaka makubwa sana. Hisa asilimia kumi tulizi-*exchange* na sheria ya kodi kuhusu *Withholding Tax* kwamba, hatutapata *Dividend*, kwa hiyo ni bora tupate *Withholding Tax*. *With-holding Tax* hatupati, hiyo *Dividend* haijawahi kutangazwa kwa sababu Bulyanhulu hawajapata faida. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho ningependa Kamati iweze kukiangalia, isiiangalie Bulyanhulu peke yake.

Kamati ya Nishati na Madini ikitaka kufanya uchunguzi ulio kamili, ifanye uchunguzi wa Mgodi wa Buhemba, pale ndio kuna tatizo kubwa sana. Kuna tatizo kubwa kwa sababu si tu Mwekezaji wa Buhemba ameondoka bila kulipa wafanyakazi, bila kufanya taratibu za kufunga Mgodi, kuathiri mazingira, Wananchi wa Buhemba sasa hivi wana matatizo makubwa ya vyanzo vya maji, kwa sababu ya yule Mwekezaji. Vilevile kuna fedha ambazo sisi tuliwapa wale wawekezaji, ndiyo hiyo mnayosikia kashfa ya Meremeta. Kamati yetu imeonyesha katika taarifa yake kwamba, tumeshindwa kufahamu ni nini hasa kilitokea katika umiliki wa Mgodi wa Buhemba na uhusikaji wa Kampuni ya Meremeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna haja kubwa sana; naliomba Bunge lako Tukufu, wakati Kamati ya Bunge ya Madini inafanya uchunguzi kuhusiana na mazingira ya Bulyanhulu, wafanye uchunguzi pia kuhusiana na mazingira ya Mgodi wa Buhemba. Wakati huo huo Serikali kwa haraka iwezekanavyo, ilipe mafao yanayostahili wale wafanyakazi wa Buhemba ambao mpaka sasa bado hawajalipwa. Vilevile kuna malalamiko katika Mgodi wa Bulyanhulu kuhusiana na jinsi gani ambavyo wananchi waliondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia pekee ya kuondoa mashaka ya kwamba malalamiko haya ni sawa ama si sawa ni kwa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kufanya uchunguzi maalum, kwa sababu kuna watu walikuja kwenye Kamati ya Mzee Bomani, wakajieleza wazi wazi kwamba ndugu zao walifukiwa kwenye mashimo, lakini mpaka leo hakuna uchunguzi wa Kiserikali ambao ulifanyika. Kwa hiyo, ningependa pia Kamati ya Nishati na Madini katika uchunguzi wake, ihusishe uchunguzi kuhusiana na kama kweli kuna wananchi ambao walifukiwa katika mashimo pale Bulyanhulu na kuweza kuona hatua gani ambazo tunaweza kuzichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni *role* yetu; ningependekeza ifikie wakati, inapokuja Miswada ambayo ni ya kitaalam sana, Kamati za Bunge ziruhusiwe kuajiri *Consultants* kwa ajili ya kufanya *Impact Study* ya ule Muswada, kwa sababu leo tunapozungumza tunapoteza kodi kwenye Migodi ni kwa sababu ya Sheria ambazo tumezipitisha sisi wenyewe. Sheria ambayo Mheshimiwa Shellukindo ameizungumza hapa kuhusiana na ile asilimia 15, *Clause* ambayo tumeitoa tukairudisha na tulibishana hapa sana wakati wa hoja ya Buzwagi kuhusiana na hiyo *Clause*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii TRA wametufahamisha katika kipindi cha miaka 10 iliyopita tumepoteza Dola milioni 883 kwa kodi ambayo imeshindwa kukusanywa, kwa sababu ya kipengele hiki cha sheria ambacho tulikipitisha ndani ya Bunge. Kwa hiyo, kuna haja kubwa sana, maana haya ni makosa tumeshayafanya, hata tufanye nini makosa yameshafanyika; cha msingi ni kuweza kuangalia mbele kuona ni jinsi gani ambavyo makosa kama haya hayajirudii kwa sababu tunakwenda kwenye gesi, tunakwenda kwenye mafuta, kuna Migodi mingine zaidi inakuja, kuna Mkataba Mpya unatakiwa kusainiwa wa Kabanga Nickel, Mwanza tena wamegundua Nickel nyingine, Kigoma Kijiji cha Mwamgongo wamegundua Nickel na baadhi yao wamegundua Uranium. Mikataba hii itakapoingiwa, kama hatujaweza kuwa tumejiwekea utaratibu ambao Kamati za Bunge zitaweza kupata ushauri wa kitaalam, tunaweza kujikuta tunarudia makosa ambayo tuliyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, kama nitatumia dakika mbili za mwisho ni kuhusiana na suala la *Ring Fencing*, Mzee Shellukindo amelizungumza. Ningependa kutoa mfano dhahiri ili Wabunge waweze kufahamu na wananchi pia waweze kuona. Suala la Mgodi wa Tulawaka unaomilikiwa na Kampuni moja na Kampuni hiyo hiyo ndiyo inayomiliki Mgodi wa Buzwagi. Ukisoma Ripoti hii ya Kamati ya Rais, utagundua kwamba fedha ambazo zilikuwa zilipe kodi Tulawaka, ndiyo zimejenga Buzwagi. Rekodi zetu zinaonyesha kwamba, *Investment* ya Buzwagi ya *400*

*million USD* imeletwa na *Pangea Minerals,* ambayo ni Kampuni Tanzu ya Barrick. Ukiisoma hii Ripoti unagundua kwamba, kwa sababu ya ukosefu wa *Ring Fencing*, gharama za ujenzi wa Buzwagi zilikuwa zinaingizwa Tulawaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha nakushukuru sana.

Naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Rais na Mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi nitoe mchango wangu katika hoja hii. Kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuweza kuunda Kamati hii ya Nishati na Madini ya Jaji Bomani. Pia naishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Nishati na Madini, ambayo na mimi natangaza *interest* nikiwa ni mbia, kwa kazi waliyoifanya kuichambua shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imedhihirika kwamba, Kamati hii ya Jaji Bomani ilifanya kazi kubwa sana na kutokana na maelezo ya *summary* ya Mheshimiwa Waziri leo, Kamati zilizoundwa zilikuwa nyingi na hii ni ya tano. Hizo zote nyingine zilianza kufanya kazi au mapendekezo yake yaliweza kufanyiwa kazi, lakini hakuna iliyokamilika. Sasa tumegundua kwamba, hii Kamati aliyoiunda Rais ya Mheshimiwa Jaji Bomani, imejumuisha Kamati hizo nyingine zote na utekelezaji wa mapendekezo kusita kwa sababu moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, Kamati ya Nishati na Madini iliyokaa Morogoro, imeichambua kwa kina na kwa ujumla imeweza kugundua kwamba kuna mambo tisa makubwa na muhimu zaidi. Pamoja na kwamba yapo mambo mengi katika Ripoti ya Kamati ya Jaji Bomani, lakini masuala ya msingi yalikuwa ni kuhusu Sera ya Madini, Sheria ya Madini, Mikataba, umiliki wa Migodi, uharibifu wa mazingira, vivutio kwa wawekezaji, ulipaji wa fidia, wachimbaji wadogo wadogo, pamoja na madini ya vito. Haya yote yamepewa ama yamepatiwa ufumbuzi na Mheshimiwa Rais kupewa mapendekezo halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja nitangulize kulisema; Tanzania tuna matatizo ya urasimu. Jambo linaweza kupendekezwa, lakini uchukuaji wa hatua ukachukua muda mrefu sana mpaka wakati ukapita likapoteza maana. Mfano halisi, Bunge lako hili Tukufu lilipendekeza miaka mingi sana, toka mwaka 2005 kwamba, kwa mfano, Kitengo cha Tansort kilichopo London kirejeshwe nchini, ni hasara kubwa; ilichukua muda mrefu mpaka Serikali kukubali. Serikali imeshakubali na sina hakika mpaka hivi sasa kimesharejeshwa hapa nchini na kila siku kuna sababu kwamba hakijakamilika kitu hiki; huu ni urasimu mkubwa.

Bahati nzuri hivi karibuni tulipotembelea Kanda ya Ziwa kwenye Migodi hiyo, hata wale wa Williamson Diamond nao wanakiri kwamba waliiarifu Serikali miaka saba iliyopita kwamba, Kitengo kile kinagharimu vibaya sana kirejeshwe hapa Tanzania. Kwa

hiyo, huo ni ushahidi kamili. Kwa maana hiyo, tunaomba huo urasimu ambao umekuwa ni silika ya Tanzania, uondoke mara moja na hatua zichukuliwe kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza Sera ya Madini ina upungufu, tuna maana ya mambo mengi. Tunaposema kwamba haiwezekani Kampuni inatoka nje kuja kuwekeza hapa si suala la *Utopia* kwamba, inawekeza angani; inawekeza hapa ardhini, ardhini ya nani ni ya Tanzania. Inakuwaje leo Serikali hata kama imejiondoa katika biashara, lakini wewe Serikali utegemee kodi tu kwa mali inayochimbwa ndani ya ardhi yako? Huo ni udhaifu, haiwezekani!

Wenzetu wa nchi jirani za Kiafrika hivyo hivyo Botswana, hawategemei mapato kutoka kwenye madini kwa pato la kodi tu. Hata ule umeme wakitoa kutoka masafa fulani wakipeleka katika mgodi, gharama zile za *investment* ya umeme ule tayari wanaongeza kama ni hasara zao, pamoja na madini yaliyomo inakuwa ni *share* za Serikali. Kwa maana hiyo, tunaposema Sera zifanyiwe marekebisho zina upungufu, suala moja zito ni hilo.

Madini mengine yaliyotajwa kama hayo ya chuma, mkaa na nickel ni madini ambayo Duniani kote nchi ambazo zinajivunia zina *flying roads*, zina viwanda vikubwa, basi madini ya chuma yanahitajika. Madini mengine hayo ndiyo yenye chanzo na msingi wa maendeleo ya nchi, haiwezekani yaachiwe mwekezaji tu. Kwa hiyo, tunaposema Sera ya Madini ibadilishwe haraka, tuna maana hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema Sera kutokuwa bayana na wasemaji wengine wazungumzia pia kwamba, haya madini ni kitu kinachomalizika, inakuwaje hatuna mipango au Sera leo tuchimbe madini kwa kiasi gani, mpaka lini na tuache kiasi gani kwa kizazi kijacho?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ikiwa tunampa mwekezaji kila mahali, hapo pana upungufu. Ushahidi kamili wa upungufu huo wa Sera ni kwamba, kwa mfano, kule Geita kuna Kijiji cha Nyakabale kiliandikishwa mwaka 1989, Kijiji hiki kikapata hati Namba 644 mwaka 2000. Wamekwenda Ashanti Gold Mine, Kijiji kina hati ya kuwepo kwao pale, Ashanti nao wamepewa umilikaji wa leseni yao. Kwa hiyo, Kijiji kipo ndani ya leseni ya Ashanti, wao wanatakiwa waondoke. Wakihitajika waondoke, wakapewa masharti ya kusaidiwa hiki, inakuwaje leo Kijiji kilichopo pale kwa muda mrefu mwekezaji apewe eneo la ndani ya Kijiji halafu wanakijiji waamriwe kuondoka; ni kitu cha kuchekesha; kwani tuna haraka gani?

Itakuwaje vijiji ambavyo vipo juu ya madini vikibakishwa ili mwekezaji apewe maeneo mengine; na maeneo hayo yatakapomalizika, ushiriki wetu na uwekezaji wetu katika hii migodi mikubwa hapo baadae hatutaweza kupata uwezo na hivyo vijiji tuwahamishe kwa utaratibu mzuri nasi tupate hiyo ardhi tuchimbe madini yaliyobakia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukizungumza kuwa kuwe na sera endelevu ni kwamba, haya madini si lazima yamalizike leo; ni lazima tujue na baadae tunaweza kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera Mpya tunayoihitaji ni ile ambayo itawezesha vivutio siyo katika uchimbaji, iweze kuleta vivutio katika utafutaji madini. Kuwekwe vivutio vingi katika utafutaji wa madini, kama hiyo misamaha iwekwe katika kutafuta na kutueleza wapi pana madini gani na kwa kiasi gani.  Katika uchimbaji, hivyo vivutio vilivyowekwa ambavyo vinatupunguzia mapato ni lazima sasa viondoshwe. Sera Mpya tunataka i-*focus* huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hivyo vivutio, mwenzangu ametoa mfano, kuna Mgodi huu wa Geita kwa mfano; unatumia umeme MW 37.  Mimi nilipokwenda kuangalia, wastani wa MW 30, inakaribiana hapo hapo. Sasa kuna *IPTL* hapo wanatumia mafuta tani 15,000 kwa mwezi, ambao wanatoa MW 100. Hawa wanaotoa MW 30 takriban wanatumia tani 4,500 za mafuta kwa mwezi. Hawa kama wanapewa msamaha, Mheshimiwa Shellukindo ameshataja msamaha wa kodi wanaopewa, lakini tani 4,500 kwa mgodi mmoja; je, hii migodi ikiwa mitano, sita, saba, wakati wapo kwenye *process* ya *production* halafu wanapewa msamaha wa kodi; hili si suala zuri na linafaa lifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia hii Mikataba ya MDA, inaonekana kwamba siyo *Mineral Development Agreement*, inaonekana ni *Mineral Devastation Agreement*, kwa sababu inatukandamiza. Leo inakuwaje mikataba hii iweze kuwa inazidi sheria ya nchi, ina nguvu kuliko sheria ya nchi?

Endapo Sheria ya Kodi inasema asilimia 15, Mkataba huu unasema asilimia tatu na wanatozwa asilimia tatu; tunaacha ile Sheria ya Nchi, hapo kidogo ni kichekesho! Kwa maana hiyo, hapo ndipo tunaposema pia na hii mikataba ibadilishwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la fidia, mpaka hivi sasa linaleta matatizo na mapendekezo yametolewa. Maana ya mrabaha hasa, kwanza tuondokane na hii dhana ya kuwa mwekezaji afanye kila kitu.  Wawekezaji wengi mpaka hivi sasa wanasema wanafanya *community development* na sana sana watataja kujenga shule, *dispensary* na visima vya maji safi; ndiyo mambo yao makubwa.  Huu mrabaha hasa maana yake ni kule kijijini kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, mapendekezo ya Kamati ya Kamati ya Nishati na Madini kwamba, Serikali mapato yake ni kodi, mrabaha unatakiwa uwepo kule.

Kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Madini na kuongezea mapendekezo ya Rais kule ni kwamba, Mamlaka ya Madini itakayoundwa ipate asilimia fulani; asilimia fulani iende kwa Halmashauri na asilimia nyingine iende kwa wachimbaji wadogo wadogo. Tuondokane na huu mrabaha kwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la fidia; sera ya sasa ni kwamba miti inatathminiwa; kiwango cha mwembe ambao mpaka kuzaa unachukua miaka mitano/kumi/kumi na tano, bei yake ikawa shilingi 20,000 mfano au viwango vingine, hailingani na thamani na lazima ilete manung'uniko kwa wananchi. Inafaa kabisa hivi sasa ardhi yoyote ambayo chini kuna madini, vipando vilivyopo katika ardhi hiyo

haiwezekani viwe sawa sawa na ardhi ambayo haina madini. Mwananchi akipewa fidia, thamani ile iwe tofauti. Hilo ni suala la kufikiriwa na kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani iwe leo mwananchi yule ambaye ana vipando vyake vile anapewa fidia ambayo kwanza, anaachiwa mwekezaji mwenyewe kuamua. Leo kuna migogoro imetokana na fidia kutopitia katika mkondo mzuri wa Halmashauri na Serikali ikahusika ipasavyo. Leo anaachiwa mwekezaji huyu anampa thamani ya mti ule au thamani ya ardhi kwa 120, mwingine anapewa 150, ni lazima migogoro iwepo. Halafu Serikali iwaangalie Wakuu wa Wilaya, walio wengi wanahusika katika migogoro hii. Serikali isifiche ukweli, itazame na yatatuliwe matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la fidia linaleta migogoro.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ninazo dakika kumi, sasa naona nikimwachia mtu dakika kumi, asije akanidai dakika tano. Kwa sababu hiyo, tutaahirisha mpaka saa 11.00, tukirudi nitakuwa na wasemaji wafuatao: Kutakuwa na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Mzeru Nibuka. Hawa ndio wasemaji nilionao na wanatosha kwa jioni.

Waheshimiwa Wabunge, naomba Wenyeviti wa Kamati zote tuwe na kikao baada ya kuahirisha hivi sasa, yaani Kamati ya Uongozi, kuna jambo la dharura ambalo inabidi tulijadili.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ambayo tuliyaanza asubuhi. Mchangiaji wetu wa mwanzo kwa jioni ya leo atakuwa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer ma Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge ajitayarishe.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie Taarifa ya Waziri wa Nishati na Madini, inayohusu Kamati ya Jaji Bomani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, kama walivyoanza wenzangu; kwa kuunda Kamati, lakini pili kwa kukubali Taarifa hii ijadiliwe hapa Bungeni. Nadhani hili ni jambo zuri na linatupa fursa ya kutoa mchango katika jambo hili kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuhudhuria mkutano mmoja wa wafanyabiashara wa sekta binafsi wakasema kwamba, Sekta ya Madini ni sekta ya dola trilioni moja. Hii inaonyesha kwamba, sekta hii inaweza ikatusaidia kubadilisha uchumi wa Taifa letu, kama sera zetu na Sheria zetu na kanuni zetu zikiwa muafaka katika mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta ni muhimu na mimi nimefurahi kwamba, tumeanza kuijadili kwa urefu na mapana namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ningependa kujikita zaidi katika utekelezaji wa sera za msingi za CCM katika miaka ya 2000 - 2010, ambayo inazungumza mambo makubwa mawili. Kwanza, inazungumzia juu ya kujenga uchumi wa sasa na Taifa linalojitegemea, lakini jambo la pili kubwa ni lile la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Nilipokuwa nasoma Taarifa hii, nadhani kuna *omission* ambayo nimeiona hasa katika ukurasa ule wa 68 katika eneo la rejea. Fedha ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2004 na Sheria ya Uwezeshaji Uchumi 2004 hazikutajwa kabisa. Mimi nilifikiri kwamba, Sekta ya Madini ni nzuri katika kumwezesha mwananchi kiuchumi, kwa maana ya kuwaongezea kipato lakini pia kuwaondolea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili haliwezi kufanya vizuri na hata rafiki yangu Mheshimiwa Shellukindo alipokuwa anawasilisha maoni yake, suala hili la uwezeshaji wananchi kiuchumi halikuonekana kwa dhahiri. Sasa nataka kulitilia mkazo hili ni muhimu na lazima tuliweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sekta mojawapo ambayo inaweza kuongoza katika kuwawezesha wananchi kiuchumi ni Sekta ya Madini, Sekta ya Miundombinu, Sekta ya Viwanda na Biashara, Sekta ya Maliasili na sekta nyingine, lakini hizi nne ndiyo zenyewe katika kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda, nimefurahishwa na pale panaposema kwamba tuwe na sheria ama sera ambazo zitawapa fursa Watanzania. Wanakamati hapa wametumia neno uzawa, sisi hatukutumia neno uzawa wakati tunaandaa sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na sheria yake, lakini hao jamaa wanatumia. Katika kutumia neno uzawa, nadhani msingi hapa ni kuwawezesha watu wadogo wadogo ambao ni wanyonge, washiriki katika uchumi wa nchi yao na kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwamba, Kamati hii ya Jaji Bomani imezungumzia kwa kirefu sana suala la wachimbaji wadogo na mimi nataka kuongezea wachimbaji wa kati. Wachimbaji wadogo na wa kati ni lazima tuwafanyie mipango na maelezo au maelekezo ya mipango yapo katika Ilani ya chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya Sera ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo na zana za kisasa; hili hatujalifanya vizuri ni lzima tulifanye sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lililozungumzwa mle ni kuwa na sera madhubuti ya kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata fursa ya kuchimba madini katika maeneo yao. Sasa hivi utakuta jamaa wakubwa hawa wakija wachimbaji wadogo wanawafukuza. Kule kwangu kuna mfano wa vijana ambao ndiyo waliogundua madini; baadhi yao ndioyo wale waliouawa pale Dar es Salaam. Wale wameondolewa kitaalamu, *of course* kwamba ninyi hamjui sheria, hamna nini wakaondolewa. Ungetarajia Serikali ya CCM ambayo ni ya wanyonge ndiyo ingewasaidia hawa wapate eneo lile lakini hawasaidiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hawa wachimbaji wadogo wasaidiwe na wasaidiwe kwa namna ambayo kwanza, wanaweza kupata mikopo lakini pia na soko la uhakika. Hivi sasa kuna benki mmoja ndani ya nchi inaitwa FBME, imeanzisha kitu kinachoitwa *fair trade gold centres*, zipo nne zimeanza; moja ipo Mwanza, mbili zipo Geita na nyingine ipo Bukombe Ushirombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti lengo la hizi *gold centres* ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata soko lakini baadaye wapate mikopo ili wapate zana za kisasa za kuchimbia. Kama tunazungumza suala la ujenzi wa uchumi wa kisasa, mojawapo ni matumizi ya zana ya kisasa au teknolojia ya kisasa. Sasa hili nalo halifanyi vizuri, kuna fikira kwamba wanaofanya shughuli hizi au benki kama hii ingepata motisha ili nao waweze kuwapa motisha zaidi wachimbaji wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hawa tunawabana, hawataweza kufanya kazi ambayo tunawatarajia waifanye. Tatizo kubwa ambalo halikusemwa vizuri humu ni biashara ya magendo ya madini. Kubwa zaidi ni hawa wachimbaji wadogo; *Artisan Gold Miners* au *Tanzanite*. Ndugu yangu pale Mbunge wa Same Mashariki alikuwa anasema kwamba, tupige marufuku upelekaji wa *Tanzanite* nje. Mfano mzuri aliutoa Mheshimiwa Mramba hapa, lakini hakufanikiwa kwa sababu haitoshi kupiga marufuku tu ni lazima muwe na mikakati mizuri ambayo itaongeza thamani ya madini hapa ndani ya nchi.

Hivi sasa benki hii inaanzisha mradi wa kuchenjua *gold* na baadaye kutengeneza vito kutokana na *Gold* kama pete na mkufu. Ndani ya nchi mkifikia hapo kwa eneo la vito, mnaweza mkapiga hatua kubwa lakini mkisema tukataze tu, hamuwezi kufanikiwa kwa sababu magendo yapo makubwa sana hapa. *Money launderers* wale ndiyo wanaonunua dhahabu yetu kwa sehemu kubwa ndani ya nchi na hata kwa majirani zetu; sasa hawa tusipowabana vizuri tusitarajie mafanikio katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la uwezeshaji wa kiuchumi wananchi lipatiwe fursa kubwa. Kwenye Sheria hii ya Uwezeshaji Kiuchumi kuna kitu kinachoitwa *National Economic Empowerment Council* na *National Economic Fund, Fund* hii haijapata pesa, imepata shilingi milioni 400 ambazo hazitoshi; ni lazima ipate fedha nyingi ili iwawezeshe wananchi hawa kuchangia katika sekta hii la sivyo hatuwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwazuia wageni kushiriki katika bidhaa fulani ambazo zingetengwa kwa ajili ya Watanzania tu lipo tayari. Sheria ya mwaka 2004 inasema kwamba, Baraza la Uwezeshaji likitamka kwamba bidhaa fulani ama shughuli fulani zifanywe na Watanzania tu, basi zitafanywa na Watanzania kwa kutangaza kwenye *official gazette*. Kwa hiyo, siyo suala la kutunga. Ninasema ni lazima tuzihusishe sheria zote hizi ili tuweze kuwa na matokeo na mafanikio ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba niseme mambo mawili ya umiliki wa Serikali. Ninakubali umiliki wa Serikali unaweza kusaidia hasa kwa mfano kupitia *STAMICO* na *NDC*. Pale *NDC* tulijaribu sana kutengeneza sheria hatukufanikiwa, sasa labda mtengeneze Sheria ya *NDC* ambayo inawapa fursa ya kuwa mwekezaji mkubwa, *participant* katika sekta ya madini *(heavy metals)*, ili awe mbia katika sekta hii kwa kuliwakilisha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *focus* iwe katika kumuwezesha mwananchi mmoja mmoja ama kupitia makampuni yao, ndiyo sera yetu tusirudi sana nyuma kwenye ubinafsishaji na utaifishaji; maana tukirudi huko tutapata matatizo kidogo kwa mazingira ya sasa. Kwa hiyo, mkazo uwe katika kuyawezesha makampuni ya Tanzania makubwa na ya kati kama hayo, ili tufikie uwezo wa kushiriki katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hisa ndogondogo kama asilimia tano, kumi, ishirini, zinaweza kuendelea kuwa za Serikali kwa kutumia huo msingi wa *current interest shares*. Hiyo inawezekana lakini baada ya hapo mtashindwa ni lazima mtakuwa mna-*contribute* na serikali haina uwezo mkubwa sana wa kuchangia kwenye makampuni binafsi. Kwa hiyo, mkazo uwe katika sekta binafsi na sasa tuongeze juhudi katika suala lile la *Public Private Partnership*. Hilo nalo tumelizungumza sana, lakini bado hatujalifanyia maamuzi. Sasa hili ndilo eneo zuri la kuwawezesha Watanzania kushiriki katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni rasilimali watu; naomba suala hili katika Sekta ya Madini nalo litiliwe mkazo kwa sababu ni muhimu sana watu wetu kushiriki katika teknolojia ya kisasa ya uchimbaji madini, bila kufanya hivyo hatuwezi kufikia malengo tunayoyatarajia. Hata hawa wageni, kama watu wetu hawataweza kushiriki humo basi tutaongozwa zaidi na wageni kuliko Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja ya Waziri. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Taarifa ya Madini ya Kamati ya Rais inayohusu masuala ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Kamati ya Jaji Bomani, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Wamepita katika maeneo yote yanayohusika; wamekutana na watu

mbalimbali, wamefanya kazi kubwa sana ambayo Mbunge anaamini kwamba ni taarifa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naipongeza Kamati ya Mwenyekiti Seneta Shellukindo, kwa taarifa nzuri waliyoileta na si taarifa hii tu, wamefanya kazi kubwa sana katika Wizara hii ya Nishati na Madini na taarifa yao kwa kweli tunaipongeza kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na mgawanyo wa mapato ya mauzo ya madini. Madini yalikuwepo tangu Mungu aiumbe dunia hii na Tanzania ametuwekea madini mengi sana, uvunaji unaendelea kila wakati lakini bahati mbaya sisi hatufaidiki wanaofaidika ni wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tathmini ukilinganisha faida na hasara, nadhani hasara ndiyo kubwa zaidi kuliko faida, waliofaidi ni wageni. Taarifa hii imebainisha kwamba, Watanzania hatukunufaika kabisa na madini, kila mtu ameiona na tunaikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii imebainisha udhaifu wa udhibiti wa mapato ya madini; hapo nashangaa kidogo kwa sababu tuna Wizara tuna wataalamu, tuna *TRA*, sidhani kama kungetokea udhaifu mkubwa namna hii, ikawa wageni ndiyo wanafaidi bila sisi kuona kwamba hapa tunadanganywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mikataba tunayowekeana na wawekezaji sana sana udanganyifu huu unatokea katika mikataba hiyo. Kwa kuwa imezungumzwa sana katika Taarifa hii, ningeomba sasa tujisahihishe ili usitokee tena mwanya kama huo kwa sababu bado tuna madini, tuna migodi mingine ambayo bado haijaanza kuchimbwa, kuna inayoendelea; nadhani tuitumie Taarifa hii kuziba mianya ili tufaidike na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la ushirikishwaji wa umiliki wa migodi. Hapa ni kama tunapeana migodi bure, *royalty* tunayopata ni kidogo sana. Tungependa sasa umiliki uwe wa kwetu na wakati mwingine ile asilimia 50 ya mwenye mali ambayo tumeipoteza tumempa mwekezaji yote asilimia mia moja, sasa ile asilimia 50 iwe ni kwa kila mgodi, hiyo siyo *royalty* tena ni asilimia 50 ya mapato ya mgodi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ambalo limetajwa kwenye Taarifa ni Serikali kuitumia *STAMICO*. *STAMICO* ilikuwepo tuliiua sisi wenyewe, sasa ni wakati muafaka kuwe na *STAMICO*, chombo ambacho kitadhibiti madini yote na kitawasomesha wataalamu wetu. Si vyema kutumia wataalamu kutoka nje, tuwasomeshe watalaamu wetu, wapo wengi sana, lakini ukitegemea wataalamu kutoka nje kila wakati; kwanza unawapata wataalamu ambao si wazuri, unawapata wataalamu ambao hawana nia nzuri na nchi yetu, unawapata wataalamu ambao ni wezi. Kwa hiyo ni afadhali kuwasomesha wataalamu wetu ili tuweze kuwatumia na pia tuwe na watafiti wetu. Nina hakika kwamba, vijana wetu wakisoma, watafanya kazi hii ya utafiti kwa maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Sera ya Madini. Sera hii irekebishwe na tukuweke ushirikishwaji kwa wananchi na kumtambua mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchimbaji mdogo hatambuliwi katika Sera hii ya Madini; sasa ni wakati muafaka watambulike na wasaidiwe. Tunawasaidia matajiri wakubwa na kila siku tunapiga kelele hapa Bungeni, lakini Taarifa ya Jaji Bomani imethibitisha hilo kwamba, hakuna msaada wowote tunaowapa wachimbaji wetu wadogowadogo, ambao ndiyo tunawategemea na ndiyo walalahoi na wanasaidia uchumi na ajira ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ushirikishwaji wananchi katika madini ya vito. Hapa ningependa kusema kwamba, madini ya vito yanapopatikana nchini yote yanasafirishwa kwenda kukatwa nchi za nje; kwa nini ukataji usifanyike katika nchi hii na vito vinatoka hapa, vinasafirishwa kwa njia ambayo hata Serikali haijui vinasafirishwaje? Naomba sasa tusikae kama matajiri waliotosheka, sisi ni maskini na tutajirike na mapato ya nchi yetu, tusikae tu kushuhudia watu wengine wakivuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulizungumzia suala la kurejesha sehemu ya mapato ya mrabaha katika Halmashauri zetu. Halmashauri zetu hawaoni chochote na wala haihesabiki kabisa kwamba kuna mapato ambayo yanatakiwa yaende katika Halmashauri. Uharibifu unatokea katika maeneo yetu, hiyo siyo hisani na wala si ombi; ni lazima Halmashauri wapate mapato kwenye machimbo yote yaliyopo katika maeneo. Kuna hii dola laki mbili ambayo wanapewa Halmashauri, nadhani ni Halmashauri chache sana ambazo zimepata. Kule kwangu kuna mgodi lakini hatujawahi kupata hata senti na sijui kama watu wanafahamu kwamba kuna Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni uharibifu wa mazingira kwamba, wenzetu wanapofanya utafiti, kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira. Wanaharibu na kuondoka, kungekuwa na fidia ya uharibifu wa mazingira, kwa sababu wanaoachiwa mazingira yale ni wananchi wa sehemu ile. Kwa hiyo, uharibifu wa mazingira ufidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya muda kwisha, ningependa kuzungumzia suala la fidia, sijui ni nani huwa anaenda kufanya *evaluation* ya fidia ili wananchi wafidiwe; kwa sababu fidia inayotamkwa pale ni kama vile kifuta jasho; kuna tofauti ya fidia na kifuta jasho kwa wananchi kutokana na uharibifu wa tembe mashambani? Kwa hiyo, huwezi kulinganisha uharibifu wa hekari moja na makazi ya mtu ambaye unamhamisha akaanze makazi mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa hii imeelezwa bayana kwamba, fidia inayotolewa kwa wananchi ni ndogo sana. Naomba Bunge hili lipitishe fidia ambayo wananchi wanapaswa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni muda wa utekelezaji wa taarifa hii. Mheshimiwa Rais, alitangaza kwamba ameunda Tume wakati analifungua Bunge hili; sasa tunakaribia miaka mitatu ndiyo tunakuja kuijadili Taarifa ya Tume hiyo; miaka mitatu sasa utekelezaji sijui utafanywa na Awamu ya Tano sijui!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba, Taarifa hii ikishapitishwa itekelezwe haraka iwezekananyo. Ukifika mwaka 2010 tuwe karibu tumekwisha-*cover* mapendekezo yote yaliyotolewa na Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema tusichelewe tena, mapendekezo mazuri yamepitishwa na yataleta faida sana kwa wananchi endapo yatatekelezwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ningependa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye taarifa hii muhimu ambayo inahusu shughuli za madini katika nchi yetu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuunda Tume hii ili kuangalia suala zima la shughuli za madini katika nchi yetu. Nadhani alifanya vile kwa uzalendo wa kuona kwamba, mali hii ya madini itumike na iwasaidie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru sana Kamati na Tume iliyoundwa na Rais, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na wametuletea Taarifa ambayo kimsingi imegusa maeneo yote na kuonyesha upungufu wote. Nadhani kazi kubwa ni kufanyiwa kazi kama walivyopendekeza wenzangu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Kamati ya Nishati na Madini, ambayo asubuhi wametueleza mambo mengi; jinsi walivyoiona Taarifa hii kwa namna ambavyo inatakiwa ifanyiwe kazi ili iweze kuokoa mali zetu. Kwa hiyo, naanza kwa kusema kwamba, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za madini ni ngumu sana, hasa kwa nchi changa ambazo zinaendelea kama Tanzania. Ugumu huu tunaushuhudia pale unapojionyesha kwenye mikataba. Mikataba mingi ina utata na mahali pengi inaleta matatizo kati ya wamilikaji wakubwa na wadogo. Vilevile tunaona kwamba, kwenye mikataba hii ndipo wananchi wanapoona mali zao zinaporwa kwa sababu hawaoni kama wananufaika na madini yaliyopo kwenye nchi yetu.

Vilevile wananchi wameona kabisa kwamba, wanaporwa mali hizi kwa sababu mazingira yao yanaharibiwa. Wachimbaji wakiondoka wanatuachia mashimo. Nadhani kwa mtazamo wangu huenda hii ilikuwa ndiyo hoja ya msingi kwa Marehemu Baba wa

Taifa, kuahirisha shughuli za uchimbaji wa madini katika nchi hii hadi hapo Watanzania watakapokuwa na maarifa ya kuchimba na kusimamia shughuli zao wenyewe.

Hii pia inajidhihirisha hata kwenye vitabu vya maandiko matakatifu, pale tunapomwona Hosea akisema watu wangu wanaangamia kwa sababu ya kukosa maarifa. Kwa hiyo, hoja yangu kubwa inajielekeza sana kwenye tatizo la kutokuwa na maarifa katika shughuli hizi za madini. Yapo matatizo ambayo tunayaona ya kutokuwa na wataalam wa kitanzania kwenye shughuli za utafiti; yapo matatizo ya kukosa teknolojia zetu sisi wenyewe; yapo matatizo ya watalaam wetu kutokuweza kuandika vizuri mikataba inayolinda maslahi ya nchi yetu kwa sababu tunatakiwa tuwe na watalaam ambao wakikaa na Mjapan kuandika huo mkataba, Mjapan anapomaliza kutia sahihi na wa kwetu akimaliza kutia sahihi, basi aondoke akijua kwamba ametia sahihi kwa kutetea maslahi ya Tanzania. (*Makofi*)

Yapo matatizo katika uchimbaji; migogoro ambayo tumesema kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo; yapo matatizo katika uuzaji, hatuna utaalam huo katika usimamizi ambao kwa sehemu kubwa ni mkubwa zaidi. Katika uchunguzi wangu, pamoja na matatizo hayo yote ambayo yapo kwenye mikataba, pamoja na matatizo ya kutokuwa na wataalam, lipo tatizo moja kubwa ambalo nadhani hata ile Tume labda ilisema kwa namna moja au nyingine, lakini haikuweka wazi. Hili ni tatizo la kukosekana kwa uzalendo wa kiuchumi *(Economic Patriotism)* na hii naweza nikatoa mfano mmoja wa kilio cha miti; wakati wote wanaona kama shoka ndiyo linalokata miti na kuiangamiza. Shoka haliwezi kuangusha miti peke yake bila kuchomekwa kwenye mpini uliotengenezwa kwa mti. Kwa hiyo, mpini na shoka vinashirikiana kwenda kuuangusha mti.

Hoja yangu hapa ni kwamba, wenzetu watendaji ambao wamekuwa wakipewa fursa ya kuandaa mikataba, kuisimamia na kuandaa mambo mbalimbali, basi kuna mahali hawafanyi inavyotakiwa ama kwa sababu zao binafsi katika maslahi kama vile kusaini na kupewa asilimia fulani. Kwa hiyo, nilidhani hili ni tatizo kubwa ambalo tunatakiwa tuli-*address;* ni namna gani tutaweza kuweka uzalendo kwa wenzetu ambao watakuwa wamepewa kazi hii. Itakuwa haina maana hata kama tutaleta sheria mpya, lakini kama hakuna uzalendo, hiyo sheria inaweza ikatumika vilevile kwa kutekelezwa isivyo sahihi kwa sababu bado sheria ikitengenezwa inabidi ikatengenezewe *regulations* ili iweze kutekelezwa.

Kwa hiyo, ikipita kwa wale wenzetu ambao hawana uzalendo wataipindisha tu na tutaendelea kupoteza mali za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la kwanza namba tukubali kuanza upya. Tulifanya makosa tumeyagundua, kwa hiyo, tuanze upya. Wenzetu wale ambao labda hawatekelezi majukumu yao vizuri, hawawajibiki vizuri, basi wakubali sasa kufuta yale makosa yao kwa kubadilika na kuwa na tabia nzuri, kwa ajili ya kujenga taifa letu na kulinda mali za Wananchi wa Tanzania. Kama wewe ulikuwa unatia sahihi kwenye mkataba baada ya kupewa asilimia kadhaa, basi tabia hiyo uiache tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili ni kwamba, sasa hivi tufanye kazi kubwa ya kutibu vidonda tulivyonavyo tusifanye kazi ya kuongeza vidonda vingine. Maana yangu ni kwamba, tushughulikie mikataba yenye utata, ile mingine ambayo inafikiriwa kuanzishwa isitishwe, tusifanye hiyo kazi sasa ili tujihakikishie kwamba tumeweka njia nzuri kwa ajili ya kufunga mikataba mingine baadaye ambayo inaweza kufuata taratibu zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendelezo langu la tatu, wameongea wenzangu na mimi nakubali na ndiyo la msingi; tukiimarishe chombo chetu cha *STAMICO*, hatuna namna kwa sababu kupitia *STAMICO* tunaweza kuandaa wataalam wa kisasa na kutafuta vyombo vya kisasa na teknolojia za kisasa. Tunaweza kuimarisha utafiti na kuwaandaa Watanzania kuwa na uwezo au kuwa na maarifa ya kuzisimamia mali zetu wenyewe.

Vilevile ni kweli kwamba, sisi hatuna uwezo pengine wa kuandaa wataalam katika kiwango cha kuweza kufanya utafiti na kugundua aina mbalimbali za madini. Zipo nchi ambazo zimetusaidia sana wakati wa ukombozi wa Bara la Afrika. Wakati mwingine unaweza ukawapeleka Watanzania kwa marafiki wa kweli kama China, wakasomeshwa vizuri na wakatusaidia kutuletea teknolojia za kisasa kwenye uchimbaji wa madini yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la nne, ni ukweli usiopingika kwamba, lazima hiyo sheria ije. Sheria ya Madini na Sera vipitiwe upya. Sheria ndiyo msahafu wa utekelezaji wa shughuli zote, bila sheria hatuwezi kufanikiwa. Kwa hiyo, naunga mkono maoni ya Tume kwamba, Sheria iandikwe upya na Sera ziletwe upya kwa ajili ya shughuli nzima ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niongezee kwamba, katika Sheria hiyo tunaomba ibainishe wawekezaji wanapokuja kufanya utafiti katika nchi zetu mara nyingi kufika kwenye maeneo wanatumia barabara ambazo zimejengwa na Serikali yetu kwa kutumia kodi za wananchi. Wanapita kwenye madaraja yaliyojengwa na Serikali yetu kwa kutumia kodi za wananchi. Kwa hiyo, kimsingi Serikali pia ni mwekezaji, ana hisa katika ule utafiti unaofanywa na yale makampuni. Kwa hiyo, sioni sababu kwa nini haya makampuni ya wawekezaji yanakuwa na lugha kwamba, hawawezi kuchangia shughuli za maendeleo eti kwa sababu sheria haisemi hivyo.

Tunaomba sheria iliangalie hili ili uwekezaji wa miundombinu uliopo kwenye zile sehemu uwe ndiyo mtaji wa Serikali au hisa za Serikali kuweza kuingia kwenye hiyo mikataba na hayo makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tumekuwa tukisema kwamba, katika kukua kwa uchumi wetu sehemu iliyochangia sana ni Sekta ya Madini. Sasa angalia mwenyewe kama tunasema madini yamechangia, pamoja na matatizo haya tuliyonayo ya ubovu wa mikataba, rushwa, migogoro; ina maana tukirekebisha hili, mchango wa madini utakuwa ni mkubwa zaidi ya hapo na tunaweza kuishi kwa raha kabisa na kutatua matatizo ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja hii na nashukuru kwa kupewa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii finyu ya kuweza kuzungumza machache kuhusu Ripoti ya Kamati ya Rais kuhusu madini. Awali ya yote, ningependa kuwapongeza walioshughulikia tatizo zima la madini, hususan Mheshimiwa Shellukindo na timu yake, kwa kuweza kuleta haya ambayo yapo mbele yetu. *(Makofi)*

Nikiangalia Ripoti nzima, nasema ni kazi nzuri; *well done*, lakini kuna kipengele kidogo tu ambacho kinanipa wasiwasi mkubwa. Siyo mimi tu pengine na wale walioshughulikia Ripoti nao wamepata kigugumizi kuongea kuhusu suala hili. Tatizo lenyewe ni Buhemba, leo ni miaka minane nazungumzia Buhemba. Kuna kamati zilizotangulia kama nne zinakwenda Buhemba lakini ripoti tunayopata hairidhishi kabisa. Nilidhani hii Ripoti ya Rais, ingeweza kutupa matumaini makubwa kuhusu tatizo zima la Buhemba. La kushangaza ni kwamba, Kamati yenyewe imeshikwa na butwaa; haikusema lolote la muhimu kuhusu Buhemba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu wanasema wamejaribu kupata maelekezo kutoka Serikalini lakini hawakupata ufumbuzi mzima. Ningependa kunukuu: "Kamati haikupata maelezo ya kina na ya kuridhisha kuhusiana na uanzishwaji, umiliki na ufilisi wa Kampuni ya Meremeta na hatimaye uanzishwaji wa Kampuni ya *TANGOLD* zilizosajiliwa nje ya nchi." Sasa kama Kamati ya Rais, imeshindwa kujua kitu gani kinaendelea Buhemba; je, mimi Mbunge nitapataje hiyo Ripoti? Rais mwenyewe hajui kinachoendelea Buhemba, Wananchi wa Buhemba hawajui, Watanzania wenyewe hawajui, Wapinzani ambao pia walikuwa ndani ya Kamati wameshindwa kunipa tatizo la Buhemba ni nini? *(Makofi)*

Nilidhani kelele za nje wakienda ndani watatupa ukweli kwamba Buhemba kuna nini, wao wamekuja mikono mitupu! Haya ndiyo nataka niwaambie wananchi wangu wa Buhemba kwamba, Serikali haijui kinachoendelea Buhemba na baadaye mnasema niunge mkono hii Ripoti, mimi nasema siiungi mkono maana fedha zilizoibiwa Buhemba ni nyingi mno zinazidi hata zile za *EPA* zinazozungumziwa.

Wananchi wanapata tabu Buhemba; shule zimebomolewa, zahanati zimebomolewa; na nani? Naambiwa kuna ubia kati ya Serikali na Wazungu wa Afrika Kusini, lakini hawajui makubaliano yalikuwaje kati ya Serikali na hao waliokimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Buhemba leo unakuta mashimo marefu kweli, kifusi kinazidi hata jengo hili. Dhahabu inachukuliwa, nyingine imefichwa Mauritius, Ripoti inasema Kampuni ya *TANGOLD* imeundwa kinyemela na ipo Mauritius; nani mmiliki wa kampuni hii? Tunachoambiwa Kamati ya Rais imeshindwa kwenda Mauritius na kuchunguza nani anamiliki Buhemba akiwemo Mpinzani. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa wamepewa nini kinachowanyamazisha? Inashangaza kweli, tukiwa Bungeni kelele nyingi, nje wanapewa pipi wananyamaza. Nataka kujua kuna nini Buhemba, Wananchi wanataka kujua? *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ninataka kujua wananchi wananisikiliza; niende nikawaambieje, mwaka juzi nilipiga kelele hapa aliyekuwa Waziri Mkuu akanipa Mawaziri watatu; Mheshimiwa Wasira alikuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Profesa Mwandosya na mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. Tukaenda pale Buhemba kwa ndege tukafika tukazungushwa nikaona wenzangu siwaelewi tena. Wakazungushwa zungushwa na Wazungu mle mimi wakaniacha nje.

Walipotoka wakaniahidi watarudi na Ripoti ya Mazingira; mpaka leo sijaipata hiyo Ripoti! Walirudi wakasema watanipa ripoti kuhusu nani mwekezaji? Mpaka leo sijaipata ripoti hiyo! Sasa tupo hapa ni usanii tunaoufanya ama tupo *serious* na nchi yetu? Ripoti inasema hawajui, ninanukuu mapendekezo sasa ya Ripoti yako ukurasa wa 116: "Kamati inapendekeza kuwa Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu uanzishwaji wa Kampuni ya Meremeta na Tangold, umiliki wa Serikali katika kampuni na Serikali inajichunguza yenyewe na kwamba hizo fedha shilingi milioni 132 waone zimekwenda wapi." Sasa hii ni Ripoti gani?

Hii ndiyo Ripoti tunayoletewa ambayo inatoa mapendekezo kwa Rais, lakini hawajui walichopata wala hawana taarifa yoyote kuhusu mgodi mzima! Huu ni mwaka wa nane nazungumzia juu ya Buhemba. Mimi sikuitwa ingawa nilimchukua Zitto akawa pale Buhemba na wenzake. Nakumbuka walikuwa wanamwambia wewe Zitto, kwetu maana ya Zitto Kabwe ni kakitu kana sumu sana, kakienda kanapenyeza saa ndiyo walivyomwambia Zitto akatoe ripoti kamili ya Buhemba. Hakuna ninachoona humu ndani; sasa nataka kujua maana aliyewapa kazi mnamrudishia kazi bila jawabu; tufunge mjadala? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka zahanati zangu zirudishwe wajenge upya, barabara zangu, shule zangu na fedha zilizoibiwa na kufichwa huko Mauritius zirudi; wananchi wangu angalau wafaidike na hizo fedha au tujue ziko wapi. Hilo ndiyo ombi langu sasa. Vinginevyo, siungi mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Jaji Mark Bomani kuhusu madini. Napenda nichukue nafasi hii, kwanza kabisa, kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa utayari wake wa kupokea mawazo mengine na kuifanya Ripoti hii, kuwa wazi na kuweza kujadiliwa ndani ya Bunge, kwa sababu zimekuwepo Ripoti nyingi za tume mbalimbali ambazo zimekuwa zikizungumzia sekta hii ya madini lakini hazikuwekwa wazi na wala hazikujadiliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa utayari huo wa kupokea mawazo mengine kutoka kwa wadau na Watanzania kwa ujumla wao. Tofauti

kabisa na wakati uliopita, kwa sababu kadhia hii ya Sekta ya Madini si mpya ni ya muda mrefu, imekuwa na manung'uniko na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, lakini kila walipokuwa wakiinua sauti zao kuzungumzia kuhusu eneo hili la madini, waliambiwa kwamba ni wachovu wa kufikiri na wana wivu wa kijinga. Matokeo yake ndipo hapa tulipofika leo. *(Makofi)*

Naipongeza sana Kamati ya Jaji Mark Bomani na Wanakamati, kwa kazi waliyoifanya. Kadhalika pia naipongeza Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, chini Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo. Pamoja na taarifa hizi na maoni ya Kamati yaliyowasilishwa, bado ninayo hofu moja kwamba, mjadala huu ni kusaidia tu kuongeza nyama katika ripoti ambazo zimetolewa au Bunge litatoa azimio kuhusu utekelezaji wa ule upungufu ambao umeonekana ndani ya taarifa. Nilikuwa nadhani ipo haja ya makusudi kabisa, kama Bunge ndiyo chombo cha kuisimamia Serikali, pamoja na kwamba hoja ya kujadiliwa kwa ripoti hii ilitolewa na Mheshimiwa Malecela, lakini leo imeletwa hapa na Serikali, nadhani ipo haja ya Bunge sasa kusema kwamba hiyo hoja ni ya Bunge na Bunge litoe azimio kuiagiza sasa Serikali itekeleze yale ambayo tumeona kwamba yanapaswa kutekelezwa kwa uharaka.

Aidha, maneno ambayo ameyasema sasa hivi Mheshimiwa Mkono siyo ya kupuuzwa na kukaa tunachekacheka tu humu ndani tunafurahia; ni hoja ya msingi ambayo imeletwa kwenye Bunge. Bunge sasa liichukue hoja hiyo na kuunda Kamati za Bunge za kuchunguza migodi yote yenye utata.

Tusiiachie Serikali; Bunge tutimize wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi na kuisimamia Serikali katika kuangalia maeneo ambayo yana upungufu kama huo Mgodi wa Buhemba, haitakuwa na maana kama tutaiachia Serikali ifanye hayo. Ipo haja sasa ya kuunda Kamati Teule ya Bunge ya kupitia migodi yote na mikataba yote yenye utata na kutoa mapendekezo ya hatua za kisheria zitakazochukuliwa dhidi ya wale wote watakaoonekana wamefanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa labda na mimi niongezee tu katika Taarifa ambayo ilikuwa imetolewa katika maeneo kadhaa. Kwa kweli Taarifa ni nzuri, inajitosheleza na imegusa maeneo mengi sana, lakini eneo moja ambalo pia limeguswa ni kuhusu watalaam. Nina mashaka, inawezekana kweli tuna upungufu huo mkubwa wa watalaam, lakini pia ninahisi kwamba wataalam wetu tunawatumia visivyo na inawezekana sana wataalam wakawa wanaitumikia siasa badala ya kutumikia taaluma zao. Matokeo yake wametufikisha hapa tulipofika na leo tunaanza kuwalaumu watalaam. Siamini kwamba nchi hii tuna upungufu mkubwa kiasi hicho cha wataalam, kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kumekuwepo na Kitivo cha Jiolojia kwa zaidi ya miaka 30, sasa bado wanasema kwamba hatuna wataalam. Inawezekana katika maeneo ya hawa mafundi staid, Chuo cha Madini Dodoma hakitoi wahitimu wa kutosheleza kujaza hizo nafasi.

Ukiisoma Ripoti hii ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, unakuta kwamba, kile kitengo cha ukaguzi wa dhahabu kina matatizo ya wataalam na vifaa. Kama hivyo ndivyo, tunafikiri kwamba, hali hii itaendelea kwa muda gani na juhudi gani zinafanywa ili kukifanya kitengo hiki kiweze kutimiza wajibu wake na kuweza kufanya ukaguzi na ili

taifa lisiendelee kupoteza? Ipo haja ya makusudi, kuangalia ni namna gani tunakiimarisha kitengo hiki kwa kupata wataalam hata kama tutalazimika kupata wataalam wengine kutoka katika nchi nyingine za Kiafrika, kama hatuna wataalam wetu wa Kitanzania, lakini ipo haja ya kuangalia eneo hili kwamba linadhibiti na kufanya ukaguzi wa dhahabu ipasavyo.

Eneo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni kwamba, je, kuna udhibiti gani katika madini mengineyo? Taarifa hii imejikita sana katika dhahabu, almasi na vito, lakini si madini hayo tu yanayopatikana katika nchi hii, nchi hii ina madini mengi. Tumeshaona ni namna gani tunapoteza kwenye dhahabu, tumeona tunavyopoteza kwenye *Tanzanite* na kadhalika; sasa tunadhibiti namna gani? Haya madini mengine ambayo tunadhani kwamba si muhimu lakini yana umuhimu na tutaendelea kama taifa kupoteza, kwa sababu hakuna mikakati yoyote inayofanywa au iliyoandaliwa ya kuweza kusimamia na kudhibiti madini mengineyo.

Labda nitoe mfano mdogo tu, Mgodi wa Chumvi Uvinza ulikuwa chini ya *STAMICO* na baadaye ukauzwa kwa bei ya kutupwa. Palikuwa na migodi miwili pale; mgodi ambao ulikuwa unatumia kuni na mwingine ambao ulikuwa unatumia umeme. Mgodi mmoja haujulikani umekwenda wapi, umeyeyuka umebakia mgodi mmoja tu unaotumia kumi, lakini mapato yanayotokana na chumvi yanapungua. Uzalishaji wa chumvi hatujui kwa nini unapungua na hakuna hata mtu mmoja anajishughulisha kutaka kujua ni sababu gani? Kinachofanya taarifa zionekane hivyo zilivyo si uzalishaji kwamba umepungua ni ujanja unaofanywa na wenye kiwanda kile. Sasa hivi chumvi hawauzi kupitia benki; ukiwa na fedha wanakuambia uje na fedha tasilimu wanakupa chumvi. Hii yote ni njia ya kukwepa mapato na kulipa kodi katika nchi hii; tunafanyaje?

Lazima uwepo udhibiti wa karibu zaidi wa kuweza kusimama kama taifa, kama nchi tunapata kodi stahiki kutoka kwa hawa walionunua viwanda, kwanza tumevitupa na sasa wanatuibia kodi zetu. Lazima tuliangalie eneo hili pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hii ada ya huduma *(Service Levy)*, ambayo inatolewa katika Halmashauri zetu ya asilimia 0.3; kiwango hiki ni kidogo sana ni vyema sasa Sheria ya Madini ikatazamwa upya, ikaangaliwa na mapendekezo yote yaliyotolewa juu ya sheria hii yazingatiwe na sheria hii isichelewe. Utashi wa kutaka kuleta mabadiliko katika sekta hii upo, lakini nina mashaka na dhamira ya Serikali ya kutaka kuleta mabadiliko katika Sekta ya Madini. Kama wana dhamira ya kweli, kama wana uchungu na nchi na kama wanawathamini Watanzania kwa ujumla wao, basi eneo la Sekta ya Madini linapaswa sheria zake zirekebishwe haraka iwezekanavyo.

Aidha, eneo lingine ni ushirikishwaji wa wananchi katika ugawaji wa maeneo ya uchimbaji. Eneo hili linasikitisha sana, leseni zinatolewa kutoka Dar es Salaam. Leo ukienda kwa mfano katika Wilaya yangu ya Mpanda, ambayo Mungu ametujalia tuna aina nyingi za madini, lakini maeneo yote muhimu ambayo yanafahamika, yameshagawanywa bila kuwashirikisha wakazi wa Wilaya ya Mpanda, lakini kila eneo limechukuliwa.

Katika hili hoja waliyokuwa nayo wananchi ni kwamba, kuna ulanguzi mkubwa unaofanywa na watumishi wa Idara ya Madini wakishirikiana na watu kadhaa wakiwemo pia viongozi wa kisiasa katika kuhodhi maeneo makubwa ya madini. Eneo hili kwa kweli ni lazima tulitazame, tuangalie ni namna gani dosari hizi tunaweza kuzirekebisha. *(Makofi)*

Mfano mzuri tu wanagawa viwanja vya madini mpaka katika maeneo ya mipaka ya Halmashauri ya Miji. Pale kwangu wameshagawa eneo ambalo kuna chuo cha *VETA*, kuna shule ya msingi, kuna mahakama na kuna tanki la kuhifidhia maji kwa ajili ya Mpanda, kwa sababu ya uchimbaji wa madini. Tunakwenda wapi jamani? Hali hii ni lazima itazamwe na iangaliwe na hatua za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie eneo la utafutaji wa madini, hasa maeneo ambayo yanachukua muda mrefu. Hata katika Ripoti hii hii limezungumziwa hilo kwamba ni lazima sasa tudhibiti, tuangalie mapato yanayotokana na hizo tafiti ili Serikali iweze kupata kodi katika hizo tafiti. Kuna eneo ambalo lipo katika mpaka wa Mpanda na Kigoma, leo utafiti unafanyika kwa zaidi ya miaka 25 kule Kupalagulu na sampuli kila siku zinapakiwa ndani ya meli na ndege zinapelekwa Ulaya. Tunapata nini, tunapoteza nini, nani anasimamia? Maeneo kama haya ni lazima tuyasimamie kwa karibu zaidi ili tuweze kupata mapato kwa ajili ya nchi yetu.

La mwisho kabisa ni utoaji wa leseni na uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wadogo. Kama ilivyo katika sera kwamba, Wizara itakuwa inatangaza maeneo, naiomba sana Wizara ya Nishati na Madini; mpaka sasa kasi ya kutangaza maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo ni ndogo mno; maeneo yaliyotangazwa kwa mujibu wa Ripoti hii hayazidi matano katika nchi hii na nchi hii imejaa madini na wapo wachimbaji wadogo wadogo wamezagaa nchi nzima. Tulikuwa tunaitaka Wizara itambue maeneo haya ya wachimbaji wadogo wadogo na iyatangaze, kwa sababu sasa hivi maeneo yote ya wachimbaji wadogo wadogo yamebebwa na wachimbaji wakubwa, wamechukua leseni kubwa za madini na kuwahodhi wachimbaji wadogo wadogo ambapo kila siku inaleta migogoro.

Migogoro hii pia ipo Mpanda na nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, ipo haja ya makusudi ya kuja kuongea na wachimbaji wadogo wadogo ili tuweze kutatua tatizo la umiliki wa eneo ambalo kwa miaka mingi limekuwa likimilikiwa na hawa wachimbaji wadogo wadogo na sasa limemilikishwa kwa mchimbaji mkubwa, ambaye ameshindwa kuliendeleza. Maeneo haya kama tutayasimamia, tutapunguza kwa kiasi kikubwa manung'uniko ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa aliyoitia Mheshimiwa Waziri leo, amekadiria karibu wachimbaji wadogo wadogo takriban 1,000,000. Hili ni kundi kubwa sana la Watanzania; hawa 1,000,000 wana familia na watu kadhaa ambao wanawategemea. Hatuwezi kuwaacha watange tange kama kuku wa kienyeji; ni lazima wawezeshwe kama kweli tuna dhamira ya kuwasaidia Watanzania na kuwaondoa katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nachukua nafasi ya mwanzo, kukushukuru jioni ya leo kwa kunipa nafasi ya kuchangia Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu ya leo ni kushauri na kutoa maoni yetu kwa kuboresha Taarifa ya Kamati iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, ili pamoja na yale ambayo wenzetu waliyatoa na haya tutakayoyatoa, iweze kuifikisha Serikali yetu mahali pa kuboresha na kuisimamia vyema Sekta ya Madini. Niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa hiyo ni lazima ni-*declare interest,* lakini pia ni Mbunge wa Jimbo ambako madini mengi yanapatikana, yakiwemo madini yale ambayo yamebeba jina la nchi yetu, yaani *Tanzanite.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitachukua nafasi hii ya mwanzo kabisa, kumtambua na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutekeleza dhamira yake aliyoionyesha wakati anafungua Bunge hili mwezi Disemba mwaka 2005. Mheshimiwa Rais, akihutubia Mkutano wa CCM kule Kizota, aliendelea kusisitiza dhamira yake ya kuona kwamba, Sekta ya Madini inahitajika iboreshe maisha ya Watanzania kwa kuchangia katika Pato la Taifa na kwa kuhakikisha kwamba, Watanzania na Tanzania tunanufaika na madini ya nchi yetu, pamoja na wawekezaji ambao nao wamewekeza katika sekta hii.

Siku chache tu baada ya Tamko lake la Kizota, kwa maana alitamka tarehe 3 na tarehe 12 aliunda Tume ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, lakini Rais aliweza kunyamazia tu baada ya kuipokea Ripoti hii na kuifanyia kazi yeye kama Rais. Rais kwa kudhihirisha dhamira yake, ametuletea na sisi tena tuiboreshe ili tuendelee kuishauri Serikali, juu ya namna bora ya kuhakikisha kwamba, rasilimali hii ya madini inachangia katika kuwaletea Watanzania maisha bora, kwa maana ya kuongeza pato la nchi. Baada ya kusema hayo ni dhahiri basi kwamba, dhamira ya Rais ni ya dhati na dhamira ya Serikali ya CCM ni ya dhati na sifa zote zielekezwe kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tuna uzoefu wa kuunda Tume nyingi sana ambazo zinatumia fedha za walipa kodi. Mheshimiwa Waziri Ngeleja, alipokuwa akiwasilisha taarifa yake leo, aliendelea kunukuu sehemu ya taarifa hii kwamba kwa upande wa sekta ya madini, hii ni Ripoti au ni Kamati ya tano. Ilikuwepo Kamati ya Jenerali Mboma, ambayo ilikusudiwa kushughulikia mgogoro uliokuwepo na ambao upo mpaka leo kati ya wachimbaji wadogo wa Mererani na Kampuni ya *AFGEM.* Kinachonishangaza wakati mwingine ni pale unapounda tume na Kamati, inafanya kazi na kuleta ushauri kwako, ripoti hiyo unaikalia na kuifungia kwenye droo!

Moja kati ya ripoti ambayo imefungiwa katika Kabati la Waziri wa Nishati na Madini ni Ripoti ya Jenerali Mstaafu Mboma na leo Waziri ameitaja kwamba, anaijua ipo

na ilikuwa inahusu mgogoro kati ya wachimbaji wadogo na kampuni kubwa ya *Tanzanite One.* Jenerali Mboma, alipendekeza kwamba, alibaini kuwepo kwa mafaili 110 yaliyochomwa moto au yaliyoungua Wizarani na mojawapo kati ya mafaili hayo ni faili lililokuwa linaonesha mpaka kati ya eneo la wachimbaji wadogo na eneo la kampuni kubwa ya *Tanzanite One.* Akasema eneo lile lipatiwe ufumbuzi kwa kushauri kwamba, eneo lile la wachimbaji wadogo lililokuwa limemegwa, lirejeshwe kwa wachimbaji wadogo. Leo ni miaka mingapi tangu Kamati ya Jenerali Mboma imemaliza kazi? Ripoti hiyo inafungiwa kwenye kabati, fedha za walipa kodi zimeungua, halafu leo tunaendelea kusomewa kwamba ni moja kati ya rejea ya leo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kwamba, Tume hizi zinapoundwa zinatoa matumaini makubwa sana kwa Watanzania na ndio maana Watanzania wanajitokeza kutoa maoni yao. Matumaini hayo tunayowapa kwa kuunda Kamati hizi ni lazima yajidhihirishe kwa vitendo, kwa kuhakikisha kwamba, yale tuliyowatuma kuyatafuta basi kwa yale ambayo wameyaona yanafanyiwa kazi. Mpaka leo mgogoro kati ya mpaka huo ni mkubwa na Jenerali Mboma alishauri kwamba, Sheria ya Madini irekebishwe ili kuhakikisha kwamba, uchimbaji wa madini ya vito kama *Tanzanite* ambayo yanachimbwa *horizontally,* sheria ile ambayo inaweka mipaka kwenda *vertically* na kwa kuzingatia kwamba Wizara hiyo hiyo na Serikali hiyo hiyo iligawa maeneo ya wachimbaji wadogo mita 50 kwa 50 irekebishwe. Mpaka leo dhamira ya kubadilisha sheria hiyo haipo, badala yake mwaka 2004 ililetwa sheria ambayo iliendelea kusisitiza kwamba, uchimbaji wa madini ya vito uchimbwe *vertically* badala ya kwenda kwa mshazari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina imani na Kamati hii, kwa sababu ni Kamati ya Rais na kwamba, Rais mwenyewe ninamjua; anaposema jambo anadhamiria kufanya. Ingekuwa sio ya Rais, ningefika mahali pa kuishauri Serikali iachane na biashara ya kuunda Kamati na Tume mbalimbali, mpaka kwanza ifanyie kazi taarifa za tume zilizotangulia ikiwemo hii ya Jenerali Mboma. Kwa nini mnapata kigugumizi pale ambapo mchimbaji mdogo anakuwa na haki dhidi ya mchimbaji mkubwa? Hapo ndipo tabu ninapoiona. Mfike mahali sasa uzalendo utawale na Watanzania kilio chao kisikike. Kuna mapendekezo mengi ambayo yametolewa na Kamati hii ya Bomani, lakini mimi nijikite katika maeneo machache sana, kwa sababu muda wenyewe ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uchimbaji wa madini ya vito na hasa haya ya *Tanzanite.* Kwanza, kuna pendekezo ambalo wametoa kwamba, madini ya vito sasa iwe ni kwa Watanzania. Hivi unapokuwa na madini ya vito kama *Tanzanite,* ambayo yamebeba jina la nchi yako halafu bado hutaki kuiacha ibaki kuwa *Tanzanite* kwa Watanzania; maana yako ni nini hasa? Mimi nilikuwa nafikiri tuishie kukubaliana na Ripoti hii ili tufike mahali ambapo madini ya *Tanzanite* yawe yanachimbwa na Watanzania peke yao. Tuchimbe wenyewe, hatutakuwa tumefanya dhambi na wala sio sisi peke yetu tulioanza haya, nchi za wenzetu walishafanya hivyo.

Ukienda Srilanka, kuna aina ya madini yanayoitwa gauda safaya, wanaochimba ni Wasrilanka peke yao. Nenda Thailand, kuna madini yanaitwa *pink safaya,* wanaochimba madini hayo ni Wathailand peke yao. Mimi nasema mnaweza mkaacha rubi, mkaacha

almasi au mkaacha dhahabu ichimbwe na watu wote lakini madini kama haya ambayo yamebeba jina la nchi, *Tanzanite* ibaki kwa ajili ya Watanzania na tuwafidie wale wengine ambao ni wawekezaji wakubwa watupishe katika biashara hii ya uchimbaji wa madini ya vito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juzi wakati natoka Tarime nilipitia Arusha kwa wachimbaji wangu wa Mererani na kwa wale *master dealers* pale, walinieleza wazi kwamba, kule Marekani na Hongkong, biashara ya madini ya *Tanzanite* sasa hivi imeshuka sana, kwa sababu wana madini mengi ambayo yapo kwenye masanduku yao yameachiwa leo. Sasa kila ukiangalia wachimbaji wadogo, kwa miaka mingi sana hawajatoa madini pale; Kamati ya Bunge iundwe ichunguze juu ya madini yaliyopo huko nje kwamba ni kiasi gani yamekwenda huko?

Ukiangalia kwenye Ripoti ya Jenerali Mboma, unaambiwa kwamba wachimbaji wa *Tanzaniate One* peke yao wanaweza kuchimba kilo 230, lakini mpaka leo kodi ya mrabaha waliyoilipa Serikali ya Tanzania ni dola milioni 1.4 ambayo ni sawa na kama shilingi bilioni mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni mbili hata Sunda aliponunua lile jengo la *Mount Meru Hotel*, alilipa shilingi bilioni sita kama ananunua shati tu. Sasa leo ukiipa kampuni kubwa halafu mnapokea mrabaha wa shilingi bilioni mbili kwa miaka kumi; huo sio wizi wa mchana? Hebu tusaidiane, nafikiri wachimbaji wadogo ni vizuri tukawapa kipaumbele.

Nilipokuwa Tarime, nilitembelea machimbo ya madini kule Nyamongo, kilio cha wachimbaji wadogo kwa rafiki yangu Mheshimiwa Charles Mwera, nakupongeza bwana ulinishinda ndugu yangu maana nilitaka usishinde, lakini bahati mbaya umenishinda. Sasa nilipotembelea kilio cha wachimbaji wadogo kule ni kufidiwa maeneo yao ambayo yamechukuliwa na makampuni makubwa. Ndivyo ilivyo Nyamongo na ndivyo ilivyo kwa rafiki yangu Mheshimiwa Lembeli, fidia bado ni tatizo. Pale kwangu Mererani ndio kabisa, leo rafiki yangu Naibu Waziri, aliposema kwamba maeneo yale yaliyogunduliwa na wachimbaji wadogo hayajatolewa kwa makampuni makubwa, nilitaka kumwambia madini ya *Tanzanite* yamegunduliwa na wachimbaji wadogo, lakini leo tunayo *Tanzanite One* ya Afrika ya Kusini na tunayo makampuni mengine makubwa yapo pale. Kwa hiyo, nilitaka nimwambie yale tuliyagundua sisi ili tu nimuwekee kumbukumbu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, nataka kuungana na pendekezo la Mzee William Shellukindo la kushauri kwamba, tuunde kamati kupitia baadhi ya maeneo ambayo Tume ya Rais haikuweza kuyaweka bayana, ikiwemo lile ambalo Mzee wetu Mkono alilipendekeza. Napendekeza tuchunguze hayo ili tuweze kujiridhisha pia.

Baada ya kusema hayo, sitaki nipigiwe kengele na hasa kwa sababu mambo yangu ni makubwa na mengi. Nataka tu niungane na Kamati kwa kutoa hoja kwamba, madhali Wabunge wote waliosimama wameunga mkono Ripoti hii iliyosomwa na Mheshimiwa Shellukindo, basi ingekuwa ni vizuri baada ya kuboreshwa kwa maoni ya Wabunge, Taarifa hiyo iwekwe kama ni sehemu ya azimio letu katika kumshauri Rais juu

ya Ripoti hii ambayo ingeweza kuwa *package* yetu Waheshimiwa Wabunge. Hapo baadaye nitaomba mwongozo wako ili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. MWERA C. NYANGURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi kwa mara ya kwanza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu kuchangia hii hoja. Pili, nachukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Tarime, kwa kuwa na imani nami na Chama changu cha CHADEMA na kuniwezesha kufika hapa. Nipende kuwahakikishia kwamba, sitawaangusha wananchi wangu wa Tarime, nitafanya uwakilishi wa kutosha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenye hoja ya msingi kwa kumpongeza Rais wetu kwa kuunda hiyo Kamati, pamoja na wanakamati wote walioshughulikia suala hili la madini. Nikianzia kwenye mambo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu hasa katika maeneo yetu haya ya Nyamongo, tumekuwa tukiwaweka hawa wawekezaji wakija; lakini je, hawa watu ambao wanakuwepo pale hawana maeneo yao ya kuchimba; ndio tumesema kwamba wachimbaji wadogo wapo; watu hao maeneo yao yapo?

Kwa hiyo, kuna suala la kuangalia pamoja na kwamba, kuna baadhi ya sehemu ambazo maeneo yapo, lakini mwananchi aliyepo katika maeneo yale, anatakiwa ashirikishwe kuhakikisha kwamba maeneo yale kabla hatujaingia katika mikataba, mwananchi mlengwa hasa mwananchi tujue anafaidikaje katika madini haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye suala la ushuru ambao Halmashauri tumekuwa tukipata, tuchukulie kama Halmashauri ya Tarime, Geita, Kahama kwa mfano, sasa tunasema tunapata kodi ya dola 200,000; ingelikuwa tunajiuliza je uzalishaji wa Nyamongo na uzalishaji wa Geita unalingana? Wakati umefika sasa wa kuhakikisha kwamba, Serikali za Mitaa ambazo zina mamlaka kamili, zihakikishwe kwamba zinahusishwa kabla *Central Government* haijaweka hii mikataba, kuhakikisha kwamba Halmashauri nazo zinakuwa zinapata *0.3* kutoka *percentage* ngapi? Ukimwuliza Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kwamba *production* ya Nyamongo ni ngapi, hana habari kama hiyo! Sasa tunakuwa tunashindwa kufahamu kwamba, *0.3 from what percentage?* Huwezi ukafahamu kitu kama hicho.

Kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba, Halmashauri zihakikishe kwamba, zinapewa na wanapokuwa wanatoa huu ushuru, utolewe kwa wakati ambao unaingiliana ndani ya bajeti. Haya makampuni wakati mwingine yanatoa hizi dola 200,000 wakati bajeti imeshaingizwa katika mpango wa maendeleo ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kuhusu suala la mazingira, kwa kweli kuna upande wa madini, kuna maji fulani yanakuwa yanawekwa pale *drainage* inaenda

kwenye Mto Mara. Si kwamba ni watu wa Mto Mara wanaokuwa wanaumia, watu wengi wamekuwa wakiumia. Sasa niiombe Kamati hii ya Madini, ifanye ziara kwa ajili ya kuitembelea hii miradi na kuona mazingira yanavyokuwa yanafanyika katika hii migodi. Kwa mfano, ukichukulia kama Halmashauri, zimekuwa zikiomba nafasi ya kutaka kutembelea hata hiyo miradi kuhakikisha ni nini kinafanyika pale, lakini hiyo migodi kutoa nafasi hiyo inakuwa ni kazi ngumu.

Sasa imefika wakati ambapo Kamati hii ya Madini ya Bunge, niiombe pengine ije iitembelee hiyo migodi, iangalie mazingira yanavyokuwa yanaharibika kwenye maeneo kama hayo. Kuna watu wameumia, kuna kemikali ambazo ni kali sana katika maeneo hayo ambayo ukiangalia, wananchi wameumia na imekuwa ikihatarisha maisha na mazingira ya wananchi. Tukiangalia mambo ya ulipaji wa fidia, Serikali isaidie katika kuhakikisha kwamba, fidia ile inakuwa ni *valid.* Mtu ana eneo kubwa lakini kadiri alivyokadiriwa ni pesa kidogo sana, ambayo haiwezi ikamsaidia kwa kitu chochote na ardhi imekuwa ni ndogo sana.

Sasa utafanyaje wakati umemkadiria kwa pesa ndogo ambayo haitamsaidia. Tuwe na vitu hivi na tuwe na wanasheria ambao wanaweza kutusaidia katika kuweka mambo ya fidia au mambo haya ya mkataba. Kwa hiyo, mwananchi wa kawaida katika kijiji; mwananchi wa Nyamongo, mwananchi wa Genkuru, kwa mfano, Nyamwaga, anajua mambo haya? Kwa hiyo ni kuhakikisha kwamba, Serikali inasaidia katika kusimamia kwa sababu wananchi wapo ndani ya Serikali, ni lazima ihakikishe kwamba wanasaidiwa kuhusu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tukiongelea mambo ya fidia ni lazima ihakikishwe kwamba, fidia hiyo inawekwa. Fidia ikiwekwa basi ilipwe kwa wakati, wakati mwingine inawekwa lakini inakuwa kila wakati ni kuomba, hakuna utekelezaji ambao unafanywa. Kamati nyingi zimekuwa zikiundwa, tukifika hapa Waheshimiwa Wabunge tunaunga kwa asilimia mia moja, lakini utekelezaji *zero;* sasa ni nini kinachokuwa kinafanyika?

Mimi nitaunga mkono hoja hii nitakapoona utekelezaji unakuwa wa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba, Kamati hizi ni nyingi. Leo ni siku ya kwanza, nawashukuru sana. Nawapongeza wananchi kwa kazi kubwa mliyoifanya, kwa kunichagua kuwa mwakilishi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuchangia kuhusu Taarifa hiyo. Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuchagua Kamati hiyo iliyoandaa Taarifa hii. Vilevile tumshukuru kwamba yeye mwenyewe baada ya kuipokea Taarifa angeweza kuifanyia kazi, lakini ameona bora ailete kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge, tutoe

mawazo yetu kabla Serikali haijaanza utekelezaji. Kwa hiyo, mimi natoa pongezi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kabla sijafika mbali, nataka nianze kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Ole-Sendeka, kuhusu uchimbaji wa *Tanzanite. Tanzanite* ni madini ya wachimbaji wadogo, tunachotakiwa sisi Serikali ni kuwawezesha wale wachimbaji wadogo kuwa na zana za kuwawezesha kuchimba madini ya kutosha. Mimi nimefika kule nikaona. Mwaka 2001 niliandaa Muswada Binafsi kuhusu uchimbaji wa vito ikiwemo *Tanzanite*, Serikali wakaona Muswada ni mzuri lakini badala ya mimi kuuleta Bungeni wakasema tuachie Serikali tutaandaa Sheria itakayozingatia jambo hili, haikuletwa mpaka leo. Madhumuni yalikuwa ni kusema waziwazi mambo mawili; kwanza, madini yale yawe ya kuchimbwa na watu wadogo; pili, uwezeshaji na tatu, kuzuwia kuuza nje ya nchi *Tanzanite* ambayo haijakatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo Waziri wa Fedha alikuwa Mheshimiwa Mramba, alitoa agizo kuzuwia *Tanzanite* izisiuzwe nje ya nchi kama hazikukatwa. Leo ni *story*, wala haikutekelezwa tumerudi kulekule. Ukienda kwa mfano India, utakuta *Tanzanite* inayokatwa na kuuzwa ina thamani zaidi kuliko *Tanzanite* inayokatwa Tanzania na *Tanzanite* inauzwa nje kwa magendo. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge wa sehemu hiyo kwamba, jambo hili ni lazima tulitazame upya kabisa na tuliwekee sheria, namna ya kuhifadhi, kusaidia na kupata mapato kutokana na *Tanzanite* yao.

Vilevile sisi tunao ushahidi pia kwamba, kampuni ile ya *South Africa* inayochimba madini, wanachukua *raw Tanzanite* wanaziweka kule *South Africa* kwa kuwa wanasema baada ya miaka tisa itaisha. Kwa hiyo, itakapoisha nchi itakayokuwa inauza *Tanzanite* itakuwa ni *South Africa* na sio Tanzania. Sasa mambo kama haya kwa nini tunayaacha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kwa mfano, nimeona Mheshimiwa Waziri amerudia. Mimi ningekuwa ni yeye nisingerudia kutaja habari ya Kamati ya Kipokola wala Kamati ya Mboma, maana yake zote zilifanya kazi lakini Serikali hawakutekeleza. Kwa hiyo, kuirudia ni kama kujipalia mkaa tu, maana Taarifa ya Mboma ilikuwa ni nzuri sana na walielekeza namna ya kusaidia wachimbaji wadogo na namna ya kuondoa migogoro; mpaka leo migogoro imeendelea. Kama Taarifa ya Kipokola ingetekelezwa, Rais asingelazimika sasa kuunda Kamati nyingine, maana imebidi *reference number one* Kamati ya Bomani iwe ni Kamati ya Kipokola; sasa tunaunda Kamati juu ya Kamati. Tunapounda Kamati moja, ikifanya kazi itekelezwe kwanza ile. Niliona niyaseme hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nilikuwa nataka kutoa ushauri kwa Serikali kutokana na mapendekezo ya Kamati yenyewe. Umezuka ugonjwa na ugonjwa huo ni wa fikira unaosema tuna madini, usipopata muwekezaji mwenye hisa kubwa hamtachimba madini, huo nao ni ugonjwa ni lazima tuukatae. Nitatoa mfano mzuri wa Botswana; Botswana ni nchi ndogo lakini inakopesha hata *IMF* wanakopa hela Botswana. Walichofanya Botswana ni nini?

Wao wana almasi, wanasema sikiliza wewe muwekezaji una vitu viwili; una teknolojia lakini huna almasi, kwa hiyo, ukija tutakwenda 50/50 kwa sababu kinachofanya mradi ule uwe *viable, bankable,* sio teknolojia ni rasilimali iliyo pale ndani ya ardhi. Kwa hiyo, kinachoanza kuthaminiwa ni rasilimali yako uliyonayo sio teknolojia; teknolojia ni *input* ya rasilimali uliyonayo katika ardhi yako. Sasa hiyo sisi tunashindwa kuitafsiri, ndio maana tunasema wawekezaji waje 100/100; kwa nini wawe 100/100 wakati mali ni yetu?

Pili, *bankable project* itauzwa, wale wanakuja wakishaona Bulyanhulu kuna dhahabu watakwenda benki watakopa; kwa nini tusikope wote kwa ubia ndio tuwaajiri wale? Serikali na kampuni iliyoundwa ya pamoja itaajiri hao. Botswana ni 50/50; mkitaka njooni kama hamtaki nendeni. Madini sio *perishable product,* nani amesema madini yataoza kama hatukuelewana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja kwa nguvu kabisa kwamba, nchi hii itaendelea kuwepo, watu wataendelea kuwepo na rasilimali zitaendelea kuwepo, lakini sisi viongozi wote ni wa kupita. Hatuwezi kuendelea kuwepo siku zote, kwa hiyo ni lazima tufanye mambo ambayo na kesho yatasaidia watu wengine kuendelea. Tusifanye kwa namna tunavyoona siku hii. Nataka niseme; uwoga huu ni wa nini? Tumefanya wawekezaji kama Mungu wa Duniani kwa rasilimali ya nchi zetu, haiwezekani. Nataka niliseme hilo kwamba, kuanzia sasa tuache uwoga tuingie ubia 50/50 kwenye madini. Wala sio jambo la kusema kwa unyonge; unakuwaje mnyonge na wewe ndio tajiri?

La pili, mimi naipongeza Serikali kwa kuamua *STAMICO* na *NDC* ziwepo na mimi ni Mwenyekiti kule *NDC,* nitasema kidogo jambo nililoliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naishauri Serikali, madini mama yamilikiwe na serikali yenyewe, nayo ni chuma na mkaa. Huwezi kumilikisha chuma kwa mtu binafsi. Unampaje mtu amiliki chuma; lazima yawe ni mali ya serikali yenyewe. Sisi tuna uwoga wa kusema, unajua *investor* akija ndio atawekeza kwa kuleta *drilling;* mimi nasema hivyo vitu wamevitoa wapi? *STAMICO* tuiwezeshe kuwa moja ya *drilling company* ya Watanzania.

Sisi tumefanya majaribio kidogo tu, Mheshimiwa Waziri wa Madini naomba nikushukuru sana na Kamishina wako; hawa Waheshimiwa hapa Dodoma wana wataalam wa kupindukia kwa mambo ya madini, hawana vifaa tu vinavyotakiwa ambavyo havizidi hata dola laki nne. Tungewapatia hawa vijana vifaa vya dola laki nne, nchi yote hii tungejua *deposit* yote ya madini tuliyonayo. Nitatoa ushahidi; sisi tumekwenda kuonana na Mheshimiwa Waziri akiongozwa na Prof. Mruma, tuliomba vijana kumi na mbili wamekwenda Liganga, hii Liganga mnayoisikia sijui tuna tani 1000, tani milioni moja na laki na mbili ni wimbo tu, kuna chuma kinachoonekana juu kingine hakionekani juu.

Mimi nilikuwa nasema jamani kazi ya Serikali ya kwanza ni kujua mlichonacho ninyi wenyewe, tugharimie kujua tulichonacho sio kuita watu waje watuambie

tulichonacho. Kwa hiyo, sisi tumekwenda kule Liganga wametupa wataalam 12, miezi miwili wametuambia bwana Mwenyekiti, Waziri Mkuu na Waziri mwenyewe wana habari wanasema, inawezekana duniani Tanzania ikawa ya tatu kama si ya pili kwa kuwa na chuma baada ya Brazil. Tumewatumia hawa vijana wetu tu na vifaa vile vichache walivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema naomba Serikali tusiogope kumiliki utajiri wa nchi yetu, ndiyo tulichotumwa na Watanzania na ndicho Mungu alichotutuma hicho kwamba mali hii itumieni kwa faida yenu si kwa faida ya watu wengine. Tunampendezesha nani katika mambo haya?

La mwisho, ambalo ningependa kumalizia na hili ni muhimu vilevile ni kwamba, ukienda Mwanza na kote ambako dhahabu imechimbwa na kiwango hiki tulichosomewa, hakuna alama wala picha yoyote ya kuonyesha kwamba tumepata utajiri. Utajiri hauwezi kupimwa kwa dola, tunataka tuvione vitu hivi. Mimi nimekwenda Botswana, nikakuta nyumba ya ajabu, nzuri mno inaitwa *Diamond House*, sasa *Gold House* yetu iko wapi?

Pili, kwa nini tunaendelea kuuza *raw gold;* sisi ni wa tatu duniani, South Africa wanakata dhahabu, Ghana wanakata dhahabu, sisi ni wa kuuza pamba *raw* kila kitu Tanzania ni *raw*? Sasa tuweke sheria ya kusema madini yote yatakatwa Tanzania; nani anatuzuia kusema hivyo? Nashangaa huu umekuwa ugonjwa wa kudumu, tangu uhuru mpaka leo sisi ni wagonjwa wa *raw material*; pamba *raw material*, kahawa *raw material,* kila kitu *raw material*; huu ni ugonjwa mbaya lazima tuachane nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu, kumpongeza Rais baada ya kusikia kilio cha Watanzania wengi. Tanzania tumejaliwa kuwa na madini mengi, ameunda Kamati imeleta mapendekezo hayo kwetu, amepelekewa Rais lakini bado Bunge limehitaji kuijadili. Naomba nichukue nafasi kumpongeza sana Rais wetu, kwa kukubali na sisi tuchangie ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha sasa ameanza kutekeleza maeneo ambayo hayaingiliani kisheria au kisera kwa kumtuma Naibu Waziri wake, kufika kwenye maeneo halisi kusikiliza wananchi wanasema nini na kuwaona wenyewe migodi wapo katika hali gani. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kumtuma Naibu Waziri kufika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli wawekezaji sina tatizo nao, lakini inapofika kuzingatia kwamba madini ni ya Watanzania, wao wamekuja kwenye maeneo yetu wamewekeza mali zao nyingi lakini wajaribu kuangalia unapoingia kwenye nchi ya mwenyewe unaishi vipi na wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kusema kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu, mahusiano ya wawekezaji wa madini na wananchi ni mabaya sana. Nalizungumza hilo kwa sababu hawaelewani katika maeneo yote waliyoyashika hao wawekezaji. Kweli wamewekeza mali zao nyingi, lakini inapofikia mahali basi hata mwenye eneo lile unaanza kumnyanyasa, ile kupata kwako itakuwa wananchi wanalalamika haikusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengi yapo katika ulipaji wa fidia; wananchi wanalalamikia fidia inayotolewa na wawekezaji ukizingatia kwamba na wao wanachuma dhahabu nyingi au almasi nyingi ambayo hailingani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepita kwenye maeneo mengi, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, bahati nzuri sehemu alizopita Mheshimiwa Naibu Waziri, tumekuta sahihi amefika na sisi tumefika tukajionea. Hili nalizungumza wazi kwamba, nimesikiliza kwa wananchi, nimefika kwa wenye migodi, hali ya mahusiano ni mbaya wala hawana mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo; tunapofikia mahali sasa wananchi wanahamishwa eneo hilo, mchimbaji mkubwa akifika pale tunatumia nguvu kubwa sana kuwahamisha; kwa nini tusifanye majadiliano hawa ni wananchi ambao wamekaa na dhahabu na almasi zile, wamekaa na *Tanzanite* zile kwa miaka na miaka; kwa nini tusitumie utaratibu wa kuwahamisha taratibu, nguvu tunazotumia ni kubwa mno, nyingine mpaka unawadhalilisha wananchi? Nitakupa mfano sasa hivi pale Geita Mjini, GGM wamehamisha watu, kuna ambao wapo kwenye mahema tangu 31 Julai, 2007, walitolewa kwenye maeneo wanakaa ndani ya mahema; je, huu ndiyo ustarabu?

Inafikia mahali sasa Watanzania wananyimwa haki yao ya kuhakikisha kwamba maeneo hayatolewi mpaka ilipwe fidia inayostahili ili waweze kufaidi maeneo ambayo wamewaachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fidia nyingine Buzwagi, tumepita maeneo yale malalamiko ni ya fidia. Wawekezaji bila kushauriana na maeneo yao, wanaamua kuwajengea nyumba kulingana na maeneo. Sasa tatizo kubwa zaidi ni mahusiano mabaya ambayo wameyajenga wale wawekezaji; nyumba zinaezuliwa mabati, madirisha na milango, sasa hapo utasema kwamba kuna mahusiano mazuri? Naomba Serikali ilifuatilie jambo hilo na Mheshimiwa Naibu Waziri, amefika maeneo hayo ameyaona; nafikiri Serikali sasa itajipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafikia sasa mahali pengine, mwekezaji anapofika kwenye maeneo hayo anaweka sheria zake ambazo zinamnyanyasa Mtanzania. Kwa mfano Geita, watu wa Saragurwa wamefungiwa njia yao ya kukatisha kwenda Geita, wamewekwa ya kuzunguka kwa saa tatu badala ya saa moja kufika Geita Mjini. Sasa ninapozungumzia mahusiano mabaya na wawekezaji, tuyaweke vizuri Serikali itusaidie kuwasimamia hawa watu kuhakikisha kwamba, hawapewi adhabu kubwa kiasi hicho. Wao wanataka njia ambayo itawasaidia, hawaingii kwenye migodi yao. Wananchi wa Saragurwa wanaomba sana ifunguliwe njia ya kutoka Saragurwa pale iende ikatize Mgusu ili wateremke waingie Geita Mjini. Wamechongewa njia ambayo inazunguka na

wanatumia muda mrefu kufika mjini, tukizingatia kwamba hawa watu wanataka kufika mjini kupeleka biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mazingira; naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini, pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Rais; mazingira yanayoachwa na wawekezaji wetu ni mabaya. Nitaomba sana, kwa mfano, Geita ukienda pale GGM mashimo yanayoachwa inasikitisha; linaachwa shimo ambalo hata maji hayawezi kujaa, kwa sababu huwa tunayategemea kama malambo wakati wa utengenezaji wa barabara na kunyweshea ng'ombe. Hayawezi kujaa hata kwa mvua ya kiasi gani, sasa nafikiri upungufu wa sheria zetu, pamoja na sera ambayo sasa tunaiomba Serikali ije ikiwa imejipanga vizuri, ihakikishe kwamba sasa hatuachiwi mashimo kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kusikitisha sana ni uchimbaji wa Mgodi wa Ulyanhulu. Uchimbaji ule ni wa chini, siku Mwenyezi Mungu atakapokasirika Tanzania tutajilaumu sana; hatujui huyu wa leseni ataishia wapi na uchimbaji wake kule ndani kwa ndani? Naomba hilo mlizingatie sana. Kuhusu masuala ya mazingira tuliangalie, siku Mwenyezi Mungu akikasirika tu juu ya uchimbaji huo, yatakayotokea sijui tutaelezana nini yatakapotokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nishauri mambo yafuatayo; niungane kuhakikisha kwamba sheria na sera zinazingatia mazingira na malipo ya fidia kwa wananchi wetu wanaowaachia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, unakuta kwa mfano Kijiji cha Mgusu kina hati ya kuwa kijiji pale, lakini bado kijiji hicho kinakuwa ndani ya mchimbaji mtafiti wa madini; hebu niambie hawa watu unawaweka katika hali gain? Naomba sheria zitakazotungwa na sera itakayotungwa, iangale wazi wanakijiji wasiwekwe katika hali ya kuwa na wasiwasi wa kuishi maeneo ambayo walishajipanga pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana suala la wale watu wanaoishi katika mahema wanaoitwa mini mpya, Naibu Waziri ameongea nao na sisi tumeongea nao, naiomba sana Serikali yetu suala hili lifanyiwe kazi haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Serikali isimamie fidia kwani wananchi wengi hawatendewi haki. Mwekezaji anafika anaongea na mmoja mmoja hatimaye wengine wanadhulumiwa hawapati haki inayostahili. Lingine naomba nishauri Kwamba, hakuna elimu ya kutosha ambayo wananchi wetu wanayo; Serikali ijipange vizuri kuhakikisha kwamba, elimu inaelimisha wajibu na majukumu ya mwananchi na haki ya mwekezaji kwa eneo analokwenda. Kwa hiyo, kama elimu hii itafikishwa kwa walengwa, nafikiri migongano hii ya wawekezaji pamoja na wananchi itaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa tujipange vizuri, huu Mgodi wa Mwadui mimi nasikitika sana; umeanza siku nyingi sana lakini wao kila siku wanasema ni hasara; kama ingekuwa ni hasara wangeshaondoka! Nakuomba sana Mheshimiwa

Waziri, hili la kutuambia kila siku ni hasara *Mwadui Diamond Limited* sasa ulichukue na bahati nzuri tumeanza kuwa na mwekezaji mwingine Mtanzania mwenzetu, El-Hirary, ambaye ataleta chachu kubwa zaidi, tuone thamani ya almasi yetu ikoje. Naomba sana suala la kuambiwa kila siku ni hasara nalo liishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba sana Serikali isimamie utoaji wa leseni, isifikie sasa kila siku tunasema leseni wapewe watu wa nje tu, naomba leseni za wawekezaji kutoka nje zisimame sasa, tujali Watanzania ambao wapo tayari kuwekeza kwenye masuala ya madini; hasa ukizingatia kwamba kuna wawekezaji kama akina El-Hirary, ambaye yupo pale karibu na Mwadui, kuna God Ainga yupo Nyalugusu na wachimbaji wadogo wadogo wengi tu wana nafasi hiyo ya kuhitaji kuchimba madini. Serikali iwasaidie sasa wachimbaji wadogo wadogo kuhakikisha kwamba, wanawatafutia nyezo za kisasa za kuhakikisha wanafukuzana na hao wachimbaji wakubwa wenyewe wanajidai na mitambo.

Hawa wachimbaji wadogo wadogo tunawaambia uwezo wa nyezo ni duni. Siku moja wakati tupo kwenye Kamati yetu, Mheshimiwa Eng. Manyanya alisema kwamba, pale Chuo Kikuu kuna mashine nzuri sana ambazo zinaweza kuwasaidia wachimbaji wadogo. Naiomba Wizara ya Nishati na Madini, ijaribu kwenda pale Chuo Kikuu ili wawaelekeze waende kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo wakaongee nao. Kama Serikali haiwezi kuwakopesha basi wao waende moja kwa moja, kuna wachimbaji wengine wadogo wadogo wana uwezo kabisa wa kununua hizo zana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa na mimi nisaidiwe, katika taarifa zote tunazozingumzia hapa; tunazungumzia almasi, dhahabu, *Tanzanite* lakini kuna madini fulani yapo Ulanga yanaitwa rubi; sijui rubi iko kwenye kiwango cha madini? Wakati Waziri akiwa anaendelea kutuelimisha zaidi kuhusu masuala ya madini, basi tuhakikishe kwamba Serikali inasimamia masuala ya fidia kwa wananchi wetu, kwa sababu hawajui sheria. Wakifika pale wakiambiwa mti mmoja shilingi mia moja wao wanakubali tu, baadaye wakishapata elimu ndiyo wanaanza kulalamika kwamba, kwa nini walipelewa laki moja. Kama Serikali itawasimamia na hasa mwekezaji awe karibu sana na Halmashauri ya Wilaya kwa maeneo hayo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja zote za Tume. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuipongeza Kamati hii iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, kwa kufanya kazi yake vizuri sana na leo tunaijadili kwa kutoa mchango wetu katika Bunge lako Tukufu. Mimi nimeshawishika kuchangia ili nitoe ushauri katika Taarifa hii kwa kuwa ni mdau. Jimboni kwetu tuna makampuni makubwa matatu yanayofanya utafiti wa *uranium,* kwa hiyo, nimeshawishika sana. Kwa sababu hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake leo, ukurasa wa tano

*paragraph* ya kwanza mstari wa pili kutoka mwisho ambao ulisema mchango wa Sekta ya Madini katika uchumi wa Taifa utaonekana endapo uwekezaji na uzalishaji wa madini utaongezeka.

Kwa hiyo, sisi kule haya makampuni yapo katika hatua nzuri ya utafiti na taarifa tu za mwanzo za kiolojia zinaonyesha kuna *deposit* ya kutosha ya *uranium* lakini kilichopo ni kwamba katika sheria na sera za sasa hivi hakuna kinacho-*govern* madini haya ya *uranium*. Hivyo, ushauri wangu kwa Serikali naiomba iharakishe mawasiliano ya mchakato huu wa kuandaa sera na sheria itakayoweza ku-*govern* madini haya kwa kushirikiana na *stakeholders* ili katika sheria hii mpya, madini ya jumla na sera inayorekebishwa itakayoletwa Aprili, 2009 iweze kuingiza vipengele hivyo vitakavyoweza ku-*govern* madini hayo ya *uranium*. Kwa sababu madini haya ndiyo kwanza yataanza kuchimbwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya yanafanya utafiti lakini madini haya yana mionzi na lazima wawasiliane na *Tanzania Atomic Energy Commission (TAEC)*, ambayo ndiyo ina majukumu na mamlaka kuhusiana na masuala ya mionzi. *Commission* hii ipo chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, lakini uchimbaji wa madini upo chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Sasa kulingana na mahitaji ya hivi sasa, tulikuwa tunaiomba Serikali ikae ione kwamba sera na sheria zitakazotungwa hazikinzani, kwa maana maamuzi yatakayotolewa yawe yenye mwono wa kuharakisha yatakayotolewa, vilevile yawe yenye mwono wa kuharakisha madini haya yaweze kufikia kuzalishwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, tuna *deposit* ya *uranium* na tutafikia katika mgodi. Wawekezaji wanafanya kazi zao na sisi tulitekeleze jukumu letu kwa umakini ili fursa hii ya kuongeza aina ya madini katika soko la dunia, tuitumie vizuri kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *uranium* ina umuhimu sana katika nishati umeme duniani; kwanza ni rahisi ku-*mine* lakini pia uzalishaji wake, inatoa kiasi kidogo sana cha *sold waste* ambayo inatakiwa itunzwe kwa umakini sana. *Tanzania Atomic Energy Commission* inapaswa iwe karibu sana katika utafiti huu na pia wakati wa uzalishaji. Kwa hiyo, tunaomba katika sheria hiyo lazima viwepo vipengele vya kuonyesha jinsi gani ya kutunza mazingira ya uzalishaji wa *uranium* hiyo na watakavyoweza kutunza *the waste* zitakazoweza kuwa zinapatikana. Kwa hali ya dunia ilivyo hivi sasa ya kupambana na athari ya mazingira duniani inayotokana na *carbon*, *uranium* ina nafasi kubwa sana na ina soko kubwa sana kwa wale wanaoituma katika kuzalisha umeme duniani. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali tusiicheleweshe wala tusizembee, madini yatatupatia na kutuongezea pato kubwa sana katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujaribu kuelezea tofauti ya *uranium* na makaa ya mawe na kwa nini dunia inahitaji *uranium*?

Tani 25 za *uranium,* ile *actual fuel* ya *uranium* ina uwezo wa kutengeneza umeme wa mega watt 1,000 kwa mwaka, lakini makaa ya mawe ni tani milioni tatu na laki mbili

ndiyo yanayoweza kutengeneza umeme na kuwa *mega watt* 1,000 kwa mwaka. *Carbon dioxide* inayotoka kwenye makaa ya mawe, kwenye tafiti wanasema ni tani milioni saba za *carbon dioxide* zinazotoka na kusambaa duniani. Kwa hiyo, *uranium* ina nafasi kubwa sana duniani, tunaiomba Serikali itazame kwa jicho la karibu ili tuweze kupata faida kubwa kutokana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, sisi Namtumbo tunaitegemea migodi hii. Kwanza naomba niungane na Kamati ya Nishati na Madini katika kifungu cha nne, kipengele kidogo cha 1.4 ambacho kinasema tozo za Halmashauri zifanane na tozo zilizopo katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, ambayo inayataka makampuni ya madini kulipa kwenye Halmashauri husika, kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo yote. Hii naungana nayo kwa sababu na wao wameunga mkono Kamati ile ya Tume ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusiana na Madini. Naomba sana katika Mikataba ya *MDAs* na sisi Namtumbo mtufikirie kwamba, lazima mikataba hiyo pia iingizwe kipengele hicho ambacho kimetolewa ushauri, tuweze kupata na sisi faida katika hili.

Vilevile naunga mkono kipengele cha 4.12 kinachosema mikataba yote itakayoingiwa iwe wazi kwa wananchi na ipatikane katika Ofisi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri ambapo migodi hiyo ipo. Kwa hiyo, naungana na Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru. Mchango wangu ulikuwa huo; ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuwa miongoni mwa wale watakaochangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ningependa nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara zake za kuamua hii Taarifa ya Kamati ambayo aliichagua yeye kwa ajili ya kuishauri Serikali kuhusu Sekta ya Madini kwamba ipitie hapa Bungeni ili Wabunge waweze kuijadili. Hili ni jambo muhimu, kwa sababu kama unavyoona ni kwamba, upo upungufu ndani ya Kamati hii. Wao kama binadamu na sisi kwa wingi wetu kama Wabunge, mambo machache tutayaongeza ili kuboresha ushauri wa Kamati hii kuhusu Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuipongeza sana hii Kamati ya Rais, ambayo ipo chini ya Jaji Bomani, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Hasa hasa ningependa kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, iliyokuwa chini ya ndugu yetu, Mheshimiwa Shellukindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo machache tu ya kuchangia katika kuokoa muda na hasa ukizingatia kwamba, mambo mengi yameshazungumzwa na wenzangu wengi waliopita. Mimi ningeanza kwa kusema kwamba, ningeiomba sana Serikali iweke wazi; namna gani itakavyoweza kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo wadogo. Najua

kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, limeelezwa jambo hili lakini halikuwa bayana kwamba watawasaidiaje hawa wachimbaji wadogo wadogo.

Hapa nilikuwa nashauri kwamba, jambo la msingi la wachimbaji wadogo wadogo ni kuwasaidia kuwawezesha kupata vifaa vya kuchimbia, kwa sababu kama unavyofahamu; hawa wachimbaji wadogo wadogo kwanza wanahatarisha maisha yao hasa hawa wachimbaji wa dhahabu, utakuta baada ya kuchimba wanachagua madini haya kwa kutumia *mercury* ambayo ni mbaya. *Mecury* ikiingia kwenye ngozi, inapita kwenye damu inakwenda mpaka kwenye figo na baadaye watapata magonjwa ya figo na pengine baadaye wengine watapata hata kansa. Wanafanya hivyo kwa sababu ya kutokujua. Hata kama wangejua, hawana njia nyingine yoyote ya kuwasaidia kuchagua ni lazima watumie *mercury*. Hivyo, kama Serikali ingewapatia vifaa vya kuchimbia kwa mfano *compressor, excavator,* pamoja na *shaking table* ambayo ni mashine maalum inayochuja dhahabu pamoja na mchanga. Kwa hiyo, kama ikipatikana *shaking table*, maana yake wasingeweza kutumia *mercury* ambayo inawahatarisha. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwa makusudi kabisa, ifanye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali kwa makusudi kabisa, ianzishe soko la kununua madini ili kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata mahali pa kuuza madini yao. Pamoja na kuuza, iwasaidie pia katika kujikwamua kiuchumi. Katika kufanya hivyo, Serikali yenyewe pia inapata ushuru au kodi ambayo ingeweza kuongeza pato la taifa letu. Kwa hiyo, hii kuacha kutokuwa na soko maalum hawa wachimbaji wadogo wadogo hawajui madini yao wanayauza wapi na badala yake pengine wajanja wachache wanaweza kuwadanganya na kununua kwa fedha kidogo na wao wenyewe kuweza kujinufaisha kwa kupata fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nimeona pia katika uangalizi wangu kwamba, upo mtindo wa wachimbaji wakubwa kupeleka sampuli za mchanga nchi za nje kwa sababu ya kufanya utafiti. Kinachosikitisha ni kwamba, sampuli hizi zinachukuliwa katika makontena makubwa tani kwa tani na mwaka hadi mwaka. Sasa mimi najiuliza; hivi hizi maabara zinazopima hizi sampuli kiasi hicho zina ukubwa gain; kwa nini kwanza mchanga upimwe kwa miaka nenda miaka rudi? Majibu hayapatikani, badala yake wao wanazidi kuchimba. Mimi ninavyoona huu ni ujanja wa wachimbaji wakubwa kuiba madini yetu na wasiyalipie kodi. Kwa hiyo, ningeomba hapa kwamba, Serikali kwa makusudi iwe macho katika kuangalia suala hili kwa sababu hapa tunaibiwa kwa kiini macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siyo kuibiwa basi inaonekana kuna njama za makusudi, kati ya wachimbaji labda na taasisi husika. Jambo lingine ni kwamba, wapo wajanja wachache huchukua maeneo makubwa sana ambayo wengine hata hawawezi kuyachimba, wanayahodhi tu. Kwa kufanya hivyo, wanawanyima haki hawa wachimbaji wadogo wadogo kupata mahali pa kuchimba ili waweze kuboresha maisha yao. Matokeo yake jambo kama hili linachochea chuki kati wananchi na Serikali yao. Serikali ina dhamira nzuri tu ya kuwasaidia wananchi, lakini hawa watu ambao wanahodhi maeneo

na kuzuia wachimbaji wadogo wadogo wasichimbe, wanazidi kuleta chuki kati ya wananchi na Serikali.

Kwa hiyo, ninaishauri Wizara husika kwamba, ikiwezekana wale wote waliochukua maeneo makubwa ambayo hawayafanyii kazi kwa wakati huu, Serikali iyarudishe ili iwagawie wachimbaji wadogo wadogo au iwape wengine ambao wanachimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naona kwamba tabia hiyo siyo nzuri ni kuwanyima haki hawa wachimbaji wetu wadogo wadogo. Ukiangalia sana hawa wachimbaji wadogo ndio wao ambao mara kwa mara wanagundua sehemu zilizokuwa na madini na badala yake wachimbaji wakubwa nao wanakuja kuvamia na wale wanawaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa nataka nichangie kidogo katika suala hili ambalo wenzangu nao wamelichangia. Baada ya kusema hayo, kama nilivyokwambia kwamba nitatoa mchango wangu mdogo sana ili kuokoa muda na kwa kujua kwamba wenzangu wameshachangia sehemu kubwa ya yote waliyokuwa wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini awali ya yote nachukua nafasi hii kuipongeza Taarifa ya Kamati ya Rais ya Madini, ambayo kwa hakika ukiondoa kasoro ndogo ndogo ambazo zipo na ambazo tunajaribu na sisi kuweka mchango wetu, Taarifa ile ni nzuri na imefanywa kwa ustadi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa siku moja kwamba, mtaji wa Mtanzania ni Utanzania wake. Ukiwa Mtanzania tu wewe ni mtaji na Tanzania siyo nchi maskini kwa sababu ina rasilimali na moja ya rasilimali hizo ni madini ambayo leo hii Mtanzania huyu anaambulia asilimia tatu tu ya mapato ya madini yote. Kwa maneno tu ambayo mengine hata tafsiri yake pengine hata wananchi hawaelewi vizuri mara mrabaha, sijui *dividend*, sijui nini lakini lugha hizi zote maana yake haileti mantiki kwa sababu bado maisha ya Mtanzania huyu ambaye rasilimali yake inaondoka hanufaiki kwa chochote. Ukilingaisha kiasi cha mali yetu hii ya madini inavyochukuliwa na makampuni haya makubwa ambayo tumeingia nayo mkataba, kwa kweli inauma na pengine si rahisi kuziba maumivu haya. Haishangazi leo sisi tunasema kwamba mababu zetu zamani zile walileletewa shanga wao wakatoa almasi, lakini na sisi hatutofautini na wao; leo hii tupo katika karne ya 21; tunachofanyiwa hapa ni kwamba tumeletewa shanga sisi tunatoa almasi. (*Makofi*)

Hali ilivyo kwa sasa ni kwamba, mfumo mzima wa Sera yenyewe ya Madini, pamoja na sheria zote, zinapaswa kufanyiwa marekebisho tena makubwa, vinginevyo hatuwezi kwenda. Mimi katika Ripoti ile nilijikita zaidi kwenye manung'uniko ya wananchi ambao sisi viongozi na Serikali ndio tunaowaongoza wananchi wetu. Manung'uniko yao yale ukijaribu kuya-*term* na kwa maana ya Ripoti ile ndio maana

nikapata msukumo wa kuomba nafasi ya kuchangia ili niweze kusema mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nililotaka kulizungumzia ni kuhusu fidia. Sheria yetu ya fidia kwa nchi yetu ipo *controlled* na Sheria ya Ardhi ambapo mtu binafsi ana-*control* ile *surface right;* maana kuna haki mbili kuna *surface right* na kuna *mining right. License* zake zinatofautina kwamba kama wewe una nyumba yako leo hapo juu umezaliwa hapo, babu yako amezaliwa hapo, baba yako kazaliwa hapo na leo wewe una watoto na wajukuu, *the whole family* au kijiji fulani haki yenu ninyi ni hapa juu tu huku chini hamna haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ilikuwa ina maana kwa wakati huo ambapo tulikuwa hatujaanza *industry* hii ya madini, lakini leo hii unaponikuta mimi nimezaliwa hapa unaniambia wanifidie kwa kijumba changu kibovu nilichokijenga, unanifidia kwa kunilipa mwembe kwa Sh.4,000/=, Sh. 5,000/= sijui mnazi, sijui mkorosho au shamba la pamba, hivi kweli inafikia thamani halisi ya hiki ambacho wanakuja kukichua wenzetu? Mimi hapa ninaona inauma na ndipo manung'uniko makubwa ya wananchi yalipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ningependekeza ifuatavyo kwamba; huyu mwananchi anayekutwa pale hebu na yeye atambuliwe kama ni mdau mzima wa ule mradi mzima maana unamkuta pale. Mimi sina elimu lakini Serikali yangu ina watu wenye elimu; kwa nini hawalindi haki zangu? Ingekuwa ni mali ilikuwa tunasema kwa sababu *the permanent owner of land* ni Serikali na kwa maana hiyo ni Rais, lakini tunapokuja kwenye suala la ile *public for public interest* kwamba Rais anachukua ardhi kwa maslai ya Taifa, pale Rais akiichukua ardhi na mimi nisifidiwe kitu chochote, kwa sababu inajengwa shule ambayo na mtoto wangu atasoma sawa, lakini inapokuwa tunataka kuchimba madini ambayo yana *wealth billions and billions* ya pesa halafu uniambie mimi sihusiki, hapa siyo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna haja Serikali ikasema kitu sheria ikabadilika kuelekea kwenye mtazamo huu wa manung'uniko. Ndio maana watu wetu ukiwaambia tunakufidia shilingi milioni tano, milioni kumi wanaridhika leo lakini kesho wakiona mali inavyoondoka pale inawauma wanaanza manung'uniko wakiangalia walichobakia nacho ni kidogo kinachoondoka ni kikubwa na kwa bahati mbaya Serikali yao haipo kwenye *share*. Tumeacha makampuni haya ya madini, tuna migodo hiyo Serikali ilikuwa na hisa zake kule lakini imejitoa kwenye hisa wameziuza. Kuuza *shares* hivi sisi Watanzania tumedanganywa na nani kwamba Serikali huwa haifanyi biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali zote makini Duniani zinafanya biashara. Ukienda nchi kama Dubai mpaka *taxi* zinamilikiwa na Serikali. Ukienda kwa wenzetu kwa mfano Ghana mfumo wao wa madini ni mfumo ambao wao wanamiliki *shares 50 by 50 or 40 by what.* Kama tungekuwa na *shares* mtu asingenung'unika kwa sababu anajua hata kama mimi sipati lakini Serikali inapata na hivyo mimi napata shule, mwalimu atalipwa mshahara mzuri, haya yote yasingekuwepo. Kinachowauma Watanzania ni kuona tunaibiwa na pengine wanakuwa na hasira na hata kuichukia Serikali kwa sababu

wanaona ndio inayowasababishia kuibiwa huku. *We must make a U-turn*, tumekosea ni lazima tusahihishe tugeuke kwa gharama yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali na hasa Wizara ya Nishati na Madini, Waziri na Naibu Waziri, juzi juzi hapa nikasikia kwamba kuna watu walikuwa wanataka kuuza kampuni yao, nafikiri ilikuwa ni *Barrick*, sijui *Williamson Diamonds,* lakini Serikali ikakataa. Nataka nikwambie rafiki yangu Waziri Ngeleja, huo ndio msimamo shikilia hapo hapo, waambie kama wanataka watuuzie sisi bora tununue yale makampuni kama wanashindwa kufanya kazi; hiyo ni janja tu. Fanya hivyo, endelea kuwa na msimamo huo mpaka turudishe vyote kama unavyofanya kwenye *IPTL* na mambo mengine. Tunajua unayoyafanya lakini endelea na huku kwenye madini, tumekosea lakini kukosea si dhambi sana kibaya ni kukubali kuendelea kukosea; kwenye madini tumepoteza, tumeumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule kwangu Mpwapwa pale Kibabwe yamegundulika madini ya safaya tena nzuri sana. Wanunuzi waliojaa kule ni Wa-Thailand na Wa-Sri-Lanka na wao ndio wana-*dominate market* kwenye *World Market* ya madini ya safaya. Kwa hiyo, hata safaya yetu inayotoka Winza Kibabwe yote inaonekana inatoka Sri-Lanka na Thailand. Sisi kwetu huku hakuna *control,* m-Thailand anaenda kukutana na mchimbaji mdogo ambaye alikuwa analima karanga sasa amepata jiwe la safaya wanaelewana; si anamwimbia tu anamwambia hii *caption*, hii nini, hakuna hapa katikati *control* ya Serikali, *the Government must come in.* Tusidanganywe, hivi hii imani ya kwamba Serikali haifanyi biashara tunaitoa wapi? Hapa tumedanganywa, tukae tufikiri upya. Leo ile safaya itoke Kibabwe, anakutana na mtu wa Kibabwe aliyekuwa analima karanga na mahindi ndio afanye biashara na m-Sri-Lanka ambaye alikuwa anafanya biashara hiyo kwenye *World Market*, lazima atamdhulumu tu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema ifike mahali Serikali tukubali kwamba tulikosea, Serikali yetu ilikosea na ijirekebishe turudi kwenye mstari wa kuzimiliki mali zetu kwa sababu kitu kama madini ni kweli yanakwisha. Niseme tu kwamba, bado tuna nafasi kwa sababu yapo madini ya chuma, makaa ya mawe na bado tuna maeneo mengi, tukifanya masahihisho hayo leo yanaweza yakatusaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya leseni, kuna leseni za utafiti na kuna leseni za uchimbaji. Wapo watu wajanja wakubwa kwa mfano ile Kibakwe karibu yote ina leseni za utafiti za watu; watu wanakaa kwenye vijiji wanakuja kushtuka tu wanaambiwa ninyi hapa mko chini ya leseni yangu. Lugha kama hii Mtanzania wa kawaida haielewi, anachoona tu Serikali imeruhusu nchi iuzwe; *how do we correct this*? Haiwezekani ukampa mtu *prospecting license* ya eneo kubwa halafu wachimbaji wadogo wakigundua unawaambia hii sehemu ilikuwa na leseni ya mtu. Huwezi kukuta mtu anayeitwa Matonya, Mazengo, Simbachawene au Malecela ana hiyo leseni, utakuta ni majina ya kigeni kigeni tu na wanachukua leseni kwenye *internet* hata huko Winza wala Mpwapwa hawajawahi kufika. Wanazitumia hizi leseni wanazopewa, kwa mfano, *prospecting license* wanazitumia kwa kwenda kununulia hisa kubwa kwenye masoko ya hisa huko London na sehemu nyingine. Wananunua hisa kubwa tu kwa kutumia ardhi yetu na mali yetu; sisi tunapata nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningesema kwamba, kuna haja ya kuangalia. Kule Kibakwe nimekataa nimesema mimi kwa ombi maalum kabisa kwa Mheshimiwa Waziri na ninakupongeza sana Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wako, mmekubali kwamba kule asifike mchimbaji mkubwa niachieni wale wale wadogo wadogo. Wameleta *impact* kubwa, sasa hivi Mpwapwa inajengeka, Kibakwe inajengeka hao hao wachimbaji wadogo wakubwa mimi siwahitaji. Wamesababisha masoko yanafanya kazi vizuri kule, watu wamekuwa wengi na watu wakiwa wengi biashara inaenda, hii yenyewe tu inatusaidia sisi, angekuja mchimbaji mmoja pale mkubwa isingetusaidia kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wachimbaji wadogo kama walivyosema wenzangu, madini ya vito yangeachiwa Watanzania wenyewe wayachimbe. Ifanyike hivyo hata kwa maeneo mengine kama dhahabu na kadhalika. Hii migodi mikubwa kama tunaweza kukusanya kodi hiyo ambayo tulikuwa tunakusanya kwa idadi kubwa, mimi nasema si vibaya wengine watakaosema wanataka kuuza tuwakatalie kama ulivyofanya Mheshimiwa Waziri. Serikali inunue na isijitoe kwenye *industry* kubwa kama hizi ambazo zinahitaji mitaji mikubwa kwa sababu wananchi peke yao hawataweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipenda tu niweke mchango wangu katika hili na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, napenda niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 68 ya Kanuni zetu za Bunge, Kanuni ya 68(8), wakati Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini, alipokuwa anazungumza na kuchangia Taarifa hii, ameongea kwa uchungu sana kuhusiana na suala la Buhemba na jinsi ambavyo wananchi wa jimbo lake wanavyopata tabu na hata kulalamika kwamba hakuridhika na kile ambacho Taarifa ya Kamati ya Rais ilichokuwa imeandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninapenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Rais ilikuwa na hadidu zake. Kamati ya Rais haikuwa *commission of Inquiry* ilikuwa ni Kamati na tulifanya pale ambapo tumefikia. Ndio maana katika mapendekezo pendekezo mojawapo na hapo naunganisha na hoja ambayo Mheshimiwa William Shellukindo ameitoa ya uchunguzi maalum. Pendekezo mojawapo ambalo Kamati imetoa kuhusiana na Buhemba ni uchunguzi wa kina kufanyika na uchunguzi huo unaweza ukafanywa na Bunge au Idara za Serikali, kwa sababu pale kuna fedha za Serikali ambazo zilipotea zaidi ya shilingi bilioni 158. Tumeandika kwenye ripoti ambazo Benki Kuu ilizitoa, ikawapa Wazungu ambao walikuwa ndio wabia kwenye Kamati yetu, lakini tulikuwa hatuna *mandate* ya kwenda Mauritius wala Afrika Kusini kuweza kujua zile fedha zilienda kufanya nini na ndio maana katika taarifa ile tumependekeza kwamba uchunguzi wa kina ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuhusiana na mwongozo wako, katika Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini ambayo imesomwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, wamependekeza kufanyike uchunguzi

maalum kwa maeneo machache ambayo Kamati ya Bunge inahisi kwamba Kamati ya Rais haikuweza kuyashughulikia, ikiwemo hisa za Bulyanhulu, suala la Buhemba ambalo Mheshimiwa Nimrod Mkono amelizungumza, vilevile ikiwemo Kiwira na Mwadui.

Kwa hiyo, tungependa sasa tupate mwongozo wa kiti chako kuhusiana na hoja mahsusi ambayo tayari imetolewa na Kamati ya Nishati na Madini, kwa ajili ya suala hilo kuweza kufanyiwa kazi ili kwa kweli hoja ambazo Mheshimiwa Mkono amezitoa kuhusiana na matatizo ya kule jimboni kwake, ziweza kushughulikiwa. Tatizo lile siyo la Mheshimiwa Nimrodi Mkono tu ni tatizo la Taifa, kwa sababu kuna fedha za umma ambazo zimepotea na ni lalamiko kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zitto Kabwe, nafikiri nimesikia taarifa uliyoitoa pamoja na mwongozo ambao umeuomba, lakini kwanza nadhani tungemsikiliza Mheshimiwa Waziri pengine angeweza ku-*react* kwenye maeneo hayo. Pamoja na hivyo, tunaupokea ushauri huo halafu utakuja kujulishwa baadaye, ahsante.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. HAZARA PINDI CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza kazi ya kamati. Naishauri Wizara itenge idara ya kushughulikia suala la madini peke yake ili kitengo hicho kiwe na *Public Private Partnership* na hatimaye kiweze kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

- Kuendeleza maeneo ya madini ambayo bado hayajaendelezwa kwa mfano Mchuchuma na Liganga.

- Kuendelea kugundua maeneo mengine ambayo kuna madini nchini.
- Suala la mikataba ya madini itakayoingiwa sasa ni muhimu iwasilishwe Bungeni kwa njia za kuwasilisha taarifa.

- Uhai wa mikataba isizidi miaka 25. kuwepo na review.

Baada ya maelezo yangu hayo, naunga mkono hoja nikiomba mapendekezo yashughulikiwe haraka.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu wa ushauri kimaandishi. Awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuunda Kamati ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Madini. Vile vile naipongeza kamati iliyoundwa kwa kutoa taarifa nzuri. Napenda kuongezea ushauri wangu kama ifuatavyo:-

1. Sheria ya madini iliyopo ibadilishwe ili iendane na Sera ya Madini.

2. Zipo dalili kubwa ya kwamba, madini yetu yanauzwa kimagendo na sehemu kubwa hailipiwi kodi na hivyo kusababisha upotevu wa Pato la Taifa. Nchi kama Ghana, imeweza kuongeza pato litokanalo na madini kwa kuanzisha kampuni ya kuuza madini ya vito *(Precious Metal Marketing Company - PMMC).* Napenda kuishauri Serikali ijitahidi kudhibiti upotevu wa mapato kwa njia ya magendo, kwa kuanzisha chombo kitakachosimamia soko la madini ili kodi ya madini ya vito isipotee kiholela.

Vilevile viwanda vya kufua madini haya vianzishwe ili kuzuia uuzaji wa madini ghafi ambayo thamani yake ni ndogo ikilinganishwa na yale yaliyofuliwa. Pia wananchi wengi wanaweza kupata ajira na kupunguza umasikini.

3. Mikataba ya Madini izingatie suala la kupanda bei ya madini mwaka hadi mwaka, pamoja na *inflation* kwa ujumla wake.

4. Utafutwe utaratibu utakaoweka wazi kiasi kitakachokuwa kinachimbwa kila siku. Ikiwezekana wawepo wakaguzi wa serikali kwa kila mgodi na mtandao wa kompyuta utakaounganishwa kwenye vituo vya uchimbaji wa mauzo na wizarani ili kudhibiti takwimu za madini yaliyochimbwa.

5. Kwa kuwa Bajeti ya Serikali huwa inaandaliwa kila mwaka, vilevile kiasi kinacholipwa na wawekezaji kwa halmashauri nacho kiongezeke kila mwaka. Hata hivyo, kiasi cha shilingi milioni mia mbili ni kidogo sana kwa kuanzia.

6. Wananchi wenye leseni za “PL” waelimishwe juu ya thamani ya maeneo yao ili wasiyauze kiholela kwa wawekezaji na kuachwa wakiwa maskini. Waelekezwe jinsi wanavyoweza kuingia ubia ili wawe na kipato endelevu.

7. Hifadhi ya mazingira ni ya muhimu katika maeneo yenye madini. Wakazi wa maeneo hayo wawezeshwe kupanda miti kwa wingi na kuendesha miradi mingine ya hifadhi ya mazingira. Hivyo, wawekezaji wahimizwe kuanzisha Mfuko wa Mazingira wa Jamii ili mazingira yao yawe angalau tofauti na maeneo mengine kufidia uharibifu utokanao na migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba na mimi nijumuike na wenzangu katika kutoa ushauri katika Sekta ya Nishati na Madini, baada ya ushauri wa Kamati ya Rais maarufu kama Kamati ya Bomani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu katika Sekta hii ya Madini ambayo ni kilio cha wananchi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sina budi kuzipongeza sana Kamati ya Rais, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa umakini waliouonesha katika kutoa ushauri ambao ni faida ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nami naomba niongezee ushauri mchache ambao haukujitokeza katika Kamati hizo kama ifuatavyo:-

1. Naomba Serikali iweke bayana jinsi itakavyowasaidia wachimbaji wadogo.

2. Serikali isitishe utaratibu wa kuwaruhusu baadhi ya wajanja wachache kuhodhi maeneo makubwa mno na hivyo kuwanyima fursa wachimbaji wadogo katika kujitafutia mapato hata kama watu hao (wajanja), hawachimbi au hawana uwezo wa kuchimba. Hivyo basi, kwa vile hawachimbi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo hawapati mrabaha wao. Hii sio nzuri hata kidogo.

3. Serikali isiruhusu tena makampuni ya nje kubeba mchanga kwa ajili ya vipimo na mchanga huo hubebwa malori kwa malori mwaka hadi mwaka. Hiyo ni aina ya wizi wa kutumia ujanja wa kuiibia serikali bila kulipa ushuru au kodi kulingana na mapato wanayopata. Swali; je ni *sample* gani inayopelekwa kupimwa nje ya nchi kwa wingi kiasi hicho?

4. Serikali iweke soko la madini hapa nchini ili iwe rahisi kwa wachimbaji wadogo kupata soko lakini pia Serikali kuchukua ushuru au kodi yake.

5. Wavamiaji binafsi waorodheshwe ili wajulikane na wao walipe kodi kwa Serikali *(TRA).*

6. Na kama madini yatapatikana katika shamba la mtu fulani, mtu huyo naye alipwe lakini alipwe asilimia fulani licha ya vijiji vinavyozunguka.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

1. Kabla ya uchimbaji madini ya *uranium* maandalizi tosha yafanyike na Sekta ya Sayansi na Teknolojia, Sehemu ya Utafiti ihusishwe kuanzia awali ili kuepuka athari mbaya zinazoweza kujitokeza katika uchimbaji.

2. Wachimbaji wadogo wadogo wawekewe mipango kabambe ya kuwasaidia ili wanufaike na uchimbaji huo.

3. Serikali iratibu uuzasji nje wa madini yetu ili tuelewe kinachotoka. Viwanja vya ndege vya migodini ni budi viwekewe vifaa vya kuchunguza na utaratibu wa kuangalia kinachotoka uwekwe.

4. Wawekezaji wapunguziwe misamaha ya kodi za mafuta, isifutwe.

5. Sekta ya Mawasiliano iwezeshwe ipasavyo ili iweze kuisaidia Sekta ya Madini. Taarifa zinazohitajika zipatikane *promptly and accurately*.
6. Yaliyobakia yote naungana mkono na Kamati ya Bunge na kumpongeza Rais kwa uamuzi wake wa kuunda Tume hiyo.

Madini yetu yadhitibiwe ili yachangie uchumi wetu kama Botswana na Afrika Kusini.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutamka kuwa naunga mkono Taarifa.

Napenda kutoa ushauri/mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Matatizo ya wachimbaji wadogo ndiyo chanzo kikubwa cha migogoro baina ya wawekezaji wakubwa na wananchi wanaoishi karibu na migodi. Ili kupunguza na au kumaliza tatizo hili, naishauri Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

- Wachimbaji wadogo wawezeshwe kupata leseni ya uchimbaji bila usumbufu kama ilivyo sasa. Gharama ya leseni ipo juu, wachimbaji wadogo wengi hawana uwezo wa kulipia leseni kwa muda.

- Uchimbaji katika maeneo wanayoishi wananchi hasa mashamba ya wananchi, ugawaji wa maeneo haya wagawiwe kwanza wananchi kabla ya wawekezaji wakubwa. Iwapo wawekezaji watakubaliana na wananchi kuchukua maeneo yote, wawekezaji na wananchi wawe na mkataba.

- Wachimbaji wadogo wapewe mgawo kupita mrabaha kwa lengo la kuwawezesha.

- Muda wa leseni ndogo za uchimbaji uongezwe kufikia miaka 15, miaka mitano ni muda wa kukusanya nguvu, miaka kumi ni kupata faida.

- Mfuko Maalum kwa ajili ya kupata mtaji wa ununuzi wa vitendea kazi kwa wachimbaji wadogo uanzishwe haraka. Madhumuni na matumizi ya Mfuko huu utungiwe sheria. Uchangiaji wa Mfuko huu utokane na mrabaha unaolipwa na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaliji fidia uzingatie sheria mpya ya ardhi. Sheria inasisitiza kuwa ardhi tupu bila mazao pia inalipiwa fidia. Wananchi wanaoishi maeneo yanayogunduliwa madini wasihamishwe kabla hawajapewa maeneo mapya kwa msaada wa serikali. Vilevile wajengewe makazi, shule, zahanati na wapate huduma ya maji kabla kama fidia kwa ajili ya usumbufu.

Wananchi wanaoishi karibu na migodi wawezeshwe na wawekezaji kwa njia ya utaalam/rasilimali ili waweze kushiriki katika kilimo cha kisasa cha mboga mboga, matunda, mpunga, uvuvi na ufugaji, kwa lengo la kuwauzia wenye migodi chakula

badala ya kuagiza kutoka nje. Utaratibu huu uwekwe kwenye mkataba na utungiwe sheria.

Kila kijiji kijengewe zahanati, kila kata ijengewe kituo cha afya na wilaya husika ijengewe hospitali ya kisasa, badala ya kuwapeleka kufanya kazi nje ya wilaya wanapohitaji huduma za afya. Vilevile nashauri iwepo na *package* ya mafunzo katika fani mbalimbali kwa wafanyakazi wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *STAMICO* itambuliwe kama chombo pekee chenye utaalamu na wataalamu wa kusimamia, kudhibiti, kuendeleza na kuratibu Sekta ya Madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahante.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hatua mbalimbali alizozichukua ili kuboresha Mikataba ya Sekta hii ya Madini.

Pili, nawapongeza kwa dhati; Waziri na Naibu wake, kwa kuendeleza juhudi hizo.

Naipongeza Kamati ya Mheshimiwa Bomani. Tulitembelea maeneo ya migodi mbalimbali hivi karibuni, kuanzia tarehe 18 – 25 Oktoba, 2008. Ufuatao ni mchango wangu katika kuboresha:-

1. Sheria zilizopo ni kandamizi na hasa kwa wachimbaji wadogo, kwani wao wamekuwa ni watu wa kuondolewa.

2. Utoaji wa leseni hauzingatii hali halisi ya mazingira yanayoendelea kama vile uchimbaji uliokuwepo mfano kesi ya Mgusu ya utapeli wa Ndugu Chipeke na wachimbaji wenzake. Ni vyema suala hili lipewe ufumbuzi, ikiwezekana aliyenunua kiutapeli kwa Chipeke aonyeshwe sehemu nyingine, kwani inaonekana hata afisa madini hakuwa na taarifa za kutosha juu ya maeneo husika kabla ya kutoa leseni kwa Chipeke. Tatizo ni kubwa sana.

3. Wachimbaji wadogo wapatiwe maeneo yao ili waweze kuendeleza shughuli za uchimbaji, kwani ndio njia pekee waliyokuwa wakijipatia kipato la sivyo ni kuwakosesha haki nchini mwao.

4. Fidia inayolipwa haizingatii hali halisi na juhudi zifanyike mara moja kumaliza tatizo la watu waliohamishwa na kuwekwa kwenye maturubai maili sita; ni fedheha kubwa.

5. Utaratibu wa kutoa leseni bila kujali wakazi (leseni ya utafiti), uangaliwe upya, kwani mtu anaweza kufanya utafiti hata chumbani kwa mtu kwa vile yeye ana leseni. Hii

imeleta kiburi kwa wenye leseni kutoa *notice* kwa wanakijiji kuwa wasifanye maendeleo yoyote ya eneo wanaloishi wakati si eneo lao la machimbo. Mfano hai ni *notice* ya GGM waliyowapa watu saba kijiji cha …(jina ninalo).

6. Ifuatiliwe kuhusu madai ya fidia ya watu 71 wa Kijiji cha Nyakabele toka GGM kwa kupisha kiwanja cha ndege.

7. Barabara waliyotengeneza kuzuia watu wa Saragurwa ni kero kubwa kiasi cha watu kupoteza maisha kwa ajili ya msitu na akina mama wakati wa kujifungua kutokana na umbali wa km 35 badala ya km 15 za awali. Kamati ilijadiliana na GGM kufuatia pendekezo la wanakijiji kuwa kuna njia fupi ya kuunganisha kijiji hicho na Mgusu, kiasi cha km 4/5 tu. GGM waliahidi kuangalia ili kutekeleza kutengeneza barabara kama ilivyopendekezwa.

8. Michango ya wawekezaji ipitie Halmashauri husika ili iweze kujulikana na vijiji vya migodi vipewe kipaumbele.

9. Wawekezaji Watanzania pia wapewe fursa ya nafuu ya kodi au vivutio kama ilivyo kwa wageni.

10. Wachimbaji wadogo wasaidiwe vifaa vya kazi kama dhamira ya serikali.

11. Kampuni moja kununua makampuni wenzake kwa biashara moja ni kuua ushindani na ni kinyume na dhana ya ushindani - *fair competition.*

12. *STAMICO* iwezeshwe kusaidia wachimbaji wadogo.

14. Uwekezaji uliofanywa na Barrick ni mzuri na wa kutia moyo japo sina uhakika na mapato ambayo nchi inapata kutoka kwao.

15. Ni vyema Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kitengo cha *COET* wahusishwe katika kusaidia wachimbaji wadogo kwani wana mitambo mingi ambayo ingesaidia lakini imeonekana hakuna mawasiliano kati yao na hao wachimbaji wadogo na pia kuhusu *technology transfer* na wataalam.

16. Sheria ya Ardhi ni kikwazo kwa fidia, nayo iangaliwe upya.

17. Mengine tutachangia kadiri itakavyowezekana wakati wa kuangalia sera na sheria zenyewe na ziletwe mapema.

18. Buzwagi wamalize kulipa fidia zinazodaiwa.

Kiujumla, malalamiko mengi yamechangiwa pia na upungufu wa mahusiano na mawasiliano kati ya wananchi na wawekezaji. Ni vyema mahusiano hayo yaboreshwe ili kuepusha migogoro.

Vilevile taratibu wakati wa kutwaa ardhi kupisha uwekezaji sio nzuri na ndizo zimesababisha migogoro. Tuwe na huruma kwa wenzetu, hali sio nzuri Jimbo la Geita kwa Mzee Mabina kuna kasheshe.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Rais, kwa mapendekezo mazuri waliyoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kujenga mazingira bora na imara ya kiuchumi, hatuna budi kubadilisha mwelekeo wa kufanya biashara. Pamoja na serikali kusema kwamba haifanyi biashara, nafikiri sasa ni wakati muafaka Serikali kuangalia ni aina gani ya biashara inaweza kujihusisha kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tumeona nchi zilizoendelea kama Marekani na *United Britain*, serikali zao zilikuwa hazifanyi biashara lakini hivi majuzi tu Uingereza imetumia fedha wanazokusanya kodi na kuziweka kwenye benki zao kama Lloyds Bank & Co. ili kukuza uchumi wao. Hivyo basi, biashara ya madini Tanzania ni lazima Serikali iwe na asilimia kubwa ili kukuza uchumi wetu.

Nakubaliana na mapendekezo ya Tume ya Rais ya kwamba, wawekezaji wakija wapewe masharti ya uchimbaji wa madini hapa nchini. Kwa mfano, kuchambua na kusafisha madini ifanyike hapa hapa nchini badala ya kupeleka mchanga huo kuuchambulia nje. Wawekezaji hawa wanabeba mchanga hatujui ni aina ngapi au kiasi gani walichokipata kutoka kwenye migodi hiyo. Yote haya yakifanyikia hapa; kwanza tutakuza ajira zetu na itatoa fursa ya kujenga viwanda hapa hapa nchini.

Serikali ikihusika kikamilifu, itaweza kumonita hawa wawekezaji wamechimba kiasi gani ili waweze kulipa kodi inayostahili badala ya wao kuchimba na kutuachia mashimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuangalia upya mapendekezo ya kwamba, wawekezaji wawe na mtaji wa kutosha na usiwe chini ya dola milioni 600. Mikataba hiyo iwe wazi kwa wananchi ili waelewe mapato yanayopatikana na mikataba hiyo. Mikataba hiyo isiwe ya muda mrefu ili mwekezaji asipotimiza masharti tuweze kusitisha mikataba. Vilevile naungana na Tume ya Rais, madini ya vito yote yamilikiwe na Watanzania.

Wachimbaji wadogo wadogo kwa mfano waliopo Mererani, wananyanyaswa sana na wachimbaji wakubwa. Wale wanaoitwa nyoka wameteseka vya kutosha. Ili watu hawa wafaidike, nakubaliana na Ripoti ya Kamati wasisaini mkataba mpya wala kurudia mpaka Sheria ya Madini ibadilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya makampuni hulipa 200,000 USD kwa ajili ya mafuta kwa mwaka na kuyafutia baadhi ya makampuni ushuru. Hii inatufanya tukose mapato mengi sana. Naungana na Kamati ya Rais, msamaha huu uondolewe kwa sababu makampuni haya yanapata fedha nyingi na faida kubwa sana. Kila kukicha dhahabu,

almasi, *Tanzanite* zinapanda bei; hivyo, wanaweza kulipa kodi hizi ili tuweze kutengeneza barabara zetu.

**MHE. HARITH B. MWAPACHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuiwasilisha rasmi Taarifa hii Bungeni. Aidha, nampongeza kwa kuwasilisha hoja yake vizuri na kwa ufasaha. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteua Kamati nzito iliyoongozwa na Jaji Bomani. Wajumbe wake wakiwa mahiri kutoka fani/nyanja mbalimbali ambao pia wamefanya kazi zao kwa uwazi kulingana Hadidu za Rejea zenye umuhimu wa pekee zenye lengo la kuleta maendeleo ya nchi zetu.

Kamati ya Bomani imefanya kazi nzuri sana katika kubainisha upungufu na mafanikio ya Sekta ya Madini ikilenga katika maeneo kuhusu Sera, Sheria ya Madini, mikataba, mikataba kuwa juu ya sheria, mapato, kero kwa wananchi katika maeneo ya migodi, kutopatikana kwa taarifa kutoka migodini, mazingira, uendeshaji wa makampuni, hali ya mazingira. Kamati imetoa mapendekezo ya kimapinduzi – *radical reform.*

Aidha, ninaipongeza Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri iliyofanya ya uchambuzi na mapendekezo yaliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, katika Awamu ya Tatu, makosa na upungufu ulijitokeza katika kuiendeleza Sekta hii ya Madini. Hayo yalitokana na shauku ya Serikali kuiendeleza sekta hii kwa haraka. Pili, hatukuwa na utaalam wa kutosha katika maeneo yanayohusu Sera ya Madini, Sheria zake na Mikataba stahili. Serikali wakati ule ilikuwa nzuri tu.

Aidha, Serikali haikushauriwa vizuri na Benki ya Dunia kuhusu masuala haya na hata *Development Partners* kumbe waliegemea sana upande wa wawekezaji. Kwa upande mwingine, bei ya madini hasa dhahabu ilikuwa chini sana na *operational costs* zilikuwa juu na hivyo njia/sababu ya kuwa na *consensus* zile ilikuwa kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka michache hiyo iliyopita, Sekta ya Madini imeibuka kuwa muhimu, imetuzindua. Tumeliwa lakini sasa tutawala mpaka kiama. Karibu nusu ya *exports* zetu leo hii ni ya mauzo ya madini na Tanzania inashikilia nafasi ya tatu Afrika katika uzalishaji wa dhahabu. Hayo yote ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, Ripoti ya Bomani ni *Radical and Positive* na uchambuzi wa Kamati ya Bunge imeongezea na kurutubisha mapendekezo ya Kamati ya Rais, sina nia kurejea kuyazungumzia masuala hayo tena. Kwa kifupi ni kiwango kidogo cha kodi, ukwepaji kodi na mapato yasiyoridhisha, *Legal*

*Framework* isiyoridhisha, uonevu, dhuluma dhidi ya wananchi, nchi kutokujua nini kinaendelea migodini, Serikali kutokuwa na hisa ndani ya migodi hii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Fundamental Publicy Changes* zinahitaji katika maeneo mbalimbali. Haya yameorodheshwa vizuri sana na Kamati ya Jaji Bomani na kufafanuliwa vizuri na Kamati ya Bunge ya Mheshimiwa Shellukindo na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, kubwa ambalo naliona kwa sasa ni *the way forward;* nini kifanyike?

Masuala haya yamekuwa ya siku nyingi, wananchi waliotuweka madarakani wanataka kujua maamuzi ya Serikali yana maslahi gani kwao? Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho yake akazingatie mambo yafuatayo:-

1. Wapo watu ambao wamedhulimiwa kwa njia mbalimbali; kufukuzwa, kutopata fidia, kunyanyaswa, kuteswa na kadhalika. Itafutwe njia ya haraka kupata orodha ya waathirika na itafutwe njia ya kushughulikia suala hili na fidia zao kufahamika. Serikali ionekane inajali masuala haya. *Quick wins.*

2. Iundwe *High Powered Implementation Committee* nje ya Wizara ya kushughulikia masula yote haya na *Task Force* ya wataalam *on full time basis.* Itabidi *Task Force* hiyo ambayo itakuwa ya kudumu kwa muda Fulani, itoe mapendekezo kwa *Implementation Committee* kuhusu mpangilio wa utekelezaji wa *Reform Programme* ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana utekelezaji ukafikiriwa kwa makini na ujiepushe na *mindset*, la sivyo itakuwa *business as usual* na Mheshimiwa Waziri akubali kwamba, Wizara haina *capacity* hiyo na tumefika hapa kutokana na upungufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo yanahitaji kushughulikiwa sasa hivi kwa upande wa nchi yetu na yapo yale ambayo pia ni kero kwa wawekezaji. Yapo pia ambayo ni *medium term* na yale ya miaka ijayo na yanahitaji kushughulikiwa kwa wakati tofauti/muafaka.

3. *Task Force* hii ni vizuri iwe na *sub-task forces* ambazo zitakuwa *specialized* na kupangiwa kazi na *Implementation Committee.* Kwa mfano, katika maeneo yanayohusu Sera; Sheria; Mikataba; Kodi mbalimbali; fidia kwa wananchi; *Local/External Accounts;* malipo kwa Halmashauri zenye *pressure* ya kuwa na wachimbaji; utendaji wa migodi; *Government Participation;* uwezeshaji wa wananchi kushiriki katika Sekta ya Madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii. Kwa mara nyingine, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi. Pamoja na taarifa nzuri ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Kusimamia Sekta ya Madini; je, Serikali imejipanga vipi juu ya kudhibiti udanganyifu wa mapato halali yatokanayo na wawekezaji hasa wa nje?

Je, Serikali inaweza kutupa *data* kamili zinazoonesha mavuno halali ya madini katika maeneo husika tangu wawekezaji waanze kuvuna; na ni asilimia ngapi?

Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha inawasaidia wachimbaji wadogo na wa kati ili waweze kuendeleza shughuli zao za uchimbaji katika maeneo husika walioyagundua wenyewe, badala ya kuwaondoa na kuwapa wawekezaji?

Serikali haioni kwamba kwa kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati, kutapunguza umaskini uliokithiri miongoni mwa Watanzania hususan wanaoishi maeneo yale?

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kwa kuisimamia vyema Sekta hii ya Madini kutaifanya Tanzania kuweza kujitegemea na kuondokana na migogoro mbalimbali kama migomo ya walimu, wanafunzi na kadhalika; pia tutapuguza vifo vya akina mama na watoto wakati wa uzazi kwa kukosa huduma sahihi kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tunaweza kupata *ambulance* na vituo vya afya bora, elimu bora kwa kuboresha mashule na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya madini ni chachu ya maendeleo ya nchi yoyote ile. Tanzania ni nchi iliyopendelewa na Mwenyezi Mungu kuwa na rasilimali hii muhimu, lakini cha kushangaza Nchi/Serikali imeshindwa kwa kiasi kikubwa, kufaidi rasilimali hii ama kutokana na ubinafsi au ukosefu wa wataalam na kadhalika.

Pamoja na matatizo hayo, bado wananchi wamejitahidi kuwa wachimbaji wadogo na wa kati. Baada ya kugundua madini, wananchi hawa wamejitahidi sana kujenga maeneo yao; mfano ni wale wa *Tanzanite* kule Arusha, ambao kwa kiasi kikubwa wameujenga Mji wa Arusha, lakini baada ya wawekezaji kuja, wamekuwa wakipeleka rasilimali hii kwao, kwani kuna msemo usemao kwamba; kila mwamba ngoma ngozi huivutia kwake na ukweli huu upo wazi.

Rasilimali watu ni msingi sana na hivyo ni vyema Serikali iwekeze kwa wataalam wetu ili wageni washindwe kutuibia na hivyo kupoteza rasilimali hii muhimu.

Madini yetu pamoja na wingi wake na aina mbalimbali, bado pato lake kwa taifa ni dogo. Moja ya sababu ya pato kuwa dogo ni kutoshirikiana na sekta nyingine kama kilimo na chakula. Kwa mfano, makampuni haya yana wafanyakazi wengi na huwa

wanahitaji chakula, lakini cha ajabu vyakula vyao vinaagizwa kutoka nje. Mfano ni Geita Gold Mine na Barrick, ambao huagiza nyama kutoka Kenya wakati hata ng'ombe hao hutoka hapa nchini kwa bei nafuu sana na baadae kuletwa kama *beef/sausage* na kadhalika. Kuku nao wanaagizwa kutoka Kenya na Afrika Kusini. Hii ni hatari na inadidimiza uchumi hasa kwa wale wanaokaa maeneo ya wachimbaji. Mfano pale Geita hali ni ya hatari kwani hali ya wananchi hai-*reflect* madini yaliyopo pale. Ni vyema basi Serikali izuie makamupuni hayo kuagiza vyakula vinavyopatikana pale kama mbogamboga na kadhalika. Hii si tu itawapa soko wananchi, lakini watakuwa na moyo wa kulima zaidi.

Ni wazi kuwa madini yakishachimbwa huisha na hivyo kuacha mashimo makubwa sana, ambayo ni hatari kwa mazingira kwani mvua zikinyesha mashimo yale hujaa maji na baadaye kuleta mmomonyoko wa ardhi, lakini pia wananchi wanaathirika.

Pamoja na ubovu wa mikataba, bado tunasema nchi hii ni changa. Hivi kweli baada ya miaka zaidi ya 40 ya uhuru, bado nchi ni changa na kwamba hatuna wataalam wetu? Wataalam wapo lakini ubinafsi na siasa, zimepelekea hali hii ya kuamini kuwa kila jambo tunali-*politicize;* haya ni makosa.

Kumekuwa na Ripoti nyingi kuhusu madini, hii ikiwa ni ya tano. Napenda kuamini kuwa, Ripoti hii itafanyiwa kazi ili kutoa aibu. Ieleweke kuwa fedha nyingi za wanachi zinatumika kwa Tume hizi lakini hakuna kilichotekelezwa. Naomba ripoti hii itekelezwe mara moja.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Kamati Kuhusu Sekta ya Madini hususan Mgodi wa Buhemba, hairidhishi hata kidogo.

Wanachi wangu wa Buhemba walitegemea kwamba, kilio chao cha siku nyingi kingepata ufumbuzi. Badala yake kamati katika mapendekezo yake yaliyowekwa ukurasa wa 116 mpaka 117, imemrudishia Rais ayapatie ufumbuzi. Hakuna *solution* yoyote ambayo imetolewa kuhusu mazingira yaliyoharibiwa wala *compensation* itakayotolewa kwa wananchi wangu wa Kata ya Buhemba. Hakuna pendekezo lolote kuhusu wizi wa dhahabu au kampuni iliyofunguliwa Mauritius kuficha mali ya Buhemba.

Nilitegemea kwamba, shule na zahanati zilizobomolewa zingejengwa upya. Nilitegemea pia Kamati hii ingejitokeza wazi wazi na kuiomba Serikali itoe tamko rasmi juu ya hatma ya Buhemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani Kamati ingependekeza *CAG* afanye *Audit* ya mgodi wa Buhemba ili Wananchi wa Buhemba wapate faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha nguvu iliyopewa hoja ya *EPA* na hii Ripoti, utaona kwamba ni ubabaishaji tu ndio uliofanyika. Wananchi wanataka kujua hatma ya Buhemba. Napendekeza Kamati Teule ya Bunge iuundwe mapema iwezekanavyo ili itoe ufumbuzi bora wa janga zima la Buhemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono taarifa hii.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuikumbusha Serikali kuwa Sera yetu ya Madini ya Mwaka 1997 inatamka kwamba, Serikali katika kuendeleza Sekta ya Madini, italenga kuvutia na kuiwezesha sekta binafsi kushika hatamu katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Aidha, dhima ya sekta ya umma itakuwa ni kuchochea na kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi katika madini kwa kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Madini hapa nchini.

Kwa hali ilivyo sasa, inadhihirisha sera hii haifuatwi na kama inafuatwa basi ililenga wageni zaidi, yaani wawekezaji. Kwa kiasi kikubwa wachimbaji wadogo wadogo badala ya Serikali kuwawezesha washike hatamu katika utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini yenyewe yanayopatikana, badala yake kila kukicha wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo mbalimbali wanafukuzwa. Baada ya muda mfupi unasikia mwekezaji amepewa eneo hilo, mfano Nyamongo, mpaka leo hawajafidiwa maeneo waliyonyang’anywa, vilevile Kahama na maeneo mengine. Wanasheria wetu wa Serikali wako wapi; kwa nini wananchi na wachimbaji wadogo walioondolewa katika maeneo yao hawalipwi kiwango kinacholingana na ardhi na mali waliyonyang’angwa? Hapa Serikali inaendelea/imeendelea kutengeneza chuki baina yake na wananchi hao, vilevile baina ya wananchi hao na wawekezaji. Mahusiano ni mabaya sana.

Naitaka Serikali iangalie upya suala hili na Kamati zote ikiwemo ya Mboma na ya Kipokola ziangaliwe upya. Tusiwe wasanii kuunda Kamati ili kuleta matarajio ya kupata ufumbuzi wa matatizo yanayohusu madini, halafu ripoti zinahifadhiwa kabatini.

Nikiendelea na Sera hiyo ya 1997, uchambuzi wake unaeleza juu ya mikakati ambayo imeandaliwa na Serikali kwa lengo la kutimiza malengo mengi ikiwemo kujenga mazingira bora na imara ya kiuchumi; kubuni na kutekeleza mfumo wa kodi ambao unafaa kwa wawekezaji na taifa lipate faida. Tumesikia hapa nchi ilipoteza shilingi milioni 885 kwa kuondoa asilimia 15; kuwa na mfumo wa sheria na udhibiti unaokubalika kimataifa, tuige mfano wa waliofaidika na madini yao mfano Botswana; kuboreshwa kwa huduma za kifedha zitakazotolewa kwa Sekta ya Madini; na uanzishwaji wa mifumo rasmi ya masoko; kushirikisha uchimbaji madini katika uchumi wa Taifa na hapa mtakubaliana nami, sekta hii inakua sana. Kwa mfano, haiongezi pato la taifa kwa kuwa kodi haitoshi na sekta hii haina *links* na sekta nyingine mfano Sekta ya Kilimo bado wanaagiza hata nyanya kutoka nje na nyama vilevile.

Vilevile kuunganisha mambo muhimu yanayohusu hifadha ya mazingira na jamii katika mipango endelevu ya maendeleo ya madini. Lengo la sera ni zuri, kwa mfano, maeneo mengi mazingira yameharibika; vyanzo vya maji vinachafuliwa na dawa za kuoshea madini eneo la Nyamongo na vyanzo vya maji vimeharibiwa na sumu hiyo. Mgodi wa Chumvi Uvinza unatumia kuni au magogo badala ya umeme, eneo linaendelea kuwa jangwa na ni hatari sana.

Mwisho, kuhamasisha maendeleo ya watumishi katika Sekta ya Madini; bado sera haijafanyiwa kazi ipasavyo, kwani anacholipwa mfanyakazi kutoka nje ya nchi ni kizuri

sana wakati yupo *level* moja au ya chini kielimu na Mtanzania.  Hili nalo liangaliwe upya.

Serikali ifuate Sera inasema nini na itekeleze yote mazuri yaliyoainishwa katika Sera hii ya Madini ili sekta hii iwe na tija kwa taifa letu.  Tutumie vizuri utajiri tulioupata bure kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mungu kwa kunipa uzima na afya njema hadi muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni moja kati ya nchi chache duniani, zilizobarikiwa kuwa na milki nyingi zenye thamani sana kama vile dhahabu, gesi, *Tanzanite, uranium* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la kushangaza sana ni kwamba, pamoja na mali yote hiyo, bado haijawanufaisha Watanzania walio wengi.  Nasema hivyo kwa sababu ni Watanzania wachache sana ambao kwa kutokuwa na uzalendo na pupa wamejikusanyia mali (pesa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara nyingi tumekuwa tunapiga kelele katika suala zima la kurekebisha sera na sheria ili ziendane na mahitaji ya sasa kwa kuwepo haja ya kuwajali sana wananchi wanaoishi katika maeneo yenye madini ili wafaidike na neema waliyobarikiwa na Muumba wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii imefika ahadi ya kuwaenzi na kuwapa nafasi zaidi hata ya kutolipa kodi wachimbaji wa kigeni wanaoitwa wachimbaji wakubwa.  Hivi tunadhani Mungu kafanya kosa madini au mali kama hii kubarikiwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tujiulize haya manung'uniko ya Watanzania kuhusu kuibiwa miliki yao yatamalizika lini?  Huu mpango wa maeneo makubwa na mazuri yenye madini kupewa wachimbaji wa kigeni unatokana na nini?  Tuseme hapa pana mchezo mbaya wa rushwa kwa wenzetu wanaohusika na shughuli za madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi serikali inasimamia vipi hii misaada wanayopewa Serikali za Mitaa; zile dola laki mbili mbona kuna manung'uniko mengi kwamba baadhi ya Halmashauri bado hawajapata hata senti?

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha Taarifa hiyo hapa Bungeni.

Kwa kuzingatia yaliyomo katika Taarifa kuhusu nafasi ya Tanzania na Watanzania kunufaika na madini yetu, nashauri tena sera mpya ya madini itamke kama ifuatavyo, kama msingi mkuu wa sera yenyewe na sheria mpya ya madini kwamba:-

(a) Tanzania imejaliwa kuwa na madini mengi na ya aina mbalimbali.

(b) Madini hayo ni mali ya Tanzania na wananchi wake wote.

(c) Madini hayo yatachimbwa kwa faida stahili ya nchi yetu na wananchi wake wote.

Haya yakizingatiwa na kutamkwa, basi dira ya Sekta ya Madini ni lazima ibadilishwe na kuondoa dira ya sasa ambayo siyo sahihi. Nilikwishaandika wakati wa Bunge la bajeti, mapendekezo ya dira *(Vision Statement)* na dhima *(Mission Statement).*

Tusiposahihisha sera kwanza kwa kutamka kwa usahihi, sheria na taratibu za uchimbaji madini haziwezi kuwa sawa na kuwa tutaendelea kunyonywa sana.

Napendekeza rasimu ya Sera ya Madini tuione ili tujiridhishe kama ipo sawa. Matokeo ya sera sahihi yatawezesha wafuatao kunufaika na uchimbaji madini:-

(a) Wananchi wote wanaoishi maeneo yenye madini, kwa kupata stahili yao moja kwa moja.
(b) Halmashauri zinazosimamia utawala wa maeneo yenye migodi kwa kupata stahili *(Administration Fees)* yake.

(c) Serikali Kuu kwa kutoza kodi stahili za uchimbaji na mapato ya mauzo ya madini.

Sera sahihi ikikosekana:-

(a) Tutaendelea kusubiri huruma ya wawekezaji kutugawia kiduchu na kwa maamuzi yao, wakati ni mali yetu.

(b) Sheria mbovu ya madini itaendelea.

(c) Tanzania na Watanzania tutaendelea kukosa matunda ya mali yetu na hivyo kuendelea kuwa maskini.

Mikataba yote ya uchimbaji madini itazamwe upya, Bunge lihusike katika kuipitia mikataba hiyo ili tusahihishe tulipokosea. Kazi hii ifanyike baada ya kuwa na sera mpya na sheria mpya.

Sheria mpya ya madini inahitajika baada ya kuweka sera mpya na sahihi.

Vyuo na viwanda vya ukataji madini vinahitajika kwa makusudi. Tayari VETA - Shinyanga ina idara ya mafunzo ya ukataji madini, hivyo iimarishwe na vyuo zaidi viongezwe ili tupate wataalam/mafundi mchundo wa fani hii. Sera mpya ya madini ilitamke suala la mafunzo kama haya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi kwa Tume ya Jaji Bomani iliyoteuliwa na Rais, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Naipongeza sana Kamati ya Bunge ya Madini chini ya Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Shellukindo, kwa kazi kubwa na nzuri.

Sekta hii ya madini inaweza kabisa kubadili maisha ya Watanzania yakawa mazuri ndani ya muda mfupi na kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa kama siyo kuuondoa kabisa.

Wizara ifanye juhudi za pekee za kuleta Sheria ya Madini hapa Bungeni ifanyiwe marekebisho mara moja na kurekebisha Sera za Madini ambazo zimetuumiza kwa muda mrefu sisi Watanzania.

Kwa muda mrefu wawekezaji wamekuwa wanavuna madini yetu, kuyapeleka nje na kunufaisha nchi zao bila huruma kwa Watanzania.

Tunao wasomi wenye ujuzi kwenye Sekta ya Madini lakini Serikali haiwatumii kuwa kama jicho kwenye migodi hapa nchini. Watanzania wanaofanya kazi migodini ni kazi za kufagia na kuhudumia chai; hawajui chochote kinachoendea. Kila mgodi awepo Mtanzania mtaalam wa kuangalia mali zetu.

Wawekezaji wananyanyasa sana wananchi waliowatoa kwenye eneo la machimbo; wanawaona kama *intruders* wanawazuia hata kupita jirani na mgodi husika. Wakati mwingine mwekezaji anawafungulia mbwa wananchi. Huu ni unyanyasaji wa hali ya juu. Wawekezaji waheshimu nchi yetu na watu wake, pesa yao isije kututesa ndani ya nchi yetu. Serikali iweke utaratibu kuwa atakayethibitika kufanya kitendo chochote cha kumtesa, kumwonea au kumnyanyasa mwananchi, apewe saa 12 kuondoka nchini.

Mchango wa huduma za jamii kwa wananchi wanaoishi kuzunguka migodi ya madini; kiasi kinachotolewa kwa Halmashauri cha 200,000,000 kwa mwaka ni kidogo sana. Kuwepo mpango unaoeleweka wa kutoa asilimia 20 kati ya kile wawekezaji wanachopata. Utoaji wa fedha hiyo ni lazima; siyo ombi wala hiari. Kuwepo kubembelezana au kuzungumzia huko, baada ya kutolewa agizo anayeshindwa kutekeleza kwa muda achukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kupigwa faini. Ni aibu; wananchi wanaoishi jirani na migodi wana hali ngumu sana, nyumba zao zinasikitisha wakati utajiri upo eneo lao.

Uchimbaji wa madini unasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Licha ya madini kuondolewa, tunaachiwa mashimo makubwa ambayo ni hatari kwa watoto, mifugo na kadhalika. Serikali ihakikishe kabla ya muwekezaji kuanza uchimbaji mahali popote, alipe kwanza gharama za uharibifu wa mazingira. Anapohama/kumaliza kuchimba, alazimike kufukia kwanza shimo moja kabla ya kuanza kuchimba eneo lingine. *Disposal* ya uchafu unaotokana na kusafirisha madini ifanywe kwa umakini mkubwa bila kuathiri maisha ya wasamaria.

Serikali ihakikishe madini yote yanasafishwa hapa nchini na hakuna kusafirisha madini ghafi. Tujue thamani ya madini yetu hapa hapa. Tuwe na wataalam wetu wenye ujuzi wa kutosha kwenye eneo la kusafishia madini ili kutathmini idadi, gharama na pato

halisi la madini yetu na tuweze kupata gawio tunalostahili kama serikali, kama Watanzania.

Fidia kwa wananchi wanaondolewa kwenye maeneo ya machimbo zinazotolewa ziendane na thamani ya ardhi waliyoondolewa na kilichopatikana pale. Haiwezekani mchimbaji wa madini alipe fidia sawa na mwekezaji wa kilimo cha pamba au kahawa; haki hapa iko wapi?

Wanaoondolewa wote wajengewe nyumba bora maeneo/maskani mapya na huduma zote za jamii ziwekwe kabla ya kuanza kazi yoyote ya uchimbaji kwa mwekezaji aliyewahamisha.

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri ili aweze ku-*react*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kusema kweli kwa sababu ya nafasi yenyewe ya taarifa ilivyo ni kwamba, sisi tumepokea huu ni ushauri ambao Waheshimiwa Wabunge wameutoa kwa nyongeza ya ushauri wote unaotolewa na wadau kwa nafasi yao kama Wabunge. Hivyo, mimi nilikuwa ninaomba nitumie nafasi hii uliyonipa kuelezea machache tu katika utekelezaji wa baadhi ya mambo na kufafanua mengine. Mara kwa mara tumekuwa tunazungumzia hapa kwenye Bunge lako hili Tukufu kuhusu umuhimu wa kuanza kuifanyia kazi kwa haraka sana Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, limejitokeza kwa mfano suala la tofauti katika *withholding tax* baina ile iliyopo kwenye sheria na ile iliyopo kwenye mikataba na kadhalika. Tukirejea nyuma ni kwamba, masuala haya yalianza kushughulikiwa labda kwenye Sera ya 1997 na Sheria ya 1998, lakini kwa mazingira maalum yaliyokuwepo wakati ule; *investment climate* na *investment incentives* ambayo kusema kweli katika miaka kumi hii tuliyokaa nayo, tumepata nafasi ya kujifunza na kujua kwamba wapi tunatakiwa kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kusema hapa nikijibu maswali kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kwamba, tumeanza kuyafanyia kazi na tunaanza kuifanyia kazi rasimu ya Muswada wa Sheria ambayo tunataraji labda mwezi wa nne utakuwa Bungeni. Ninafikiria kwamba, pamoja na huo ushauri aliopewa Rais kwenye Kamati hii aliyoiteua, niseme hapa hapa kwamba mambo mengi yaliyotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge ni ushauri ambao kusema kweli utazingatiwa sana katika kuandaa rasimu hiyo ya Muswada wa Sheria hiyo ya Madini, ambayo tunakusudia kuileta Bungeni mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumzie pia suala ambalo limezungumzwa na Kamati lakini pia amelileta Mzee Shellukindo na mimi nilikuwa nimekusudia nilisemee kidogo, ni suala la umiliki wa migodi. Kusema kweli ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ni jambo la kulitazama hasa pale Mzee Mzindakaya aliposema kwamba, hawa wanaokuja kumiliki migodi hii na mitaji yao wanaenda kukopa. Wanaenda kukopa wakiwa wanatarajia *a certain retainer in investment* na hili

jambo tulilisema wakati wa Hotuba ya Bajeti kwamba ni wakati ambapo na sisi sasa kama Taifa, tuanze kuweka mikakati ya makusudi ya kuboresha siyo tu utaalam wetu lakini *capacity* ya utaalam wa kuingia kwenye masuala haya ya *negotiations*, lakini pia kwenye masuala ya kuangalia ni wapi tunaweza kuingia na tukawa sisi wenyewe wamiliki kwa ufahamu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli nadhani wenzetu hawa wanapokuja wa nia ya kuwekeza unakuta wamekuja na taaluma na *exposure* ambayo ni pana na ni kubwa; unajiuliza sijui kama tunavamia haya mambo kwa namna gain? Kitu kimoja kikubwa ambacho tunakifahamu ni kwamba, tunahitaji kuwa na *exposure* zaidi na ufahamu zaidi na *specialization* pia katika masuala haya ya *negotiations, especially* kwenye masuala ya *Mining Development Agreements* na *Mining Development Contract* kwa kuzingatia *experience* za watu wa Ghana, Botswana, South Africa, India, China na ile kitu ambayo wataalam kwa lugha ya Kiingereza wanasema *the importation of technology, capital, the distinguish and both of them.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu naomba nizungumzie suala dogo ambalo limezungumzwa na nimelifanyia kazi kwa maagizo ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ni suala la ulipaji wa fidia. Waheshimiwa Wabunge, ushauri wenu ni wa dhati, ninaushukuru kwa sababu nimeona kwenye *theory* ni tofauti kusema kweli. Kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Rais alipompa nafasi ya kuwa kwenye Kamati, ameenda kujifunza mambo mengi ambayo alikuwa anayaona *in theory* na mimi kusema kweli ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa nafasi hii niliyopata, nimeenda kukuta mambo mengi kwenye Sekta ya Madini tofauti na vile tunavyoyafahamu. Jambo mojawapo ni ulipaji wa fidia, suala ambalo kusema kweli Sheria ya Madini inabidi iliingilie kwa kina zaidi na ni ushauri ambao umetolewa na Kamati na sisi wenyewe tumeanza kuufanyia kazi, hasa kwa kuangalia namna tunavyoioanisha na Sheria ya Ardhi na haya masuala yote kama alivyosema Mheshimiwa Simbachawene ya *mining rights vs surface rights* na kadhalika.

Ndugu zangu tukubaliane kwamba, hata hivi vipengele vya sheria vilikuwepo, vinaingia na matatizo si kwa sababu ya ukwasi wa sheria lakini pia pana matatizo kabisa ya nia ya dhati ya wale watekelezaji wa ile sheria ya fidia. Wengine tumekwenda kule tunalifanyia kazi hilo suala la Buzwagi, matatizo mengine kweli ni ya ujanja wa ndani kwa ndani lakini mengine yanatokana na uzembe tu katika utekelezaji kwa yale ambayo usimamizi wake upo chini ya mamlaka yetu sisi wenyewe. Tunaangalia kwa upana ni wapi ambapo kusema kweli sheria inataka iwe na ukali zaidi na ni namna gani ambavyo sheria italinda maslahi ya wale Watanzania wanaolipwa fidia, ambao mara nyingi wanakuwa hawana hatia na ufahamu wao katika masuala haya unakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la wachimbaji wadogo; ninaomba niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeanza kulifanyia kazi kama nilivyosema asubuhi ni juzi tu tumetoka kwenye maeneo ya Kahama, Geita na maeneo ya Kwimba kwa Mama Nyawazwa, tulikwenda kuangalia ni namna gani ambavyo Serikali inaweza ikaingiza hii nadharia ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wadogo *in practice.* Moja katika hayo kuna Mbunge hapa amechangia amesema kwamba, Serikali

iangalie namna ya kuwapa pampu kwa sababu vikwazo wanavyoingia navyo katika utendaji wao wa kazi mara nyingine ni vitu ambavyo ni *basic* lakini kwa sababu ya kukosa mtaji mdogo tu wa milioni 15, 20, 30 wanashindwa kuendelea. Unakuta mgodi umekwama, umejaa maji lakini wanaona kwamba chini dhahabu ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunayaangalia hayo yote, tutayafanyia kazi na wawekezaji wakubwa na wadogo. Pia tunapitia upya suala la utoaji wa leseni ambalo nadhani sheria inabidi tuiangalie ili impe mamlaka zaidi Waziri wa Nishati na Madini, kuingilia kati pale ambapo maslahi ya Taifa yanaingia kwenye *conflict* na maslahi ya wawekezaji binafsi. Nadhani hilo ni eneo ambayo tumekwenda huko na tunaendelea kusema tutafanya utafiti ili tukileta sheria mwakani iwe ni sheria ambayo inazingatia yote haya mliyotuambia.

Vilevile iwe ni sheria ambayo inazingatia maslahi mapana ya wadau wote wa Sekta ya Madini; wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa, kila mmoja kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kutoa majumuisho kuhusu mjadala ambao ulikuwa unaendelea hapa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, naomba nianze kwa kuwatambua wale ambao wamechangia kwa kuzungumza, lakini pia na wale ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza wa kwanza alikuwa Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, huyu ni Waziri Kivuli, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mwera C. Nyanguru, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka Mzelu, Mheshimiwa George B. Simbachawene na hatimaye Mheshimiwa Adam K. Malima, ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni wafuatao; Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa … *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unaweza kuendelea tu halafu utawataja baadaye, mwombe Naibu Waziri akusaidie.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi nilikuwa ninaweka kumbukumbu sawa. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhwanya, Mheshimiwa Bakari Shamisi Faki, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge, kwanza na kwa ujumla kabisa, kuipongeza kwa mara nyingine tena, Kamati ya Rais iliyoundwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, kwa jinsi ambavyo wamefanya kazi nzuri. Shukrani zetu kwa niaba ya Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini tulisema wakati tunawasilisha bajeti yetu ya makadirio mwezi wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi, wamechangia kwa uchungu mkubwa na kwa nia moja tu, yaani kwa nia ya kuiboresha Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuitambua na kuipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ametusaidia kama Mheshimiwa Naibu Spika alivyosema asubuhi, kutuongoza na kuturahisishia mjadala huu ambao kwa kweli unahusu maslahi ya Taifa. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Nishati na Madini na Kamati yako nzima, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, hii ni Taarifa ya Kamati ya Mheshimiwa Rais, kwa ujumla yapo mambo mengi sana ambayo yameongelewa. Hitimisho la yote ni kwamba, Serikali kwa hatua hii tunachukua maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambao sisi tunaamini kwamba ni wadau wakubwa na muhimu sana katika kuboresha mambo mbalimbali lakini kwa leo tumeongelea Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, zipo hoja nyingi sana alizozisema ambazo zimeturahisishia pia sisi Serikali kuweza kuona uelekeo wa jinsi ambavyo tunaweza kuzifanyia kazi.

Nipende kusema machache miongoni mwa haya ambayo amesema nianze na hili ambalo hivi karibuni Mheshimiwa Kabwe Zitto alikuwa amesimama kulitolea taarifa kuhusu uchunguzi maalumu juu ya jinsi Serikali ilivyouza hisa zake na mahali fedha hizi zilipokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na imani kama ambavyo mmeiamini Serikali ilipoahidi kuwasilisha taarifa yake na ikaileta. Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tuijadili hapa na tunawahakikishieni maoni na ushauri unaotolewa hapa; kwetu sisi ni vitendea kazi na nyenzo muhimu sana katika kuboresha Sera na Sheria ya Madini ambapo tumejiwekea ratiba kufikia mwezi wa nne mwaka kesho, lazima jambo hili liwe limeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka nitumie nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwahakikishieni kwamba, tutazingatia maoni na ushauri wenu wa dhati kabisa na tutakwenda kuufanyia kazi.

Zipo hoja mbalimbali na nyingine Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuhusu masuala ya fidia kwa wachimbaji wadogo. Kuhusu suala la usafirishaji wa madini ya vito ni zito na historia inaonyesha kwamba limejadiliwa kwa muda mrefu kidogo. Sisi tunaamini hatujachelewa sana, pamoja na kwamba jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu, bado ni imani yetu kwamba, tukijipanga kuanzia haya marekebisho tunayoifanyia Sekta ya Madini kwa ujumla tuna fursa nzuri. Kwa takwimu tulizonazo, hata huu uchimbaji wa Madini ya *Tanzanite* acha madini mengine ya vito, siyo wa kuisha mwaka 2012. Takwimu tunazo, bado kuna safari ndefu ya kuendelea kuyachimba haya madini, cha msingi ni sisi kuendelea kujipanga vizuri.

Ninaamini kwamba, tukijipanga vizuri tutafaidika sana. Sisi Tanzania leo katika historia ya uchimbaji madini duniani, hatuna zaidi ya takribani miaka kumi *large scale mining.* Tunapojilinganisha na nchi kama Botwana, ambayo ina zaidi ya miaka 50, unajilinganisha na nchini kama ya Ghana ambayo ina zaidi ya miaka 100, wenzetu kama wa Afrika Kusini ambao wana miaka 100 na pengine zaidi, bado tunaona kwamba hatujachelewa. *(Makofi)*

Ninataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kabisa kwamba, zipo nchi ambazo zilitutangulia sana katika shughuli za madini, leo wanakuja kujifunza kwetu mojawapo ni Ghana. Kwa hiyo, tunasema zipo kasoro katika mfumo wetu wa miaka 100 hii tuliyofanya, lakini bado tuna fursa kama Taifa ya kurekebisha kasoro hizi na hatimaye kunufaika. Tuna imani Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria. Sisi tunasema ushauri tunaoupata leo unaotokana na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Rais aliyoiunda mwaka jana, tunaamini kwamba unaitoa Tanzania hapa ilipo kuipeleka hatua nyingine ya mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja kubwa na nzito nikadhani ni vyema kuisema kwa mfano ya kuwanyang'anya baadhi ya wachimbaji migodi na kuwakabidhi wananchi. Sisi kama taifa, nadhani ni jambo jema kulisema walau kuelewa tuna msimamo gani kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaondolea hofu Watanzania wenzangu kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, tupo makini hizi kasoro tutazirekebisha. Nadhani hatujafikia mahali pa kusema tuanze kuwanyang'anya wawekezaji waliopo kwa sababu tumeingia nao mkataba kwa mazingira ambayo tulikuwa na dhamira sahihi na tukaweka

taratibu nzuri za kuwapa leseni hizi. Nadhani tukishafikia hatua ya kusema tuwanyang'anye, tutakuwa tume-*extreme to the end* na ningeomba tusifikie hatua hiyo, lakini tuhakikishe tu kwamba tuna fursa ya kurekebisha. Ninarudia tena kusema, yapo mambo tumepoteza kwa sababu ya kasoro zilizopo lakini hatujachelewa sana, bado tunahakikisha kwamba tutarekebisha hizi kasoro na tutaendelea kujiweka sawa kuhakikisha kwamba hizi kasoro zinaboreshwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetolewa na ninamshukuru sana Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwamba, hili zoezi litakapokuwa linaendelea la kurekebisha Sera na Sheria za Madini, tafadhali tukumbuke kwamba, kuna Sera na Sheria ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2000.

Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa tunakushukuru, tutazingatia. Ulisema kwamba, nadhani Kamati ilipitiwa kuoanisha na kinachosemwa na Sera hii ya Mwaka 2004, ambayo inahusu kuwawezesha kiuchumi Watanzania na ndiyo maana haikujitokeza hapa. Tunashukuru ndiyo manufaa ya mijadala kama hii kwenye hatua kama hii. Tunafahamu baada ya hapa tutatoka nje, wapo wadau wengine nje ya Bunge hili Tukufu watapata nafasi, zipo taasisi mbalimbali na zipo asasi za Kiserikali zisizo za Kiserikali. Mjumuiko wa haya maoni na ushauri ambao watatupa wao tuna imani kwamba, watatufanya tutengeneze kitu kilicho bora zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado tuna imani kwamba tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetolewa ya kwamba, madini yote ya vito yakatwe hapa ndani. Nakumbuka pia Baba yangu Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya alisema, kwa nini madini yote yasiwe *processed* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja nzuri na tumekuwa tukisema hapa wakati mwingine tunapokuwa tunajibu maswali, hili lina pande mbili; sisi kama Taifa lina misingi yake na mmojawapo ni kuendesha shughuli za madini. Tumesema Sera yetu ya Madini, naamini hapa tunafanya marekebisho sasa hivi hatutaki kuondoa ile dhana ya ushiriki wa Sekta Binafsi. Nina imani kwamba, wapo Watanzania wenye uwezo, wakikaa na kujipanga vizuri na wakidhamiria kulisaidia Taifa kupitia majaliwa ya Mwenyezi Mungu, aliyowajaalia wao kuwa na uwezo wa kiuchumi, tunaweza kujenga viwanda vya ku-*process* hapa Tanzania. Kwa hiyo, wito wangu bado nasisitiza kwa niaba ya Serikali kwamba, wapo Watanzania wanaoweza kutusaidia sana kututoa hapa.

Zipo nchi zimefanikiwa lakini msingi wa yote kama alivyosema Mheshimiwa George Simbachawene ni kwamba, mtaji wetu sisi Watanzania ni Utanzania wetu. Ninaamini pia mchango wa ushiriki wetu Watanzania kuitoa Tanzania ilipo hapa, unategemea sana ushiriki wetu katika hili. Mheshimiwa Zitto Kabwe, alikuwa anatukumbusha asubuhi mgodi mkubwa wa *Nickel* pale Kabanga, hawa wote wanahitaji kuwa na *refinery plants* ambazo zinaweza kufanya kazi na mimi ninaamini kwa sababu masuala haya si fedha zao za mfukoni, wanatumia *projects* ambazo zinachukua mkopo kwenye benki na ni jambo ambalo linawezekana. Bado ninaamini kwamba, Watanzania

wana fursa, nadhani tuendelee kuyaboresha haya mazingira kwa ajili ya ushiriki wa Watanzania na hata kwenye vito hivyo hivyo.

Leo hii tukapitisha Sheria tuseme kwamba madini yote ya vito yasipelekwe nje; tumejiandaa kiasi gani? Hoja inakuja, ushiriki huu wa maandalizi ni wetu sote, sisi Serikali tunasema tusifanye biashara moja kwa moja, hata leo tukipitisha Sheria hapa lazima tutategemea Sekta Binafsi ya Watanzania. Ninaamini kwamba, Watanzania wapo na hata ndani ya Bunge hili wapo wafanyabiashara wazuri, hebu tuliangalie kwa mtazamo wa Taifa kwa sababu ni manufaa yale ya kibiashara, hatuwezi kupiga hatua kubwa zaidi kama Watanzania watajitokeza waka-*form consortium* wakatengeneza kampuni hata kwa kuunganisha nguvu zao tukaja kujenga *refinery plants*.

Leo tunalaumiana hapa udongo wa Bulyanhulu, Kamati ya Nishati na Madini iliyokwenda pale juzi imeona kazi inayofanyika pale; ule mchanga hivi ni hatuwezi kufanya sisi wenyewe kupitia wawekezaji wetu wa ndani wakajiunga kupitia Shirikisho la Wafanyabiashara wa Tanzania wakaandika *proposal* nzuri wakaipeleka tukapata? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaamini kwamba, mambo haya yanawezekana na ni imani yetu kwamba, tukiendelea kufanya vile na sisi tuna utaratibu na mpango wa kuhamasishana. Tuwaite *TCI* tukae nao na tuone ni namna gani tunaweza kusaidiana katika kusukuma nchi kwa kupitia Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa kwamba Taifa halijanufaika na madini hata kidogo, ninaelewa *statement* hizi zinatokana na mtazamo wa ujumla lakini nataka niseme ni bahati nzuri siwezi kusema ni bahati mbaya. Mimi ninatoka kwenye maeneo ya uchimbaji madini, mwaka 1991 nilikwenda Bulyanhulu pale kulikuwa na wachimbaji wadogo.

Mwaka 1987 nilikwenda Nyamongo, siyo manufaa ya moja kwa moja, kasoro iliyopo hapa nakubaliana na Mheshimiwa Zitto Kabwe ile *forward and backward linkages* kwenye uchumi mpana hatujaiweka sana. Kasoro ambayo sasa hivi tunaishughulikia lakini kusema kwamba hatujanufaika sitaki kwenda mbali, kwa sababu nipo hapa kwenye *podium.*

Kama tunategemea hali halisi ya mambo yanavyobadilika kwenye maeneo ya migodi Wilaya ya Sengerema inazaliwa kutokana na Wilaya ya Geita wakati Kampuni ya Buckreef inafanya kazi vizuri. Wilaya ya Sengerema imeundwa rasmi mwaka 1975. Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa unakumbuka, Wilaya ya Sengerema ilikuwa na kasi ndogo na iliipita Geita, baada ya kufifia uzalishaji wa dhahabu pale Geita. Nawaambieni baada ya uzalishaji wa migodi ya dhahabu kurudi Geita, basi Sengerema imepitwa na Geita.

Nataka niwaambie nilipokwenda Kakola mwaka 1991 haikuwa hivyo. Leo maisha ya Shinyanga na Kahama ni ghali kuliko Makao Makuu ya Mikoa ya Tanzania kwa sababu *purchasing power* ya wananchi wa maeneo hayo imeongezeka. Kwa hiyo, uwezo wa kifedha umeongezeka kutokana na matokeo mazuri yanayotokana na shughuli

nzima zinazofanyika, mojawapo ikiwa ni shughuli za migodi. Ukienda pale Kakola leo kuna *Guest House*, kile kilikuwa ni kijiji tunafahamu maisha yaliyokuwa pale.

Ukienda Nyamongo leo, Mheshimiwa Zitto Kabwe tunakubaliana umetoka pale juzi si hivyo, sasa haya siyo mambo ya moja kwa moja yanayoonekana katika uchumi. Yapo matokeo hapa lakini nataka tuunganishe tulisimamie vizuri jambo hili, namna ambayo uchumi wetu unasimama kupitia Sekta ya Madini. *(Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasema, manufaa yapo nenda pale Kahama, maisha ya pale utadhani upo Dar es Salaam; yote hii ni kwa sababu watu wengine hawaulizi chenji, ukikodi teksi watu hawataki kuuliza chenji. Lipo jambo la ajira; migodi hii leo inaajiri zaidi ya Watanzania 10,000, tuseme ukweli Watanzania mpaka sasa hivi kweli tuna *options* nyingi; tunasema hili kundi la Watanzania 10,000 ambao wanategemewa na familia zao, wengi wao wanaendesha magari, wengine wanafanya biashara, wengine wana maduka yao. Kwa sababu nyingine tu ukisema tufunge hili kundi la watu 10,000 lote likose kazi, je, tuna *options* nyingi kweli za kuwa na kazi? Kwa hiyo, nataka kuonyesha picha ya kwamba migodi hii pamoja na kasoro tunanufaika.

Juzi wakati wafanyakazi wa Mgodi wa Bulyanhulu wamegoma, nilikwenda pale tarehe 09 nikawa naongea nao; ni jambo la kisheria wapo watu wengine walikuwa wanajipanga kwenye mageti wanasubiri kuajiriwa. Inapelekea picha gani? Inapelekea picha kwamba kuna mambo ya kuzingatia kabla hatujafanya maamuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwape matumaini Waheshimiwa Wabunge kwamba, tupo makini na hatuogopi kufanya maamuzi magumu. Tanzania ya leo siyo ya kesho, neema imejaa kupitia Sekta ya Madini na tuna uhakika. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nihitimishe kwa kusema katika kuioboresha Sekta ya Madini kupitia Sera na Sheria, tutazingatia kuhakikisha kwamba tunaongeza manufaa ya taifa, lakini pia misingi ya Utawala Bora kwa maana ya kuheshimu Utawala wa Sheria. Tutalizingatia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamesema, kuna mambo mengi wameyaona wakati wanapita sehemu mbalimbali zikiwemo Kamati. Mambo mengine yapo Mahakamani si rahisi sana kwa nchi kama yetu ambayo hatuendeshi nchi kiubabe, mkitofautiana mkafikishana mbele ya chombo cha Mahakama ambacho ni mhimili mmojawapo wa dola, haiwezekani mhimili mwingine kwenda kuingilia. Unasubiri kwanza shughuli yenyewe iishe kwa utaratibu huo uliopo kwa kupitia mhimili ambao unatambulika Kisheria. Kwa hiyo, huo ni upungufu lakini tunasema kama hatuyawasilishi vizuri kwa wananchi na sisi kama Viongozi tunaweza kupeleka chuki kwa wananchi, wakajenga hisia mbaya kwa mambo mengine ambayo ni ya msingi kabisa.

Katika mabadiliko haya ya Sera ya Sheria, hatuwaogopi wawekezaji. Leo tunaangalia migodi sita mikubwa ambayo inamilikiwa na wawekezaji wa nje, sisi kwa

takwimu tulizonazo Wizara ya Nishati na Madini, leseni nyingi zimeshikwa na Watanzania hawa wapo wa viwango tofauti tofauti; wapo wadogo na wa kati na tunaamini hawa wa kati watakwenda watakuwa wakubwa. Sera na Sheria tunayotaka kuitunga leo hatutaki iwe *biased* kwa kuangalia leo wanao-*dominate* soko kesho watakuwa Watanzania hawa, tutavurugana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba, tutazingatia *international best practice*, tunataka tuifanye Tanzania iendelee kuwa kivutio kwa ku-*balance interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Nimrod Mkono tumekusikia, suala la Buhemba tunalishughulikia na tunaendelea. Kimsingi, mojawapo ya suala la malipo tumeshafikia mbali sana, tutatoa taarifa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na hayo makofi maana yake watu wameridhishwa na mchango wako mdogo. Kwa ujumla ni kwamba, michango yote imeshakusanywa na Wizara na watakwenda kuifanyia kazi. Hicho kilichokuwa kikifanyika ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mnachangia na mnaongezea kile ambacho kimeshafanywa na Kamati ambayo iliundwa na Mheshimiwa Rais. Sasa nyongeza ambayo imetoka leo basi Wizara au Serikali itakaa kitako ili iweze kuifanyia kazi.

Kuna mwongozo ambao Mheshimiwa Zitto Kabwe ameutoa, naye nimwambie kwamba, nitampa majibu katika vikao vitakavyokuja hapo baadaye, yaani kuanzia kesho halafu tuone ni namna gani. Nadhani kwa kuanzia, tuiache Wizara au Serikali waanze ku-*react* kwenye haya ambayo tayari wameshayapata kwa sababu ni haki yetu kama Bunge kuunda hizi Kamati Teule na kuweza kuchunguza kwa undani, masuala mbalimbali ambayo yanajitokeza.

Kwa hayo, machache nadhani muda wa shughuli zetu umekamilika. Kwa hiyo, napenda niahirishe kikao hiki mpaka kesho asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Oktoba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*